# Kiswahili

## Kidato cha 6

## Mchepuo wa Lugha (LFK)

## Mwongozo wa Mwalimu

© 2022 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi
Haki zote zimehifadhiwa.
Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi.
Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi wakati yaliyomo yamenukuliwa.

## DIBAJI

Mwalimu mpendwa,

Bodi ya Rwandaya Elimu ya Msingiinayo heshima kwa kutoa mwongozo wa mwalimu kwa kidato cha sita, mchepuo wa lugha, katika ngazi ya juu ya elimu ya sekondari. Mwongozo huu ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo. Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira. Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji.

Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo. Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi. Wanafunzi, kwa msaada wa walimu, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao binafsi bali pia hata kwa taifa. Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu. Katika mtaala unaoegemea uwezo, ujifunzaji huchukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema. Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

- Katika mtazamo huu, ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako kama mwalimu litakuwa : Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa;
- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano ya wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwaufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa

kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu;

- Kushirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi;
- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano;
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti;
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi;

Kuutumia mwongozo huu kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi. Ingawa mwongozo huu wa mwalimu  una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini.

Napenda, kwa moyo wote, kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mwalimu, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi ( REB/CTLR) walioandaa mchakato wa kazi hii tangu ilipoanzishwa. Pongezi maalum ziwaendee walimu wa ngazi tofauti kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili. Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, REB.**

## SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaana kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mwalimu. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu za kwanza ni kwa wafanyakazi wa Bodi ya Rwandaya Elimu ya Msingi walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Pia napenda kutoa shukrani kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikamilisha kitabu hiki.

**MURUNGI Joan**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana ( CTLR-REB)**

**YALIYOMO**

DIBAJI ... ii

SHUKRANI ... iv

YALIYOMO ... v

SEHEMU I. UTANGULIZI WA JUMLA ... 8

1.1. Muundo wa Mwongozo wa Mwalimu ... 8

1.2 Muelekeo wa ufundishaji ... 8

1.2. 1. Mwelekeo wa Kuendeleza Uwezo ... 9

1.2.2 Kuingizwa kwa Masuala mtambuka katika somo. ... 10

1.2.3. Uangalizi wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum ... 10

1.2.4 Mwongozo wa Tathmini ... 10

1.2.5Mbinu na Mikakati ya Kuendeleza Ufundishaji na Ujifunzaji ... 11

1.2.6 Mbinu za Ufundishaji ZinazokuzaShughuli ya UjifunzajiShirikishi ... 12

MADA KUU YA 1 : FASIHI KATIKA KISWAHILI ... 18

MADA NDOGO YA 1: UFAFANUZI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI ... 18

1.1.uwezo upatikanao katika mada ... 18

1.2 .Ujuzi wa awali ... 18

1.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake ... 18

1.3.1.Kidokezo cha mada ... 18

1.3.2 Maelekezo ya kidokezo cha mada ... 18

1.4. Orodha ya masomo ... 19

SOMO LA 1: DHANA YA TANZU ZA FASIHI ANDISHI ... 23

SOMO LA 2: UTANZU WA HADITHI FUPI ... 29

SOMO LA 3: UTANZU WA RIWAYA ... 35

SOMO LA 4: UTANZU WA TAMTHILIYA ... 41

SOMO LA 5: UTANZU WA USHAIRI ... 49

1.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ... 55

1.5.1. Maelezo ya Ziada kwa Mwanafunzi ... 55

1.5.2. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu ... 58

1.6 TATHMINI YA MADA YA KWANZA ... 60

1.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI ... 64

1.7.1 Kazi za urekebishaji ... 64

1.7.2 Kazi za uimarishaji ... 65
1.7.3 Kazi kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka ... 67
MADA KUU YA 2 : FASIHI KATIKA KISWAHILI ... 67
MADA NDOGO YA 2: UHAKIKI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI ... 67
2.1. Uwezo upatikanao katika mada ... 67
2.2. Ujuzi wa awali ... 67
2.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake ... 68
2.3.1. Kidokezo cha mada ... 68
2.3.2. Maelekezo ya kidokezo cha mada ... 68
2.5. Orodha ya masomo ... 68
SOMO LA 1: DHANA YA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI ... 73
SOMO LA 2: UHAKIKI WA HADITHI FUPI ... 77
SOMO LA 3: UHAKIKI WA MASHAIRI ... 85
SOMO LA 4: UHAKIKI WA TAMTHILIYA ... 90
SOMO LA 5: UHAKIKI WA RIWAYA ... 96
2.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ... 102
2.5.1. Maelezo ya Ziada kwa Mwanafunzi ... 102
2.5.2. Maelekezo kwa Mwalimu ... 109
2.6. TATHMINI YA MADA YA PILI ... 120
2.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI ... 124
2.7.1. Kazi za urekebishaji ... 124
2.7.2. Kazi za uimarishaji ... 125
2.7.3. Kazi kwa wanafunzi wenye kipawa na kipaji ... 127
MADA KUU YA 3 : UBUNAJI ... 129
MADA NDOGO YA 3: HOTUBA NA UFUPISHO ... 129
3.1. Uwezo upatikanao katika mada ... 129
3.2. Ujuzi wa awali ... 129
3.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake ... 129
3.3.1. Kidokezo cha mada ... 129
3.3.2. Maelekezo ya kidokezo cha mada ... 130
3.3. Orodha ya masomo ... 130
SOMO LA 1: DHANA YA HOTUBA NA MWONGOZO WA UTUNGAJI WAKE ... 134

SOMO LA 2: UCHAMBUZI WA HOTUBA ........ 142
SOMO LA 3: DHANA YA UFUPISHO NA SIFA ZAKE ........ 148
SOMO LA 4: MBINU ZA UFUPISHO ........ 154
3.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ........ 160
3.5.1 Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi ........ 160
3.5.2 Maelekezo ya ziada kwa mwalimu ........ 161
3.6 TATHMINI YA MADA YA MADA YA TATU ........ 164
3.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI ........ 167
3.7.1. Kazi za urekebishaji ........ 168
3.7.2.Kazi za uimarishaji ........ 169
3.7.3. Kazi kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka ........ 170
MADA KUU YA 4 : UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO ........ 171
MADA NDOGO YA 4: MDAHALO NA MJADALA ........ 171
4.1. Uwezo upatikanao katika mada ........ 171
4.2. Ujuzi wa awali ........ 171
4.3. Kidokezo ........ 172
4.3.1. Kidokezo cha mada na maelekezo yake ........ 172
4.3.2. Maelekezo ya kidokezo cha mada ........ 172
4.4. Orodha ya masomo ........ 172
SOMO LA 1: DHANA YA MDAHALO NA MWONGOZO WAKE ........ 175
SOMO LA 2: DHANA YA MJADALA NA MWONGOZO WAKE ........ 183
4.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI ........ 189
4.5.1 Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi ........ 189
4.5.2 Maelekezo ya ziada kwa mwalimu ........ 190
MAREJEO ........ 193

# SEHEMU I. UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1. Muundo wa Mwongozo wa Mwalimu

Kitabu hiki ni mwongozo wa mwalimu katika mchakato wa ufundishaji wa somo la Kiswahili, kidato cha sita, mchepuo wa lugha katika shule za sekondari nchini Rwanda. Kimetayarishwa kwa mwelekeo wa uwezo unaoegemea mtaala. Mwongozo wa mwalimu huu umezingatia mada muhimunne kama ifuatavyo:

1. Ufafanuzi wa Tanzu za Fasihi Andishi katika Kiswahili
2. Uhakiki wa Tanzu za Fasihi Andishi
3. Hotuba na Ufupisho
4. Mdahalo na Mjadala

Kila mada hujigawa katika mada ndogo na kila mada ndogo katika masomo mbalimbali. Kila somo hufuata muundo ufuatao:

1.1. Kusoma vifungu vya habari
1.2. Maswali ya ufahamu
1.3. Matumizi ya msamiati wa msingi
1.4. Sarufi
1.5. Matumizi ya lugha
1.6. Kusikiliza na kuzungumza
1.7. Kuandika.

Mwongozo wa mwalimu hutia mkazo kwenye majibu ya mazoezi yaliyotolewa pamoja na mbinu za kufundishia kwa kila zoezi.

## 1.2 Muelekeo wa ufundishaji

Kinyume na mtaala unaoegemea Ujuzi, mtaala unaoegamea Uwezo huwa na lengo kuu la kumfanya mwanafunzi awe mlengwa wa somo na kumshirikisha kimatendo katika mchakato wa ujifunzaji wake. Hapa mwalimu hatawali somo bali wajibu wake ni kumuelekeza au

kumwongoza mwanafunzi katika somo lote. Kwa ufupi, mwanafunzi hachukuliwi kama mgeni katika somo lake bali huchukuliwa kama mshiriki – mlengwa.

**1.2. 1. Mwelekeo wa Kuendeleza Uwezo**

Katika mchakato wa ujifunzaji wa Kiswahili, uendelezaji wa uwezo wa jumla kwa mwanafunzi unapewa kipaumbele sana. Uwezo huo wa jumla wa kuendelezwa ni kama vile tafakuri tunduizi, ubunifu, utafiti, utatuzi wa matatizo na ushirikiano. Haya yote yanafanikishwa katika ufundishaji kwa lengo la kuhakikisha kuwa mahitaji ya mwanafunzi yametoshelezwa. Hivyo basi, wanafunzi watapewa kazi mbalimbali zinazohitaji ushirikiano kati yao ili kukamilisha kufanya tafiti zao au kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika maisha. Kila ujifunzaji na ufundishaji wa kila somo lililoandaliwa unazingatia nafasi ya kumjengea mwanafunzi stadi sahihi za mawasiliano katika miktadha mbalimbali ya kimaisha kama mtu aliye na uwezo wa kushilikiana na watu mbalimbali katika miradi tofauti ya kijamii na kimaendelezo. Uwezo unaotakiwa katika kumjenga mwanfunzi utajikita katika mazeozi ya kusoma, kusikiliza, kuzungumza na kuandika kama njia muhimu za kudumisha mawasiliano katika lugha ya Kiswahili.

Ili kumwezesha kuwasiliana kwa usahihi na katika hali inayoweza kuyatatua matatizo yanayowakabili wanafunzi, mwalimu akumbuke kumwezesha katika kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Pia ufundishaji unaotarajiwa katika masomo husika ni kumwezesha mwanafunzi kupata menejimenti yake kama mtu binafsi aliye na malengo mahususi na pia katika mahusiano yake na watu wengine. Haya ni kusema kwamba mada mbalimbali zilizojadiliwa zinajenga muktadha wa kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kukuza na kuendeleza uwezo wa kila mwanafunzi.

Katika uendelezaji wa uwezo huu, mwanafunzi hushirikishwa katika kuyaelewa vyema maisha ya nchi na matatizo yake ya kila siku. Ndiyo sababu jambo la masuala mtambuka hutiliwa mkazo ndani ya kila somo. Ukweli ni kwamba uwezo peke yake wa mwanafunzi hauwezi kuendelezwa wakati ambapo masuala mtambuka yamewekwa pembeni. Masuala mtambuka yote manane yanayojitokeza katika mtaala wa taifa kama vile: Mafunzo dhidi ya mauaji ya kimbari, mazingira na maendeleo ya kudumu, usawa wa kijinsia, mafunzo kuhusu ujinsia, mafunzo kuhusu amani na maadili mema, mafunzo kuhusu uzalishaji mali, desturi ya usawa, mafunzo kuhusu elimu isiyo

na ubaguzi. Uingizaji wa masuala mtambuka katika somo hufaulu zaidi kutokana na jinsi mazoezi ya kimajadiliano yalivyotayarishwa na mwalimu.

### 1.2.2 Kuingizwa kwa Masuala mtambuka katika somo.

Katika kitabu hiki mwalimu awaongoze wanafunzi katika ujifunzaji na kutumia maswala mtambuka yafuatayo:

- Mafunzo kuhusu mauaji ya kimbari
- Mazingira na maendeleo endelevu
- Usawa wa jinsia
- Elimu kuhusu ufahamu wa ujinsia
- Mafunzo kuhusu amani na maadili.
- Elimu kwa wote/Elimu isiyo na ubaguzi
- Mafunzo kuhusu uzalishajimali
- Mila na desturi ya uchunguzi wa viwango

Mwalimu awasaidie wanafunzi kuingiza masuala mtambukahaya kwa kila somo wanalojifunza na kutafuta suluhisho kuhusu masuala hayo.

### 1.2.3. Uangalizi wa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum

Malengo ya ujifunzaji na ufundishaji humhusu kila mwanafunzi darasani bila ubaguzi au utengano wowote. Kwa hiyo, inambidi mwalimu kuyakumbuka na kuyahudumia makundi mbalimbali ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu au ya kipekee katika ujifunzaji wao. Hao ni kama vile wanafunzi wenye tatizo la kutoona, kutosikia, kutoandika, kutosoma, kutozungumza na matatizo mengine ya kiakili. Kwa kuwashirikisha wote, mwalimu hulazimishwa kutayarisha mazoezi ya aina aina kulingana na mahitaji ya kila mwanafunzi. Huduma zinazotarajiwa kutolewa zinaandaliwa na mwalimu kutokana na jinsi mahitaji maalumu ya wanafunzi darasani yalivyo.

### 1.2.4 Mwongozo wa Tathmini

Tathmini ni jambo muhimu sana katika njia hii ya ufundishaji na ujifunzaji. Lengo kuu la tathmini ni kupima maendeleo ya somo ambapo mwalimu huweza kuchagua aina ya tathmni kulingana na malengo yake.

- **Tathmini Endelezi**

Tathmini hii hulenga kupima jinsi ufundishaji na ujifunzaji unavyoendelea au kama makusudi au malengo ya ufundishaji na ujifunzaji yamefikiwa kwa kiwango fulani ili kuamua kuhusu uboreshaji wa baadaye. Tathmni hii inafanywa wakati masomo yangali yanaendelea na hulenga kuangalia uhusiano uliopo kati ya ufundishaji na ujifunzaji yaani uhusiano kati ya mwalimu na mwanafunzi. Hujumuisha upimaji wa mwenendo wa somo kabla somo lifikie kikomo. Tathmini endelezi inapaswa kuwa na dhima mwafaka katika ufundishaji na ujifunzaji. Inambidi mwalimu kuwahamasisha wanafunzi kufanya mazoezi na majaribio binafsi, mazoezi ya makundi, kwa kutumia mbinu zinazoegemea kwenye uwezo, maadili na mwenendo mwema kulingana na kila somo husika.

- **Tathmini ya jumla**

Kila tathmini huwa na dhima yake katika ufundishaji na ujifunzaji. Kwa mfano, tathmini ya mwishoni mwa mada itafikiriwa na itafanyika mwishoni mwa mada nzima kabla ya kutangulia mada nyingine. Aidha, tathmini inayofanyika mwishoni mwa muhula na mwishoni mwa mwaka zitakuwa mojawapo ya tathmini za jumla na wakati huu hulenga kurekodi ujuzi, uwezo, maadili na mwenendo mwema miongoni mwa wanafunzi kiasi kwamba walimu, viongozi wa shule na wazazi hupata na kuchunguza matokeo ya tathmini iliyofanywa. Tathmni zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi zitamwelekeza mwalimu kubashiri matatizo yaliyopo kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa kiwango cha kuwaelekeza wanafunzi kupata uwezo walio nao katika somo hili. Hivyo basi, tathmini zilizopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi ni msingi wa mambo mengine ambayo mwanafunzi atayakuta katika miaka mingine ya masomo yake ya Kiswahili kwa shule za sekondari.

### 1.2.5Mbinu na Mikakati ya Kuendeleza Ufundishaji na Ujifunzaji

Katika kuendeleza ufundishaji na ujifunzaji, mwalimu achunguze mambo yafuatayo:

- Upekee wa somo,
- Kielelezo cha somo,
- Malengo maalum ya kutimiza,
- Kuchunguza idadi ya vipindi mahususi kwa madhumuni ya kutimiza malengo ya somo,
- Maelekezo muhimu kuhusu vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji vinavyopatikana katika mazingira halisi,

- Jinsi wanafunzi watakavyokaa darasani,
- Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu,
- Uwezo na mtindo wa ujifunzaji.

### 1.2.6 Mbinu za Ufundishaji ZinazokuzaShughuli ya UjifunzajiShirikishi

Ili kufanikisha malengo ya somo lake, mwalimu azingatie njia zifuatazo:

- **Njia Shirikishi**: Njia shirikishi hutumia makundi ya wanafunzi ambapo mwalimu huwawezesha wanafunzi kushiriki katika kitendo cha ufundishaji na ujifunzaji. Kinachopaswa kufanywa hapa ni kuwapatia wanafunzi wote fursa ya kushiriki katika shughuli zinazopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi. Hali hii hutokana namazingira yanayojengwa na mwalimu ambapo kila mwanafunzi ndiye ambaye huchukuliwa kama kiini cha ufundishaji na ujifunzaji. Hivyo basi, wanafunzi watatumia makundi yao kwa kufanya shughuli zote watakazoombwa na mwalimu kama vile majadiliano, midahalo na mazungumzo ya aina tofauti kama yalivyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.
- **Njia ya kibinafsi:** Njia hii inahusu kazi binafsi za kila mwanafunzi ambapo atapewa kazi ama mazoezi yake binafsi iliaweze kufikia kiwango cha umilisi wa lugha kinachotarajiwa. Baada ya kufanya kazi na mazoezi hayo, ni vyema mwalimu akumbuke kuambatanisha njia aliyoitumia na njia shirikishi kwa kumwomba mwanafunzi achunguze maoni na hoja za wanafunzi wenzake katika makundi yao. Katika njia ya kibinafsi, mwalimu anaweza kuomba mwanafunzi kwa mfano kujisomea kifungu cha habari, kutambua maana za maneno mapya na kuyatumia katika sentensi zake, n.k.
- **Maswali na majibu**: Mara nyingi somo huchukua mwelekeo wa majadiliano kati ya mwalimu na wanafunzi. Kuhusiana na mbinu hii, mwalimu atawauliza wanafunzi maswali mbalimbali nao watajibu maswali hayo. Kwa upande mwingine, wanafunzi wanaweza kumwuliza mwalimu wao naye akawajibu. Vilevile, maswali na majibu haya yanaweza kujitokeza kati ya wanafunzi wenyewe. Katika hali hii, mwalimu atawaelekeza wanafunzi wake kujitafutia majibu kwa maswali wanayouliza huku akiwapa maelekezo muhimu au mwongozo unaofaa kwa kusahihisha makosa wanayoyafanya.
- **Maelezo ya mwalimu**: Mwanafunzi hupewa muda wa kushiriki yeye binafsi katika somo. Katika njia hii, mwalimu atakuwa mwelekezi na shughuli yake muhimu itaegemea

kuwaongoza wanafunzi kupata ufahamu na uelewa unaofaa. Kwa hiyo, mwalimu atatumia mbinu hii kwa kueleza mambo yatakayohitaji maelezo yake ili kufanikisha somo lake.

## SEHEMU II: SAMPULI YA ANDALIO LA MASOMO

### ANDALIO LA SOMO

**Jina la shule:………………….** **Jina la mwalimu:…………………..**

| Muhula | Tarehe | Somo | Kidato | Mada | Idadi ya masomo | Muda | Idadi ya wanafunzi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1/10/2022 | Kiswahili | 6 | 1 | 1 kwa 4 | Dakika 80 | 45 |

| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ya kielimu pamoja na idadi yao:**<br><br>Mwanafunzi mwenye matatizo ya kuzungumza: 1 | |
|---|---|
| **Mada kuu** | FASIHI KATIKA KISWAHILI |
| **Mada ndogo** | UFAFANUZI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI |
| **Uwezo mahususi upatikanao katika mada** | Kutumia tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani; Kutunga sentensi kwa usahihi kufuatana na vifungu vya sentensi |
| **Kichwa cha somo** | Dhana ya tanzu za Fasihi Andishi |
| **Malengo ya ujifunzaji** | Kwa njia ya majadiliano na uwasilishaji darasani, wanafunzi waeleze kwa ufasaha dhana ya fasihi andishi katika Kiswahili kwa kusisitizia maana ya fasihi andishi, asili yake, faida na hasara zake pamoja na tofauti iliyopo kati ya fasihi simulizi na fasihi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | andishi. | | |
| **Mahali ambapo somo litatolewa** | Darasani | | |
| **Zana au vifaa** | Kitabu cha Kiswahili (Kidato cha sita, kitabu cha mwanafunzi na mwongozo wa mwalimu ), Kamusi ya Kiswahili Sanifu, ubao, kalamu, karatasi, flip chati, n.k. | | |
| **Marejeo** | REB (2022), Kiswahili kwa Shule za Rwanda. Kitabu cha Mwanafunzi, Kidato cha Sita | | |
| **Muda na hatua** | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji | | **Uwezo wa jumla na**<br>**Masuala mtambuka na maelezo mafupi** |
| | Kwa njia ya majadiliano katika makundi madogomadogo, wanafunzi wazungumzie kwa ufasaha dhana ya fasihi andishi katika Kiswahili. | | |
| | Wajibu wa mwalimu | Wajibu wa mwanafunzi | |
| **1. Utangulizi**<br>**Dakika 7** | - Kufanya kidokezo cha somo<br>- Kumshirikisha mwanafunzi mwenye matatizo ya kuzungumza kwa kumpatia fursa ya kutoa maoni yake kwa njia ya kuandika kwenye karatasi. | - Kutoa maoni kuhusu kidokezo cha somo<br>- Kujibu maswali ya mwalimu | ❖ **Uwezo wa jumla**<br>**(a) Mawasiliano katika lugha rasmi.**<br>Katika mawasiliano baina yao wenyewe au pamoja na mwalimu, wanafunzi wasisitiziwe kuzungumza kwa ufasaha wakitumia Kiswahili sanifu.<br>**(b) Tafakuri tunduizi:** Katika majadilianoyao, wanafunzi hujizoeza |
| **2. Somo lenyewe** | - Kuunda makundi manne ya wanafunzi | - Kufuata agizo la mwalimu la kuunda | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Dakika 60** | - Kuwapa wanafunzi kazi za kushughulikia katika makundi kama ifuatavyo:<br><br>*Kundi la kwanza: kueleza maana ya fasihi andishi;<br><br>*Kundi la pili: kueleza asili ya fasihi andishi;<br><br>*Kundi la tatu: kujadili faida na hasara za fasihi simulizi<br><br>*Kundi la nne: kutoa tofauti iliyopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. | makundi.<br><br>-Kujigawa katika makundi yaliyopangwa na mwalimu na kushiriki kikamilifu kwenye kazi iliyotolewa. | kufikiri kabla ya kujibu au kutoa maoni ili kuepuka upotovu wowote.<br><br>**Masuala mtambuka**<br><br>❖ **Elimu jumuishi:**<br><br>Kila mwanafunzi hushirikishwa kikamilifu kwa kupewa kazi za ujifunzaji husika bila kuwasahau wanafunzi wenye mahitaji maalum ya ujifunzaji.<br><br>❖ **Mafunzo kuhusu amani na maadili** |
| **2.1.Zoezi la ugunduzi** | Kuandika ubaoni maoni tofauti kuhusu dhana ya fasihi andishi na kuwaomba wanafunzi kuchagua maoni yanayohusika sana na fasihi andishi.<br><br>. | Kusoma maoni yaliyotolewa na mwalimu na kuyatenganisha kulingana na dhana ya fasihi andishi. | Katika majadiliano kuhusu umuhimu au faida za fasihi, wanafunzi wasisitizie amani na maadili kama lengo kuu la fasihi.<br><br>❖ **Mafunzo kuhusu uzalishajimali**<br><br>Wanafunzi waendeleze uwezo wa kutetea jinsi fasihi andishi inavyotumiwa kama njia ya kujitegemea |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **2.2. Uwasilishaji wa wanafunzi** | - Kutoa mwongozo wa uwasilishaji wa kazi iliyoshughulikiwa na kila kundi<br>- Kutega sikio kwa makini uwasilishaji wa kazi na kuongoza uwasilishaji<br>- Kutoa nyongeza au swali | Kuwasilisha kazi zilizoshughulikiwa kwa kuyaheshimu maagizo ya mwalimu | kiuchumi. |
| **2.3. Uchambuzi** | - Kuuliza maswali kwa kundi lililowasilisha kazi ili kuimarisha maelezo ya wanafunzi<br>- Kutoa nyongeza, kukamilisha au kusahihisha maoni yasiyo ya ukweli. | Kushiriki kwenye uchambuzi wa kazi zilizowasilishwa kwa kujibu maswali husika au kutoa nyongeza. | |
| **2.4 .Hitimisho** | Kuwaelekeza wanafunzi katika kuendeleza muhtasari wa somo | - Kutoa muhtasari wa somo. | |
| **3. Tathmini**<br>**Dakika 13** | - Kutoa zoezi au jaribio kwa wanafunzi na kuwaelekeza katika masahihisho.<br>- Kutoa kazi ya nyumbani na | - Kufanya zoezi au jaribio kama kazi binafsi<br>- Kuandika kazi ya nyumbani katika daftari | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | maelekezo husika. | | |
| **Tathmini ya mwalimu** | Kulingasha matokeo ya tathmini kwa wanafunzi na malengo ya ujifunzaji ili kuhakikisha mafanikio ya mbinu za ujifunzaji na ufundishaji zilizotumiwa. | | |

## SEHEMU YA III: UUNDAJI WA MADA

## MADA KUU YA 1 : FASIHI KATIKA KISWAHILI

### MADA NDOGO YA 1: UFAFANUZI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI KATIKA KISWAHILI

**1.1.uwezo upatikanao katika mada**

Kutumia tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani; Kutunga sentensi kwa usahihi kufuatana na vifungu vya sentensi.

**1.2 .Ujuzi wa awali**

Katika kidato cha nne na cha tano, wanafunzi walizungumzia kwa ubaga maana ya fasihi, umuhimu wake katika jamii pamoja na tanzu zake ambapo fasihi andishi ilidokezewa sana. Haya yanahakikishwa na mada zifuatazo:

- Fasihi katika Kiswahili (Kidato cha nne; somo la 9 – 11)
- Nadharia ya fasihi katika Kiswahili (Kidato cha tano; somo la 1)

**1.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake**

**1.3.1.Kidokezo cha mada**

Ainisha hati za Kiswahili zifuatazo katika sarafu mbili: sarafu ya tanzu za fasihi simulizi na sarafu ya fasihi andishi.

**1.3.2 Maelekezo ya kidokezo cha mada**

Chagua vitabu au hati tofauti; au chagua vichwa vya hati za kazi za fasihi simulizi pamoja na fasihi andishi. Washirikishe wanafunzi kubainisha hati za fasihi simulizi na kuzitenganisha na zile za fasihi andishi. Waombe wanafunzi kutetea msimamo wao kwa kutemea mwelekeo wa enzi pamoja na vifaa vilivyotumiwa kutengeneza hati hizo.

### 1.4. Orodha ya masomo

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| **1** | Dhana ya tanzu za fasihi andishi | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha tanzu za fasihi andishi<br><br>**Stadi :**Kutofautisha tanzu za fasihi andishi<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha nia ya kusoma tanzu tofauti za fasihi andishi kwa ajili ya mafunzo ya sanaa | **6** |
| **2** | Utanzu wa hadithi fupi | **Maarifa na ufahamu:**Kutambua maana ya hadithi fupi na sifa zake<br><br>**Stadi** : Kutunga hadithi fupi kwa kuzingatia muundo wake.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujenga moyo wenye huruma, utu na busara kutokana na maudhui yanayozingatiwa katika hadithi fupi | **16** |
| **3** | Utanzu wa riwaya | **Maarifa na ufahamu:** Kufafanua maana ya riwaya na sifa zake<br>**Stadi**: Kutunga riwaya kulingana na muundo wake.<br>**Maadili na mwenendo mwema**:Kukuza stadi za ubunifu katika uandishi wa riwaya | **16** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | Utanzu wa tamthiliya | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza maana ya tamthilia na sifa zake<br><br>**Stadi :**Kubuni au kutunga tamthilia kufuatana na muundo wake.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kusisimua watu na kuiburudisha jamii | **16** |
| | Utanzu wa ushairi | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya ushairi andishi<br><br>**Stadi**: Kutunga shairi kwa kuheshimu kanuni husika<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kukuza kipaji cha utungaji wa mashairi | **16** |
| - | Sarufi: Virai na vishazi katika Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:**Kuainisha vifungu vya sentensi katika Kiswahili<br><br>**Stadi :**Kutunga sentensi sahihi kwa muelekeo wa kirai na kishazi<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:**Kuimarisha maarifa ya kuichambua sentensi ya Kiswahili kulingana na vifungu vyake**.** | **-** |
| **Tathmini ya mada** | | | **2** |
| **Jumla ya vipindi vya mada ya kwanza** | | | **72** |

**Maelekezo kuhusu uandaaji wa masomo yaliyoonyeshwa hapo juu**

- **Vipengele vya muundo wa somo**

Kila somo hujengwa na vipengele vifuatavyo:

1. Kusoma na ufahamu vifungu vya habari
2. Msamiati kuhusu vifungu vya habari vilivyosomwa
3. Matumizi ya lugha
4. Kusikiliza na kuzungumza
5. Sarufi
6. Kuandika

- **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila kipengele cha somo**

**(a) Kusoma na ufahamu kifungu cha habari**

- **Kusoma:**Kwa kutegemea kitabu cha mwanafunzi au nakala ya vifungu vya habari, wanafunzi washirikishwe kwenye kazi ya kusoma kifungu husika kwa njia tofauti: kusoma kimya au kusoma kwa sauti. Mwalimu ashirikishe wanafunzi wote kwenye kazi hii kwa kutumia njia moja au nyingine. Ili kurahisisha kazi hii na kufaulu kuwashirikisha wanafunzi wote, kazi hii huweza kufanyika katika makundi madogomadogo au katika jozi.
- **Ufahamu:** Ufahamu wa kifungu cha habari huweza kufikiwa kwa njia nyingi kama vile kufasiri michoro au picha zilizotumiwa katika kifungu cha habari husika; kuuliza maswali ya ufahamu, kutoa dhamira kuu zilizosisitiziwa katika kifungu cha habari, kutoa muhtasari wa habari iliyozungumziwa, n.k. Kwa hiyo, inambidi mwalimu achagua njia moja au zaidi baadhi ya hizi au nyingine ambayo haikutajwa hapa juu.

**(b) Matumizi ya msamiati**

Katika kipengele hiki, mwalimu anastahili kujenga kwa wanafunzi tafakuri tunduizi, yaani kuwaongoza wanafunzi kugunduwa wao wenyewe maana ya msamiati husika kwa kutegemea muktadha wa kifungu cha habari kwa ujumla. Si vizuri kupendekeza matumizi ya kamusi kama hatua ya kwanza ya kutoa maana ya msamiati. Kadhalika, maana ya msamiati huweza kupatikana kwa kutumia michoro au picha husika. Vifaa hivi huweza kuandaliwa na mwalimu lakini ni vizuri kuwashirikisha wanafunzi katika zoezi la kuchora michoro kulingana na maana ya msamiati husika. Pia, mbinu ya kutoa kinyume au kisawe cha msamiati husika huwa muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati.

**(c)Matumizi ya lugha**

Ni wajibu wa mwalimu kuhusisha kifungu cha habari na maisha ya kila siku ya wanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima wanafunzi wapewe kazi zinazostahili kuamsha akili ili kutafuta njia ya utatuzi wa matatizo yanayoweza kuikumba jamii wanamoishi.

**(d) Kusikiliza na kuzungumza**

- Kusikiliza: Wanafunzi wanaweza kukuza uwezo wa kusikiliza kwa njia tofauti: kusomewa kwa sauti kifungu cha habari, kusikiliza habari au hotuba zilizorekodiwa, kusikiliza hadithi au habari kwenye redio, televisheni au tarakilishi. Kwa hiyo, inambidi mwalimu kutumia njia hizi tofauti za kukuza stadi za kusikiliza kwa wanafunzi.
- Kuzungumza: Kuna njia nyingi za kukuza stadi za kuzungumza kwa wanafunzi. Baadhi ya hizi kuna midahalo na mijada, maigizo, uwasilishaji darasani, nyimbo, michezo, mazungumzo, masimulizi, mhadhara, n.k.Katika kazi zake za ujifunzaji, mwanafunzi ashirikishwe kikamilifu katika kazi mbalimbali kwa kuchanganya mbinu zilizotajwa hapo juu.

**(e) Sarufi**

Sarufi inayotarajiwa katika uwezo mahsusi wa mada **haifundishwikamasomo la kujitegemea baada ya mada**bali hujitokeza mwishoni au kati kati ya kila somo. Kwa hiyo vipera vya sarufi hii hujigawa kulingana na idadi ya masomo yanayoiunda mada nzima.

**(f) Kuandika**

Wakati wa kazi zinazofanyika katika makundi madogomadogo, wakati wa maelezo ya mwalimu, wakati wa uwasilishaji wa kazi darasani, wakati wa kutoa muhtasari wa somo na hasa wakati wa majaribio na mitihani au katika kuziandaa kazi za nyumbani, inambidi mwalimu awashirikishe na kuwahimiza wanafunzi kuandika. Pia, mwalimu asisahau imla kwa wanafunzi katika kazi zao za ujifunzaji.

## SOMO LA 1: DHANA YA TANZU ZA FASIHI ANDISHI

**i) Malengo ya ujifunzaji**

Kubainisha na kutofautisha tanzu za fasihi andishi

**ii) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za majaladaya vitabu vya kazi za fasihi andishi
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Sampuli ya kazi za fasihi andishi.
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenyematatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

### iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

### iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi

**Kusoma na ufahamu:Kifungu kuhusu tanzu za fasihi andishi**

**Maswali ya ufahamu*(Uk.3 - 4)***

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome kifungu cha habari kuhusu tanzu za fasihi andishi na kutoa majibu sahihi kwa maswali husika. Majibu yanayopendekezwa ni haya yafuatayo:*

1. Fasihi andishi ni aina ya sanaa ambayo msanii au mtungaji hutumia maneno ambayo huandikwa kwa lengo la kupitisha ujumbe.
2. Dunia ya leo imekuwa kama kijiji kimoja kutokana na maendeleo ya fasihi andishi yaliyoenea kote duniani kupitia kwa uandishi na usomaji kwenye mtandao.
3. Riwaya, hadithi fupi, tamthilia na ushairi.
4. Huwa na wahusika wengi wa kubuni na huandikwa kwa aya na kwa mfululizo wa matukio mengi.
5. Beti, mishororo na mizani.
6. Hadithi fupi huwa na wahusika wachache sana ilhali riwaya huwa na wahusika wengi. Hadithi fupi huhusisha visa vifupi vifupi ilhali riwaya huhusisha usimulizi wa matukio marefu.
7. Tamthilia huandikwa kwa mtindo wa maneno kuandikwa mbele ya mhusika anayeyezungumza ilhali shairi huandikwa kwa kutumia beti zenye mishororo.
8. Fasihi andishi huchangia katika ukuzaji wa lugha kwa sababu watu wanaweza kuhifadhi msamiati wao wa kale kupitia kwa kazi ya uandishi. Fasihi andishi hukusanya matukio ya dunia na kuyaleta karibu na msomaji, hivyo basi hurahisisha ufahamu wa historia ya wengi. Huchangia katika maendeleo ya utamaduni wa nchi kupitia kwa maandishi ambayo huzingatia elimu kuhusu utamaduni. Fasihi andishi ni sanaa inayomsaidia binadamu

kujiendeleza na kuelimika kuhusu historia ya mtu tangu kale na pia kutabiri kisayansi mambo yatakayoathiri binadamu siku zijazo.

9. Msanii hutunga kazi za fasihi akilenga kupitisha ujumbe kwa hadhira yake.
10. La. Kazi ya fasihi andishi ni mali ya mtu binafsi hivyo basi mtu yeyote hawezi kuibadilisha kazi ya mwingine.

**Matumizi ya msamiati**

**Zoezi la 1A: (uk. 4)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi washirikiane kwa kutafuta maana ya msamiati uliopigiwa mstari. Majibu yanayopendekezwa ni haya yafuatayo:*

1. Tamthilia - hadithi ambayo imeandikwa kama mazungumzo kati ya watu; mchezo wa kuigiza. 2. Riwaya - hadithi ndefu ya kubuni yenye wahusika na mtiririko wa visa iliyoandikwa kwa lugha ya mfululizo.
2. Shairi - mtungo wenye muundo na lugha ya kisanii unaofuata utaratibu wa vina na mizani, hisi au tukio juu ya jambo au maisha.
3. Hadithi fupi - ni utungo wa kinathari ambao unazungukia tukio moja kuu na unaosimulia kisa kinachomhusu mhusika mmoja au wahusika wachache sana na unaozungumzia kipindi maalumu kwa mtindo wa kibanifu.
4. Ishara - alama au tendo linalowasilisha kitu halisi.
5. Mizimu - vivuli vya watu waliokufa zamani vinavyowatokea watu kwenye ndoto.
6. Mtandao - mfumo wa mawasiliano wa kielektroniki unaopitia katika kompyuta ambao watu huutumia kupata taarifa za aina mbalimbali au kuwasiliana.
7. Wahusika – mtu, mnyama au kiumbe yeyote katika hadithi ya kubuni anayetenda mambo kadhaa kulingana na atakavyo mtunzi ili kuijenga hadithi yake.
8. Sanaa - uhodari wa kuwasilisha hisia za mwanadamu kwa maandishi. Kwa mfano: kupitia kwa riwaya, tamthilia, hadithi fupi na mashairi andishi.
9. Wasanii - watu walio na ujuzi wa kuchora, kutunga au kuchonga.

**Zoezi la 1B (Uk. 4 -5)**

*Katika jozi, wanafunzi waweke sentensi walizopewa katika hali kanushi. Majibu yanayopendekezwa ni yafuatayo:*

1. Tamthilia niliyoisoma haisisimui.
2. Sisi hatusomi riwaya kila muhula.
3. Sitatunga shairi lenye beti sita.
4. Hadithi fupi nzuri haiwi na wahusika wachache.
5. Lugha ya ishara haitumiwi sana na wasanii wengi.
6. Mtoto hakuota akikimbizwa na mizimu.
7. Sitasakura kwenye mtandao ili kupata habari kamili.
8. Sijazoea kusoma vitabu vyenye wahusika wengi.
9. Sanaa ya uandishi haipendwi na wengi.
10. Wasanii wengi hawatungi kazi zao wenyewe.

**Zoezi la 2 (Uk.5)**

*Katika makundi, wanafunzi wajaze nafasi iliyoachwa wazi kwa kutumia msamiati unaofaa. Majibu yanayopendekezwa ni yafuatayo.*

1. Fasihi andishi
2. lengo
3. hadhira
4. mali
5. wachache
6. Riwaya
7. mishororo

**Matumizi ya lugha:Umuhimu wa fasihi andishi (uk.5)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wazungumzie mambo matano yanayoonesha umuhimu wa fasihi andishi katika jamii. Mfano wa maoni yaoneshayo umuhimu wa fasihi andishi katika jamii ni kama:*

1. Kuiongoza na kuielekeza jamii: Fasihi andishi ni wenzo muhimu ya kuwaelekeza watu na kuwakanya dhidi ya kufanya jambo fulani. Kwa mfano, kupitia kwa mashairi andishi, tabia ambazo hazikubaliki katika jamii huweza kukejeliwa.
2. Fasihi andishi huhifadhi historia ya jamii fulani: Kwa kusoma hadithi zinazohusu matukio halisi ya kihistoria katika jamii na pia kuhusu mila na tamaduni za jamii husika, historia ya jamii hiyo huhifadhiwa.
3. Huakisi na kuonyesha imani, itikadi na msimamo wa jamii fulani kuhusu mambo mbalimbali. 4. Huburudisha wanajamii: Mashairi mengi husomwa kwa ajili ya burudani. Halikadhalika, riwaya na hadithi fupi pia husomwa kama njia ya kujiburudisha.
4. Hukuza na kuendeleza stadi za lugha miongoni mwa wanajamii: Kutokana na mbinu mbalimbali za uandishi ambazo hutumiwa na wasanii wengi, ukuzaji wa stadi ya utungaji na uandishi hukuzwa.
5. Hukuza na kuimarisha uhusiano kati ya wanajamii mbalimbali

**Sarufi: Maana ya sentensi**

**Zoezi la kidokezo**: *Katika makundi, wanafunzi watunge sentensi kamili na sahihi kwa kupanga vizuri maneno waliyopewa kama ifuatavyo:*

1. Wewe huenda shuleni kila siku.
2. Mimi ni mwanafunzi wa kidato cha sita.
3. Mwalimu wetu anafundisha somo la Fasihi.
4. Kwa nini unakariri shairi hilo polepole?
5. Riwaya huwa na wahusika wengi walio wa kubuni kuliko hadithi fupi.
6. Tamthilia ni utanzu mmojawapo katika tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili

**Zoezi la 3 (uk.6)**

*A. Katika jozi, jadili maana ya sentensi.Mapendekezo kuhusu maana ya sentensi Ni yafuatayo:*

Sentensi ni kundi la maneno au neno moja lililo na maana kamili. Maana katika sentensi huonyeshwa na kitenzi. Kundi la maneno lisilohusisha kitenzi si sentensi, na neno moja ambalo si kitenzi kikuu nalo haliwezi kuwa sentensi.

**Zoezi la 4 ( uk.7)**

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wajadili sifa za sentensi kamili katika lugha ya Kiswahili.*

Sentensi kamili ya Kiswahili:  Yafuatayo ni majibu:

1. Huwa na ujumbe uliokamilika na unaoeleweka.
2. Huwa na mpangilio maalumu wa maneno. Yaani: kiima na kiarifu (K+A).
3. Huwa na kauli ya vitenzi. Kwa mfano: tendwa, tendeka, tendea n.k.
4. Huhusisha hali ya vitenzi katika sentensi husika. Kwa mfano: yakinishi, kanushi, amrishi n.k.
5. Huwa na nyakati za vitenzi katika sentensi. Kwa mfano: uliopo, uliopita, ujao n.k.

**Zoezi la 5 (uk. 7)**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wachunguze sentensi zifuatazo kisha wachague na kubainisha sentensi zisizo kamili. Waeleze pia sababu za upungufu wa sentensi watakazozichagua.Majibu ni yafuatayo:*

- Sentensi zisizo kamili ni: 1, 4, 5 na 10. Sentensi hizi hazina vitenzi.

**Zoezi la 6A (uk.8)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunziwachunguze sentensi walizopewa nakujadili aina za maneno zinazounda sehemu za kiima na sehemu za kiarifu katika sentensi hizo.Mwelekeo ufuatao uzingatiwe:*

1. Kiima (nomino), kiarifu (kitenzi, nomino, kivumishi).
2. Kiima (kiwakilishi), kiarifu (kitenzi, nomino, kivumishi).
3. Kiima (kiwakilishi), kiarifu (kitenzi, kielezi).
4. Kiima (nomino), kiarifu (kitenzi, kielezi, kielezi).
5. Kiima (nomino), kiarifu (kitenzi, nomino).

**Zoezi la 7 (uk.10)**

*Katika jozi, wanafunzi waainishe aina za maneno yanayounda kiima na kiarifu kwa kutumia jedwalila sehemu ya kila sentensi kupitia jedwali. Haya ni mapendekezo ya jibu:*

1. Mama analima shamba kubwa.
   Kitenzi + shamirisho (nomino + kivumishi).
2. Yeye ni mwanafunzi hodari.
   Kitenzi + shimirisho(Nomino + kivumishi).
3. Sisi tutaimba vizuri.
   Kitenzi + chagizo (kielezi)
4. Kamana ataenda sokoni jioni.
   Kitenzi + chagizo (kielezi + kielezi)
5. Mwalimu anafundisha fasihi.
   Kitenzi + shamirisho (nomino)

## SOMO LA 2: UTANZU WA HADITHI FUPI

### i) Malengo ya ujifunzaji

Kuelezadhana ya hadithi fupi  na kuitunga kwa kuzingatia mwongozo wake.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za majalada ya hadithi fupi
- Tarakilishi, projekta

- Redio rekoda au simujanja
- Ubao, chaki
- Sampuli ya vitabu vya hadithi fupi.
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu awe huru katika kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wanafunzi wenye matatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi**

**Kusoma na ufahamu: Hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira**

**Maswali ya ufahamu *(uk. 13)***

*Katika jozi, wanafunzi wasome kifungu husika na kutoa majibu sahihi ya maswali ya ufahamu. Hakikisha kuwa wanafunzi wanashirikiana kikamilifu. Majibu yanayopendekezwa ni yafuatayo.*

1. Kware, korongo, tai, mwewe na heroe.
2. Kulikuwa na wawindaji, wavuvi, wauza kuni, wauza mbao na wachoma makaa ambao waliuvamia msitu wa Nyarume kwa shughuli zao za kujinufaisha.
3. Misitu ni makazi ya wanyamapori kwa kuwa wao huishi humo na wengine katika mapango yaliyo misituni. Miti iliyo misituni huleta mvua ambayo maji yake hunywewa na wanyamapori.
4. Wanyamapori huwavutia watalii kutoka kote duniani kuja kuzuru nchi yetu kwa ajili ya kuwaona na kuiletea nchi yetu pesa zinazosaidia katika maendeleo mbalimbali nchini.
5. Huwahifadhi wanyamapori ambao watalii huja nchini kuwaona na kulipa pesa ambazo hutumika kuendeleza nchi.

6. Wanyamapori hukosa makazi na kufa. Wanyama wengine huhamia kwenye maeneo ya mbali na pale ambapo makao yao yameharibiwa.
7. Hupunguza idadi ya wanyamapori kutokana na wao kuuawa. Hupunguza idadi ya watalii wanaozuru nchi na maendeleo ya nchi huathirika kwa sababu pesa za kigeni kutoka kwa watalii hupungua.
8. Watu hukosa maji ya kunywa, kuoga, kupika na kufua nguo. Viumbe wanaoishi majini watakosa makao kwa sababu ya ukame. Maji ni uhai kwa viumbe wote pamoja na mimea.
9. Miti ni makao ya ndege, huleta mvua, hutupatia kuni na makaa na pia hutupatia mbao. Maji ni makao ya wanyama wanaoishi majini, hutumika katika shughuli za nyumbani za kuosha, kunywa na kupika na pia maji hunyunyiziwa mimea.

10.

a) Bwana Bakame ni mwenye bidii kwa kuwa amefanya kazi kwa miaka mingi. Ni mpole, mcheshi na mwenye hekima kwa sababu watu wengi walimpenda sana. Yeye ni kiongozi bora kwa kuwa anachaguliwa na wapiga kura wengi sana.

b) Mlinzi mkuu wa msitu Nyarume ni mwenye hekima na maarifa. Anakanya dhidi ya kuharibu mazingira na pia anatoa maelezo kuhusu umuhimu wa wanyamapori.

**Matumizi ya msamiatiwa hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi washirikishwe kutoa maana ya msamiati kutoka kifungu cha habari kilichosomwa kwa kutumia njia tofauti za ujifunzaji wa msamiati. Matumizi ya Kamusi sanifu ya Kiswahili yaruhusiwe. Yafuatayo ni majibu yanayopendekezwa.*

**Zoezi la 1 (uk.14)**

1. - J 2. - F 3. - G 4. - D

5. - H 6. - B 7. - CH 8. - E

9. - A 10. - I

**Matumizi ya lugha (uk.14)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waongozwe katika majadiliano yao kuhusuuhifadhi wa mazingira. Hakikisha kuwa wanafunzi wanawasiliana katika Kiswahili. Yafuatayo ni mapendekezo ya maoni yanayoweza kutolewa:*

1. Faida mbalimbali za kuhifadhi mazingira yetu ni kama vile: Kuepuka magonjwa mbalimbali, kupata mazao ya shambani, kupata maji safi ya matumizi n.k.
2. Madhara ya kuharibu mazingira yetu ni kama vile: Kukosa maji safi ya kutumiwa na viumbe na mimea, kukosa chakula na hata kushikwa na magonjwa mbalimbali.
3. Njia za kuhifadhi mazingira yetu ni kama vile: Kupanda miti mingi, kufyeka nyasi ndefu zilizo karibu na makao ya binadamu, kuepuka kutupa takataka ovyo n.k.
4. Shughuli zinazoharibu mazingira yetu ni kama vile: Kutupa takataka ovyo ovyo, kukata miti ovyo ovyo, kumwaga kemikali na uchafu kwenye vianzo vya maji n.k.
5. Umuhimu wa mazingira kwa wanyamapori ni kama vile: Wanyamapori hupata makao, chakula na hata maji safi ya kunywa.

**Zoezi la 2A (uk.15)**

*Kwa kazi za makundi au kazi binafsi, wanafunzi wafupishe hadithi fupi waliyopewa kwa kuzingatia mwongozo ufuatao:*

- Soma kifungu mara mbili na kwa makini.
- Jibu maswali kama vile: - Kifungu kinahusisha wahusika gani? - Mandhari ya kifungu ni yapi? - Wahusika muhimu ni akina nani? - Kifungu kinaeleza mawazo gani?
- Jibu maswali hayo kwa kuyaandika kwenye karatasi. b) Kufuata taratibu za kuandika ufupisho wenyewe.
- Andika kichwa cha ufupisho.
- Tutumia maneno yako mwenyewe.
- Tumia Kiswahili sanifu. (Usichanganye lugha mbalimbali)
- Kazi iwe safi na mwandiko wako uweze kusomeka.
- Hakikisha kwamba unaepuka makosa ya kisarufi katika ufupisho wako.
- (Zingatia matumizi sahihi ya alama za uandishi, matumizi sahihi ya ngeli, n.k.)
- Usipunguze, usiongeze wala usiende kinyume na mawazo asilia ya mtunzi wa kifungu.
- Usiandike zaidi ya maneno uliyoagizwa.

Ufuatao ni mfano wa ufupisho kuhusu zoezi lililotolewa:

Bwana Bakame aliishi katika msitu wa Nyarume uliokuwa na ndege na wanyamapori wengi. Kando ya msitu huo kulikuwa na vijiji vya watu wengi waliomfahamu Bwana Bakame ambaye alikuwa na uwezo wa kuwaelekeza wageni wote katika msitu huo kwa kuwa alikuwa ndiye kiongozi huko. Msitu ulikumbwa na shambulizi baada ya miaka miwili na wanyama wengi walifariki. Hili lilisababisha kuandaliwa kwa mkutano mkubwa wa wanyamapori wote msituni humo. Katika mkutano huo, mlinzi mkuu aliwapa pole wanyama kwa shambulizi lililowakumba. Baadaye, aliwapa ushauri kuwa ni muhimu kuyatunza mazingira. Aliwaonya dhidi ya kukata miti kwa sababu huku kuliwakosesha wanyamapori makazi.  Baadaye, aliwaeleza umuhimu wa wanyamapori kwa kusema kuwa walikuwa kivutio cha watalii ambao walileta pesa nyingi ili kuwaona wanyamapori hao. Mwisho, alitoa ushauri kuhusu maji na umuhimu wake na akaomba kuwa maziwa na mito ilindwe. Bwana Bakame alikamilisha mkutano kwa kumshukuru mlinzi mkuu na kuwaomba wanayamapori kusahau shambulizi lililowakumba na kuwasisitizia uimarishaji na ushirikiano mwema na watu wote katika shughuli za kuhifadhi msitu.

**Kusikiliza na kuzungumza: Sifa bainifu za hadithi fupi**

**Zoezi la 3 (uk.16)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waongozwe katika kueleza kinagaubaga sifa bainifu za hadithi fupi kwa kuzingatia mwelekeo ufuatao:*

1. Hadithi fupi huwa na wahusika wachache. Huwa na mhusika mmoja mkuu ambaye humwongoza msomaji.
2. Hadithi fupi huwa fupi na inaweza kusomeka katika kikao kimoja.
3. Hadithi fupi hushughulikia tukio moja kuu katika maisha ya mhusika mkuu.
4. Hadithi fupi huwa haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo ikilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi andishi.
5. Hadithi fupi huhusisha usimulizi wa moja kwa moja.
6. Hadithi fupi hulenga sana kuibua hisia za msomaji kuliko kuchochea fikira zake.
7. Hadithi fupi huenda haraka kimatendo, kiwakati, kimasafa na kimatukio

**Zoezi la 4( uk.16)**

*Katika makundi ya watatu watatu, wanafunzi wajadiliane kuhusu mambo muhimu yaliyopatikana katika hadithi fupi waliyosoma hapo awali kuhusu uhifadhi wa mazingira na kuyalinganisha na maisha yao ya kila siku.* Wanaweza kutaja hoja kama vile:

1. Ukataji wa miti ili kupata kuni, makaa na mbao husababisha uharibifu wa mazingira. Katika maisha ya kila siku, kuna watu ambao hujiingiza katika shughuli hizi za ukataji miti ovyo na kuishia kuyaharibu mazingira yetu. Hili linahitaji kurekebishwa.
2. Katika maisha yetu ya kila siku, panapotokea janga au shida fulani katika jamii, wanajamii huitwa kwenye mkutano ili kujadiliana kuhusu suluhisho la tatizo lililowakumba. Wanyamapori wote wanaitwa kwenye mkutano wanapokumbwa na shambulizi la mazingira yao kuharibiwa.
3. Mazingira ya msitu wa Nyarume yalianza kuhifadhiwa vyema tena baada ya kukumbwa na shambulizi la uharibifu. Katika maisha ya kila siku, mtu anapofanya kosa ni muhimu kurekebisha na kuanza upya tena.
4. Maji ni muhimu katika shughuli za binadamu za kila siku kama vile: kupika, kuoga na kusafisha mazingira n.k. Pia, maji ni muhimu kwa mimea na viumbe wengine

**Zoezi la 5(uk. 16)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi watetee umuhimu wa hadithi fupi katika jamii. Maoni haya yanapendekezwa:*

1. Huburudisha.
2. Huelimisha.
3. Hupitisha ujumbe kuhusu jamii fulani.
4. Hututahadharisha kuhusu mazingira yetu.
5. Hushauri wanajamii dhidi ya mambo mbalimbali.
6. Huhifadhi utamaduni na historia ya jamii fulani.

**Sarufi: Maana ya kirai**

**Zoezi la 6*(u*k.17)**

*Katika jozi, wanafunzi waeleze tofauti iliyopo kati ya sentensi kamili na kirai. Mwalimu awaongoze kwenye maelezo yafuatayo :*

- Sentensi ni fungu la maneno lenye muundo wa kiima na kiarifu na huwa na maana kamili ilhali kirai ni kipashio kinachoundwa kwa neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima na kiarifu.
- Sentensi huundwa kwa vipashio viwili ambavyo ni kiima na kiarifu.
- Kirai huundwa kwa neno moja au zaidi bila ya kuwa na kiima na kiarifu.
- Sentensi haiwezi kuwa kamili bila ya kitenzi.
- Kirai huweza kuwa kamili bila ya kitenzi.

**Zoezi la 7*(uk*.18)**

*Katika makundi, wanafunzi wabainishe sentensi kamili na kirai baadhi ya sentensi walizopewa. Mwalimu awaongoze kwenye jibu hili.*

1. Sentensi
2. Kirai
3. Sentensi
4. Kirai
5. Kirai

**SOMO LA 3: UTANZU WA RIWAYA**

**i) Malengo ya ujifunzaji**

Kuelezadhana ya riwayana kuitunga kwa kuzingatia sifazake.

**ii) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za majalada ya riwaya
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simujanja
- Ubao, chaki
- Sampuli ya vitabu vya riwaya
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu awe huru katika kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wanafunzi wenye matatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi**

**Kusoma na ufahamu: Sura moja ya riwaya kuhusu uchaguzi wa viongozi**

**Maswali ya ufahamu *(uk. 22)***

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome riwaya au dondoo walilopewa na kujibu maswali ya ufahamu husika. Yafuatayo ni majibu yanayopendekezwa.*

1. Inspekta Fadhili, Kazija, Mzee Bakari na askari.
2. Inspekta Fadhili alikuwa na jukumu la kiusalama, yaani, kuhakikisha kuwa kulikuwa na utulivu wakati wa mkutano.
3. Kwa sababu walistahili kujibu mashtaka ya kesi ya jinai mbali na madai ya ufisadi waliyokuwa wamelimbikiziwa.
4. Mwanasururu

5. Kuwasikiliza watetezi wakijielezea.
6. Alikuwa na ujeuri, majivuno na kujiona.
7. Kwa sababu alikuwa ametoa ahadi alizotaja awali na hakuwahi kuzitimiza.
8. Bwana Maksuudi alipokuwa Mkuu wa Wilaya alikula pesa za mkewe Mzee Japu ili kumtilia sahihi alipotaka kununua kiwanja cha kujengea nyumba.
9. Alipokewa kwa shangwe, nderemo, makofi na vigelegele.
10. Bwana Maksuudi ni fisadi, dhalimu na asiye na utu. (Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu sifa za Bwana Maksuudi)

**Msamiati kutokana na sura moja ya riwaya husika**

**Zoezi la 1*(uk. 23)***

*Katika makundi, wanafunzi washirikiane kuchagua neno lenye maana sawa na lile lililopigiwa mstari. Haya ni mapendekezo ya majibu :*

1. aliyokusanya
2. Wagombea wetu
3. tamko
4. kiburi
5. fimbo
6. Jina la kiongozi maalum
7. nguo za wanawake
8. Uhusiano
9. kikamweka kando

**Zoezi la 2 (uk. 23)**

*Katika makundi au jozi, wanafunzi wachague maana sahihi ya msamiati uliopigiwa mistari kutoka kwenye mabano. Yafuatayo ni majibu:*

1. aliyokusanya

2. Wagombea wetu
3. tamko
4. kiburi
5. fimbo
6. Jina la kiongozi maalum
7. nguo za wanawake
8. Uhusiano
**9.** kikamweka kando

**Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za riwaya**

***Zoezi la 3:***Katika makundi, wanafunzi wasome tena sura moja ya riwaya waliyosoma hapo awali kisha watathmini aina za wahusika na matukio katika kifungu hicho. Kwa mfano:

**i)** **Wahusika wakuu:** Hawa ni wahusika ambao wanahusishwa na takribani visa vyote katika riwaya. Wahusika hawa huhusishwa kutoka mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano: Bwana Maksuudi. 59 Fasihi katika Kiswahili.

**ii)** **Wahusika wasaidizi:** Hawa ni wahusika wanaosaidia kumjenga mhusika mkuu. Hujitokeza mara nyingi katika hadithi. Wahusika wasaidizi wanaweza kuwa na visa vyao. Kwa mfano: wanaweza wakawa ni marafiki na aila za wahusika wakuu. Kwa mfano: Kazija na Inspekta Fadhili.

**iii)** **Wahusika wadogo:** Hawa ni wahusika ambao wanafanya kazi ndogo sana katika fasihi kama vile kujenga maudhui au mandhari. Wahusika hawa wakitolewa, riwaya inaweza kuendelea bila kubadilika sana. Kwa mfano: Mzee Japu na Mzee Bakari.

**Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano kuhusu maudhui**

**Zoezi la 4*(uk* 24).**

*Katika makundi, wanafunzi wajadili maudhui yapatikanayo katika sura moja ya riwaya waliyoisoma. Baadhi ya maudhui ni:*

1. Ufisadi: Bwana Maksuudi anadaiwa kuitisha shilingi mia mbili ili kutia sahihi stakabadhi za mkewe Mzee Japu za kununua kiwanja cha kujengea nyumba.
2. Bidii: Umati unaokusanyika uwanjani unadhihirisha bidii na ari waliyonayo katika siasa. Wamekusanyika ili kuwasikiliza watetezi wao wakiomba kura.
3. Ujasiri: Kazija haogopi kumwambia Bwana Maksuudi ukweli kuhusu uongozi wake na tabia zake. Anasimama kidete na kusema yote ayajuayo kumhusu Bwana Maksuudi bila woga wowote. Biti Shomari pia haoni woga kusema kuwa yeye anamjua mtetezi wake. Anatamka haya kwa sauti ya juu zaidi.
4. Umoja: Umma unasawiriwa kuwa wenye umoja. Hii ni kwa sababu wanapoghadhabika, wanaungana kwa pamoja ili kupigana na viongozi hao wabaya. Kunao wanaobeba bakora na wengine wanafinyanga ngumi ili kulipiza kisasi.

**Zoezi la 5( *uk* 24)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wabainishe wahusika wanaopatikana katika dondoo la riwaya walilosoma pamoja na tabia zao. Wanafunzi waelekezwe kwenye maoni yafuatayo:*

**i) Bwana Maksuudi**: Mhusika huyu anasawiriwa kama fisadi na asiye na utu. Kwenye riwaya, Bwana Maksuudi anadaiwa kuitisha shilingi mia mbili ili kutia sahihi katika stakabadhi za kununua kipande cha kujengea nyumba. Huu ni ufisadi kwa kuwa kiongozi hafai kuchukua hongo ili kuwahudumia wananchi. Bwana Maksuudi anakosa utu pale ambapo tunaelezwa kuhusu yeye na mwanawe wa kiume ambao hawajaonana kwa mwaka mmoja sasa. Halikadhalika, Bwana Maksuudi anadaiwa kumnyang'anya mkewe mali yake na kusababisha kifo chake.

**ii) Kazija**: Kazija ni mhusika jasiri. Ni kutokana na ujasiri wake ndipo anaamua kusimama na kuzungumza kumhusu Bwana Maksuudi na matendo yake mabovu. Kazija haogopi lolote wala chochote. Anayatamka mambo mengi kumhusu Bwana Maksuudi na uongozi wake. Kazija pia ni msema ukweli kwa kuwa hadanganyi katika yote anayozungumza kumhusu Bwana Maksuudi.

**iii) Mzee Bakari**: Huyu ni mhusika mwoga. Baada ya Bwana Zanga kuzungumza, anawauliza wananchi iwapo walikuwa na swali. Mzee Bakari hasemi yaliyokuwa moyoni mwake kwa sauti ila anajisemea kimoyomoyo.

**iv) Inspekta Fadhili**: Huyu ni mpenda amani kwa kuwa zogo linapozuka, anaamua kuwatuliza wananchi kwa kuwaambia waiachie sheria itekeleze wajibu wake kufuatia madai waliyo nayo kwa Bwana Maksuudi na Bwana Zanga. Anafaulu katika kuutuliza umati wa watu kupitia sifa yake ya kupenda amani na pia umaarufu wake. Mwalimu ahakikishe wanafunzi wanawalinganisha wahusika hawa na watu katika maisha yao ya kila siku. Kupitia majadiliano haya, wanafunzi wafahamu sifa nzuri za kuiga na sifa hasi za kutupilia mbali.

**Sarufi:Kirai kivumishi**

**Zoezi la sarufi, (uk. 25)**

**A.**

1. Maneno '**nzuri kabisa'** ni kivumishi + kielezi, hivyo yanaunda kirai kivumishi.
2. Maneno '**mwenye sauti laini'** ni kivumishi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda kirai kivumishi.
3. Maneno '**yenye kuta ndefu**' ni kivumishi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda kirai kivumishi.
4. Maneno '**ndefu sana**' ni kivumishi + kielezi, hivyo yanaunda kirai kivumishi.
5. Maneno '**wenye kutukana viongozi**' ni kivumishi + kitenzi + nomino, hivyo yanaunda kirai kivumishi.
6. Maneno '**mwenye kuhifadhi sheria**' ni kivumishi + kitenzi + nomino, hivyo yanaunda kirai kivumishi.
7. Maneno '**nyingine yenye huduma nzuri**' ni kivumishi + kivumishi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda kirai kivumishi.
8. Maneno '**mzuri wa kuuzwa**' ni kivumishi + kivumishi '-a' unganifu + kitenzi, hivyo yanaunda kirai kivumishi.
9. Maneno '**mpungufu wa akili**' ni kivumishi + kivumishi '-a' unganifu + nomino, hivyo yanaunda kirai kivumishi.

**B.** Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu tofauti kati ya kirai nomino na kirai kivumishi.

Msingi wa kirai nomino ni nomino ambayo hutangulia na msingi wa kiraikivumishi ni kivumishi ambacho hutangulia. Kwa mfano:

1. Kirai kivumishi: Kitabu **kipya kikubwa** kimelowa maji. (kivumishi +kivumishi)
2. Kirai nomino: **Kitabu kipya kikubwa** kimelowa maji. (nomino+kivumishi+kivumishi)
3. Kirai kivumishi: Mtoto **mpole sana** amelala. (kivumishi +kielezi)
4. Kirai nomino: **Mtoto mpole sana** amelala.(nomino+kivumishi+kielezi)

***Zoezi la* 6, (uk. 26)**

*Katika makundi, wanafunziwabainishe virai vivumishi katika sentensi walizopewa kisha waelezane virai vivumishi hivyo vimeundwa kwa maneno gani.Majibu yanayopendekezwa ni haya yafuatayo:*

1. ‘fisadi sana (kivumishi+kielezi)
2. ‘mengine yenye utamu’ (kivumishi + kirai kivumishi)
3. ‘mwenye kuuza matunda’ (kivumishi +kirai kitenzi)
4. ‘zile nzuri kweli’ (kivumishi +kirai kivumishi)
5. ‘mwenye gari kubwa’ (kivumishi +kirai nomino)
6. ‘warefu sana’ (kivumishi + kielezi)
7. ‘wanyonge wote’ (kivumishi + kivumishi kingine)
8. ‘zile kabisa’ (kivumishi + kielezi)
9. ‘mwenyewe’ (kivumishi)
10. ‘matamu matano’ (kivumishi + kivumishi kingine)

## SOMO LA 4: UTANZU WA TAMTHILIYA

### i) Malengo ya ujifunzaji

Kuelezadhana ya tamthiliyana kuitunga kwa kuzingatia sifazake.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za majalada ya tamthiliya
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simujanja
- Ubao, chaki
- Sampuli ya vitabu vya tamthiliya
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Michoro au picha za jukwaa pamoja na waigizaji
- Mtandao wa intaneti

**Tanbihi**: Mwalimu awe huru katika kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wanafunzi wenye mahitaji maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu:Sura moja ya tamthilia**

**Maswali ya ufahamu *(uk. 34 )***

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome tamthilia au dondoo la tamthiliya na kujibu maswali ya ufahamu husika. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wameshiriki kwa kutumia Kiswahili sanifu. Yafuatayo ni majibu yanayopendekezwa:*

1. Wahusika watatu
2. Rahma ni shangazi yake Zainabu.
3. Aisha ni mjukuu wake Bi. Rahma. Kwa hivyo, Bi. Rahma ni nyanyake Aisha.

4. Sele anajitenga na watu, hamu ya chakula imemwisha, hasemi na akisema, anayosema hayaeleweki.
5. Wanashughulika na kazi zao nyingi tu ambazo siyo za kinyumbani.
6. Zainabu ni mtu makini sana. Anachunguza mienendo ya Sele na kujua tabia yake. Pia, anaelewa namna Aisha alivyo mpishi hodari. Zainabu pia ni mdadisi. Anamuuliza Bi. Rahma maswali mengi kuhusiana na suala la kumpeleka Sele kwa waganga ili afanyiwe kafara. Yeye pia ni karimu kwa kuwa anamwambia Aisha atayarishe chai itakayonywewa na bibiye pamoja na Sele.
7. Katika onyesho hili, wanajadili: afya, elimu, mabadiliko na ushirikina. Onyesho hili linahusu hali ya kiafya ya Sele ambaye anaonekana mnyonge kwa sababu hali chochote. Kila anachoandaliwa akila, anakula kidogo tu na mara nyingi hali kabisa. Kielimu, Aisha anaonekana kama aliyeegemea sana katika masomo ya kisasa na kusahau masuala ya kijamii hivi kwamba anawapuuza Bi. Rahma na Zainabu anapoingia chumbani na kuanza kupekuapekua penye vitabu. Mabadiliko yanadhihirika katika hali ya kimaisha ya Aisha na Sele. Sele anabadilika kiafya na kiakili kwa kuwa anaonekana msahaulifu sana na anayeongea maneno yasiyoeleweka. Aisha kwa upande wake, anabadilishwa na kisomo anachopata na pia mapito ya wakati. Anasema kwamba anaishi maisha ya kisasa wala siyo ya kale. Suala la ushirikina linajitokeza waziwazi pale ambapo Bi. Rahma anasisitiza kuhusu kumpeleka Sele kwa waganga ili afanyiwe kafara.
8. Aisha na Sele ni mke na mume.
9. Aisha ni mwenye mapuuza kwa kuwa anapoingia chumbani, hatilii maanani kuwa wazee wake wapo chumbani na wanastahili kuamkiwa. Yeye anatamka tu salamu za jumla na kuendelea na shughuli zake. Aisha pia anadhihirisha kuwa amepuuza hali ya mumewe Sele kwa kuwa anasema hamwelewi mara nyingi anapoongea ila hasemi iwapo kunacho anachofanya ili kuhakikisha kuwa amemwelewa. Aidha, Aishaamekengeuka hivi kwamba anasema kuwa mwanamke wa sasa hana tofauti na mwanamume kwani yeye anakwenda na majira ya usasa.
10. Bi. Rahma anashikilia kuwa Sele apelekwe kwa mganga ili afanyiwe kafara. Ana itikadi ya ushirikina.

**Msamiati kutokana na sura moja ya tamthilia husika**

***Zoezi la 1, (uk. 34)***

*Katika makundi, wanafunzi watafute msamiati mpya kutoka katika sura ya tamthilia waliyosoma hapo awali kisha waeleze maana zake na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Wazingatie muktadha wa sura husika. Kwa mfano:*

1. papa - samaki mkubwa kuliko samaki wote baharini, mwenye ngozi ngumu ya kijivu na meno makali.
2. kitoweo - mboga, mchuzi, nyama au samaki ambayo huliwa pamoja na chakula kingine.

***Zoezi la 2, (uk. 35)***

*Katika makundi, wanafunzi wanne wanne watumie mshale kwa usahihi kuonyesha maana za msamiati wa maneno katika sehemu ya A.Yafuatao ni majibu:*

| | |
|---|---|
| *1. G* | *2. I* |
| *3. H* | *4. E* |
| *5. CH* | *6. J* |
| *7. A* | *8. D* |
| *9. B* | *10. F* |

**Matumizi ya lugha:Sifa bainifu za tamthilia**

**Zoezi la** ***3, (uk.35 )***

*Katika makundi madogomadogo, wanafunziwajadilisifa bainifu za tamthiliya pamoja na tofauti iliyopo kati ya riwaya na tamthiliya. Katika uwasilishaji wa matokeo ya kazi za wanafunzi, mwalimu ahakikishe kuwa mambo yafuatayo yamegusiwa.*

**a) Sifa bainifu za tamthilia ni**:

1. Tamthilia huwa na maelezo ya jukwaa yanayoeleza namna jukwaa/ eneo la onyesho lilivyo.
2. Tamthilia hutawaliwa na mazungumzo na majibizano.

3. Tamthilia hutoa maelezo kuhusu wahusika – hisia zao, mavazi na matendo yao.
4. Tamthilia hugawika katika maonyesho/sehemu mbalimbali kutegemea matendo na matukio.
5. Tamthilia hushirikisha hadhira.
6. Tamthilia huhusisha mgogoro fulani hasa katika upeo wake.
7. Tamthilia huweza kutumia mtindo wa kishairi.
8. Utendaji wa tamthilia huambatana na miondoko - yaani, ni vipi viungo vya mwili vya mtendaji, kama vile: kichwa, mikono na miguu vinavyosongezwa.

**b) Tofauti kati ya utanzu wa riwaya na utanzu wa tamthilia**:

1. Riwaya huwa ndefu kimaandishi kuliko tamthilia.
2. Riwaya huandikwa kwa kinathari ilhali tamthilia huandikwa kwa muundo wa mazungumzo na majibizano.
3. Riwaya ina wahusika wengi kuliko tamthilia.

c) Wahusika katika tamthiliya :

- Wahusika bapa : ni wahusika wasiobadilika kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi Kwa mfano: mhusika mbaya anabakia kuwa mbaya kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi.
- Wahusika bapa -sugu : wahusika ambao huonyesha msimamo wao kulingana na masimulizi ya msanii.
- Wahusika ambao msimamo wao hutambulika kulingana na majina yao huitwa wahusika bapa-vielelezo. Kwa mfano: Mhusika Rehema ni mwenye huruma na neema kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi.
- Wahusika duara: Hubadilika kitabia katika fasihi. Hawa huwa hawana msimamo thabiti. Wao hubadilika kulingana na maudhui na mazingira. Wahusika hawa huitwa wahusika duara. Kwa mfano: Msichana aliyeanza akiwa mpole na mwadilifu anapobadilika na kuwa mtovu wa nidhamu, kahaba na asiyeshirikiana na mtu yeyote.
- Wahusika ambao huwa katikati ya wahusika bapa na wahusika duara huitwa wahusika wafoili. Hawa wanaweza kuchukua msimamo fulani katika masuala fulani lakini pia wanaweza kubadilisha msimamo huo wakati mwingine kulingana na hali. Wahusika hawa hutegemea wahusika duara na wahusika bapa ili kutoa sifa zao. Kwa mfano: Wahusika hawa wakiishi na mhusika bapa, wanaweza kuchukua msimamo wa mhusika huyo lakini

wakihama na waishi sana na mhusika mwengine, wanabadilika. Wahusika hawa aghalabu huwakilisha uhalisi wa binadamu.

**Zoezi la *4, uk. 36)***

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi washirikishwe katika tathmini sura ya tamthiliya waliyosoma kisha waelezane iwapo mwandishi wa sura hiyo alizingatia sifa bainifu za tamthilia kama zilivyoelezwa hapo juu kwenye maelezo muhimu.Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu iwapo mwandishi alizingatia sifa bainifu za tamthilia.*

***Kwa mfano**:*

1. *Kuna maelezo kuhusu jukwaa lilivyopangwa.*
2. *Maelezo kuhusu hisia za wahusika yametolewa hasa katika mabano.*

**Zoezi la *5, (uk. 36)***

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili mchango wa tamthilia za Kinyarwanda kutoka kipindi cha 'Urunana' yenye wahusika kama vile: Aline, Nadine, Stefano n.k. katika kuimarisha hatua za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi. Kila kikundi kiwasilishe majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao darasani. Tamthiliya iliyorekodiwa inastahili kuandaliwa na kutumiwa darasani ili kuwakumbusha mojawapo ya kipindi cha tamthiliya hizo.*

**Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo**

**Zoezi la*6, (uk. 36)***

*Katika makundi yanayolingana na idadi ya wachezaji kutoka tamthiliya 'Kijiba cha Moyo', wanafunzi washirikishwe katika uigizaji wa tamthilia hii. Hakikisha kuwa wanafunzi wote wamepewa wajibu katika mchezo huu. Pia, hakikisha kuwa vifaa vya kutumia jukwaani ni rahisi kupatikana.*

**Zoezi la** ***7, (uk. 36)***

*Kwa kurejelea tamthilia ya 'Urunana', katika makundi ya watatu watatu,*
*wanafunzi wajadili tabia za wahusika Stefano, James na Nadine katika tamthilia ya Kinyarwanda pamoja na mchango wa tamthilia hii katika kuwasaidia vijana kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi. Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao.*

**Zoezi la** ***8, (uk. 37)***

*Katika makundi ya watatu watatu, wanafunzi wasome tena sura ya tamthilia waliyosoma hapo awali kisha wajadili tabia za wahusika: Aisha, Zainabu na Bi. Rahma huku wakilinganisha tabia zao na maisha yao ya kila siku. Mapendekezo ya majibu ni haya yafuatayo:*

1. Aisha ni mhusika mwenye mapuuza kwa kuwa anapoingia chumbani, hatilii maanani kuwa wazee wake wapo chumbani na wanastahili kusalimiwa. Yeye anatamka tu salamu za jumla na kuendelea na shughuli zake. Aisha pia anadhihirisha kuwa amepuuza hali ya mumewe Sele kwa kuwa anasema hamwelewi mara nyingi anapoongea ila hasemi iwapo kunacho anachofanya ili kuhakikisha kuwa amemwelewa. Aidha, Aisha amekengeuka hivi kwamba anasema kuwa mwanamke wa sasa hana tofauti na mwanamume kwani yeye anakwenda na majira ya usasa.
2. Zainabu ni mtu makini sana. Anachunguza mienendo ya Sele na kujua tabia yake. Pia, anaelewa namna Aisha alivyo mpishi hodari. Zainabu pia ni mdadisi. Anamuuliza Bi. Rahma maswali mengi kuhusiana na suala la kumpeleka Sele kwa waganga ili afanyiwe kafara. Yeye pia ni karimu kwa kuwa anamwambia Aisha atayarishe chai itakayonywewa na bibiye pamoja na Sele.
3. Bi. Rahma ni mdadisi. Yeye anauliza maswali mengi kuhusu hali ya Sele pamoja na jamaa wengine. Halikadhalika, anamuuliza Aisha maswali mengi sana kuhusu namna anavyoishi. Yeye pia ni mcheshi. Anapoambiwa kuwa Sele hali vidagaa kwa kuvionea huruma kwa kuliwa na papa, yeye anamshauri Zainabu kumpikia papa ili alipize kisasi kwa niaba ya vidagaa. Ni mshirikina kwa kuwa anashikilia kauli kuwa Sele alistahili kupelekwa kwa

mganga ili afanyiwe kafara. Kwake, anaamini kuwa kumpeleka Sele kwa mganga ndiko kutamponya.

**Sarufi: Kirai kitenzi**

**Zoezi la *9, (uk. 39)***

*Katika makundi ya watatu watatu, wanafunzi waonyeshe virai vitenzi katika sentensi walizopewa kisha waelezane virai vitenzi hivyo vimeundwa kwa maneno gani. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wameyarejelea majibu hapa chini.*

1. ‘iliendelea kunyesha usiku kucha’ (vitenzi viwili + kielezi + kielezi)
2. ‘aliwafundisha wanafunzi kukariri mashairi’ (kitenzi + kirai nomino)
3. ‘walipalilia mimea yao’ (kitenzi + kirai nomino)
4. ‘alikuwa akipika wali’ ( vitenzi viwili + nomino)
5. ‘waliabiri basi jipya’ ( kitenzi + kirai nomino)

**Zoezi la *10,*(uk.39)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi watunge sentensi tano sahihi zenye miundo mbalimbali ya virai vitenzi. Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe miundo mbalimbali ya virai vitenzi. Kwa mfano:*

***1. Mwandishi** ameandika tamthilia nzuri sana**.***

***Kirai kitenzi kimeundwa kwa ‘kitenzi + kirai nomino chenye* nomino na *kirai***

***kivumishi’***

***2. Wanafunzi** watakariri shairi fupi**.***

***Kirai kitenzi kimeundwa kwa ‘kitenzi + kirai nomino chenye nomino na***

***kivumishi’***

***3. Gloria** ameamka alfajiri na mapema**.***

***Kirai kitenzi kimeundwa kwa 'kitenzi + kirai kielezi'***

4. ***Neli*** *atafika sasa*.

***Kirai kitenzi kimeundwa kwa 'kitenzi + kielezi'***

5. ***Mwalimu Julia*** *amewasili darasani humo*.

***Kirai kitenzi kimeundwa kwa 'kitenzi + kirai nomino chenye nomino na kivumishi'***

## SOMO LA 5: UTANZU WA USHAIRI

### i) Malengo ya ujifunzaji

Kuelezadhana ya ushairi na kutunga shairi kwa kuzingatia kanuniza utungaji wake.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za majalada ya mashairi
- Tarakilishi
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Sampuli ya vitabu vya mashairi.
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Vitabu vya mashairi
- Mashairi yaliyorekodiwa
- Mtandao wa intaneti

**Tanbihi:** Mwalimu awe huru katika kuandaa vifaa kadhaa vinavyoweza kumsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wanafunzi wenye mahitaji maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa au zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu:Shairi kuhusu kuyalinda mazingira**

**Maswali ya ufahamu(uk. 41 )**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome shairi husika na kujibu maswali ya ufahamu. Hakikisha kuwa wanafunzi wamesoma shairi kwa ufasaha kwa kuzingatia mdundo wa sauti kutokana na urari wa mizani pamoja na vina. Yalinganishe majibu ya wanafunzi na haya yafuatayo.*

1. Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.
2. Kilimo hutusaidia kujikimu kibiashara na hutupatia chakula.
3. Mazao ya mifugo ni muhimu kwa binadamu. Mifugo hutupatia maziwa na nyama kama chakula. Ngozi ya wanyama hutumika katika viwanda vya kuundia viatu na mikoba.
4. Beti sita
5. Nguru, dagaa na sangara
6. Hazina limetumika kama pesa.
7. Vina vya kati ni '**we**' na '**ma**' na vina vya mwisho ni '**mu**' na '**ra**'.
8. Mishororo thelathini (30) kwani kila ubeti una mishororo mitano (5).
9. Katika shairi, mwandishi anasema kuwa mashamba ni sharti yalimwe na mifugo ifugwe ili kujikimu kimaisha. Anasema pia biashara ifanywe kwa kuwa ni jukumu letu. Mwandishi anasisitiza umuhimu wa kuyalinda mazingira kwa kutokata miti. Maziwa sharti yalindwe ili tupate samaki wa kila aina na wanaoharibu maziwa wakemewe na kuadhibiwa. Mwandishi pia anasisitiza kuhusu usafi wa kila mahali kwa kuyalinda mabonde yanayotupa hewa safi.
10. Mizani ya ubeti wa kwanza:

Mshororo wa 1: 8, 8

Mshororo wa 2: 8, 8

Mshororo wa 3: 8, 8

Mshororo wa 4: 8, 8

Mshororo wa 5: 8, 8

**Matumizi ya msamiati (4k.42)**

***Zoezi la 1, (uk. 42)***

*Katika makundi, wanafunzi watafute msamiati mpya kutoka katika shairi walilosoma hapo awali kisha waeleze maana zake na kutunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Wazingatie muktadha wa shairi husika. Waruhusiwe kutumia kamusi inapohitajika.*

***Zoezi la 2, (uk. 42)***

*Katika makundi, wanafunzi watumie mshale kuonyesha maana sahihi ya msamiati ulio katika sehemu A na maana yake kutoka katika sehemu B. Yafuatayo ni majibu:*

| | |
|---|---|
| 1. - CH | 2. - A |
| 3. - G | 4. - I |
| 5. - H | 6. - D |
| 7. - J | 8. - E |
| 9. - F | 10. - B |

**Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za shairi**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili sifa bainifu za shairi katika Kiswahili pamoja na tofauti iliyopo kati ya utanzu wa shairi na utanzu wa riwaya. Waongoze wanafunzi kurejelea maoni yafuatayo.*

**i) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa shairi (uk. 42):**

1. Huwa na muundo maalum. Yaani, hupangwa katika beti zinazoundwa kwa mishororo.

2. Ni kazi ya kubuni kwa kutumia lugha. 3. Hufumbata ujumbe mpana wa maneno machache teule.
3. Hutumia tamathali za usemi kwa wingi zaidi kuliko tanzu nyingine.
4. Huzingatia sheria/ arudhi fulani katika utunzi wake.
5. Hushikana zaidi na hisi- hisi za mapenzi, chuki, faraja au hata werevu hujidhihirisha katika shairi.
6. Hubeba mawazo, fikira, falsafa na hisia za mwandishi katika mtazamo wake kibinafsi na kuziwasilisha kwa hadhira.

**ii) Tofauti kati ya utanzu wa shairi na utanzu wa riwaya**

1. Shairi huandikwa kwa lugha ya mkato na hupangwa katika beti ilhali riwaya huandikwa kwa lugha ya kinathari na hupangwa katika aya kadhaa.
2. Maneno katika shairi huwa teule na huweza kuandikwa kwa mbinu za kisanaa kama vile kufupisha (inkisari) na kubadilisha namna ya mwendelezo wa maneno fulani (tabdila) ilhali maneno katika riwaya hayabadilishwi kimaendelezo kwani riwaya huandikwa kwa lugha sanifu aghalabu bila ya kuiboronga.
3. Shairi halitoi maelezo kuhusu wahusika wake ilhali riwaya huwa na maelezo ya wahusika kuhusu wasifu wao, mavazi, tabia na dosari zao.

**Zoezi la 3 (uk.43)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili maana ya vina, kibwagizo, beti, mizani, mishororo ; wahusishe vipera hivi pamoja mawazo makuu na shairi 'Tuyalinde Mazingira'. Waelekeze wanafunzi kwenye matokeo haya :*

1. Vina ni silabi za namna moja zinazopatikana katikati na/au mwishoni mwa mishororo. Katika shairi hili, vina vya kati ni 'we' na 'ma' ilhali vina vya mwisho ni 'mu' na 'ra'.
2. Kibwagizo ni mshororo wa mwisho unaorudiwarudiwa katika kila ubeti. Kibwagizo hubeba kiini cha shairi. Kibwagizo hurudiwarudiwa katika kila ubeti. Kibwagizo cha shairi hili ni: Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.
3. Ubeti (wingi ni beti) ni kifungu katika shairi kinachojitosheleza kimaana. Shairi hili lina beti sita.

4. Mizani ni silabi zinazotamkika katika maneno ya mshororo. Shairi hili lina mizani ya kumi na sita (16) katika kila mshororo, themanini (80) katika kila ubeti na mia nne na themanini (480) katika shairi zima.
5. Mshororo ni mstari katika ubeti. Shairi lina mishororo mitano katika kila ubeti na kwa jumla, shairi lina mishororo thelathini (30). Mshororo wa kwanza huitwa mwanzo, wa pili ni mloto, wa tatu ni mleo na wanne ni mwandamizi.
6. Mawazo makuu katika shairi ni jumla ya mambo yanayozungumziwa kwenye shairi husika. Katika shairi hili, mwandishi anasema kuwamashamba ni sharti yalimwe na wanyama wafugwe ili kujikimu kimaisha. Anasema pia biashara ifanywe kwa kuwa ni jukumu letu. Mwandishi anasisitiza umuhimu wa kuyalinda mazingira kwa kutokata miti. Maziwa sharti yalindwe ili tupate samaki wa kila aina na wanaoharibu maziwa wakemewe na kuadhibiwa. Mwandishi pia anasisitiza kuhusu usafi wa kila mahali kwa kuyalinda mabonde yanayozaa hewa safi.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Zoezi la 4,(uk.43)**

***Zoezi hili limerekebishwa kama ifuatavyo:***

*Kwa kusikiliza shairi lililorekodiwa, wanafunzi katika jozi wajadili dhamira kuu iliyozungumziwa katika shairi husika.*

**Sarufi :Maana ya kishazi**

**Zoezi la sarufi (uk.43 – 44)**

*Katika jozi, wanafunzi wabainishe sehemu za sentensi na kuainisha vishari huru vishazi na vishazi tegemezi. Linganisha matokeo yao na haya yafuatayo:*

1. Sehemu ya ‘lililotiwa hamira’ siyo sentensi kamili (ni kishazi tegemezi). Sehemu ya ‘andazi linafura na kujaa vizuri’ ni sentensi kamili (ni kishazi huru).
2. Sehemu ya ‘waliotia bidii mwaka jana’ siyo sentensi kamili (ni kishazi tegemezi). Sehemu ya ‘wanafunzi walipita mtihani’ ni sentensi kamili (ni kishazi huru).

3. Sehemu ya 'alilonunua' siyo sentensi kamili (ni kishazi tegemezi). Sehemu ya 'shati limefuliwa na dadake' ni sentensi kamili (ni kishazi huru).
4. Sehemu ya 'Kalisa anasoma Hisabati' ni sentensi kamili (ni kishazi huru). Sehemu ya 'Gatete anachora michoro' ni sentensi kamili (ni kishazi huru).
5. Sehemu ya 'nitawajibika' ni sentensi kamili (ni kishazi huru). Sehemu ya 'utafaidika' ni sentensi kamili (ni kishazi huru).

**Zoezi la 5 (uk.44)**

*Katika makundi, wanafunzi wachunguze sentensi zifuatazo kisha waonyeshe vishazi vinavyojitokeza katika sentensi hizi.Yafuatayo ni majibu:*

1. a. aliyeishi hapa naye (kishazi tegemezi)
   b. Mwanamke alipoteza mtoto wake. (kishazi huru)
2. a. aliyepoteza maisha jana (kishazi tegemezi)
   b. Mtoto amepokelewa mbinguni. (kishazi huru)
3. a. alipomaliza masomo ya chuo mwaka jana naye (kishazi tegemezi)
   b. Gisa alipata shahada ya kwanza. (kishazi huru)
4. a. Watoto wanacheza. (kishazi huru)
   b. Wazazi wamekaa sebuleni. (kishazi huru)
5. a. Wavulana walishinda mabao mengi. (kishazi huru)
   b. Refa amewaonea sana. (kishazi huru)
6. Kamana alifua nguo zake. (kishazi huru)
7. Mutoni ataondoka kesho. (kishazi huru)
8. Ninawapenda wote. (kishazi huru)
9. ` Waziri alizindua mkutano. (kishazi huru)
10. Mwenyekiti alisoma hotuba nzuri sana. (kishazi huru)

**Zoezi la 6 (uk. 45)**

*Kwa kazi binafsi, mwanafunzi achague kitenzi kinachofaa na kujaza nafasi iliyoachwa wazi. Chunguza ikiwa amefaulu kutoa majibu yafuatayo:*

1. angewahi      2. alipigwa kalamu

3. tutafurahia      4. nitamweleza

| | |
|---|---|
| 5. atapelekwa | 6. kukabidhiwa |
| 7. alimwandalia | 8. aliwadharau |
| 9. kutupatupa | 10. Aliyefyatua |

**Zoezi la 7, (uk. 45)**

*Wanafunzi wajigawe katika makundikisha waelezane aina za vishazi wanavyovifahamu pamoja na kuvitungia sentensi sahihi kwa kila aina ya kishazi.*

## 1.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 1.5.1. Maelezo ya Ziada kwa Mwanafunzi

***Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi ni maelezo ambayo yameandaliwa kuongezea au kukamilisha yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima yazingatiwe katika ufundishaji wa somo husika. Yafuatayo ni maelezo zaidi kuhusu somo la 4 «*** **Utanzu wa tamthiliya » na somo la 5 « Utanzu wa Ushairi .»**

☞ **Somo la 4 : Utanzu wa tamthiliya**

**Matumizi ya lugha (Uk.35): Dhana ya tamthiliya katika Kiswahili**

Tamthilia ni sanaa ambayo huwasilisha mchezo wa kuigiza kwa njia ya maandishi. Majina ya wahusika huandikwa katika upande wa kushoto, kisha koloni, halafu hufuatiwa na maneno halisi yaliyotamkwa na mhusika huyo. Kwa maana nyingine,tTamthilia ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa ili uigizwe jukwaani kwa kuwasilisha ujumbe kwa jamii.

**Aina za jukwaa**

Kuna aina mbili za jukwaa:

- Jukwaa la akilini kama hali ya kujiundia akilini k.v. mchezo unaoigizwa redioni.
- Jukwaa la hadharani, yaani mahali ambapo maonyesho ya tamthilia yanaigiziwa mbele ya watazamaji au wasikilizaji.

**Aina za tamthilia**

Tamthilia au mchezo wa kuigiza huwa na aina mbalimbali kulingana na dhamira kuu inayoendelezwa. Utaipata tamthilia ya mapenzi, ya kihistoria, ya kisiasa, ya kidini, ya kiuchumi, n.k. Tamthilia hizi zote huangukia baadhi ya makundi makuu yafuatayo:

**(a) Tanzia**

Ni aina ya tamthilia iliyojaa, huzuni ndani yake, mikasa, matokeo ya vifo na mateso makali. Mwisho wa hadithi za aina hii huwa ni wa masikitiko, maanguko na hasara kubwa kwa mhusika mkuu au jamii inayoibushwa. Wengine huita aina hii tamthilia simanzi au trejedia.

**(b) Ramsa**

Tamthilia zenye kuchekesha kutokana na utani, mzaha, kejeli, maneno yaonyeshayo ujinga, n.k. Iwapo hadithi hizi huwa na dhana ya uchekeshaji, lengo lake ni kukosoa jamii, watawala na tabia mbaya na watu binafsi. Aina hii huitwa tena Tamthilia cheshi au komedia.

**(c) Tanzia – ramsa**

Tanzia – ramsa au simanzi – cheshi ni mchezo wenye sifa za ramsa, lakini ndani ya uchekeshaji wake na tanzia kama vile kifo cha mhusika mkuu au kuanguka kwa jamii. Pengine huitwa Trejikomedia.

**Sifa za tamthilia**

Sifa za mchezo wa kuigiza hujitosheleza kama ifuatavyo:

- Wahusika wake huwakilishwa na watendaji ambao hujieleza au hutenda wenyewe.
- Watazamaji au wasikilizaji hushirikishwa.
- Mchezo hutokea kwenye jukwaa mbele ya hadhira.
- Mapambo hutumiwa ili kuashiria kubadilika kwa mazingira au wakati.
- Hutumia mbinu za lugha kama vile chuku, tanakali za sauti, tamathali na nyinginezo.
- Huhusisha aina nyingine za sanaa kama vile ushairi na nyimbo.

☞ **Somo la 5 : Utanzu wa Ushairi**

**Matumizi ya lugha (uk.42) : Dhana ya mashairi**

Ushairi ni utungo wa kisanaa unaotumia maneno ya mkato na lugha yenye kuvutia (lugha teule na mpangilio fulani wa maneno badala ya kutumia lugha natharia) na ambayo yamepangwa kwa urari wa mizani na vina maalum. Ushairi unaweza kuwa kipera cha fasihi simulizi (nyimbo) na pia katika fasihi andishi kwa sababu mashairi yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya kukariri na pia kwa njia ya maandishi. Mashairi yanayoghanwa badala ya kuimbwa huitwa maghani.

Kuna aina kuu tatu za ushairi: Mashairi, Ngonjera na Tenzi.

**(a) Shairi:**

Shairi ni mtungo wa kisanaa wenye mpangilio maalum na kutumia lugha ya mkato na mnato kwa kuelezea hisi na mawazo ya jamii husika na kuwasilisha ujumbe fulani. Mashairi hugawika katika makundi mawili: mashairi ya kimapokeo au mashairi arudhi na mashairi huru. Mashairi arudhi hutungwa kwa kufuata au kuzingatia sheria na kanuni au kaida za utunzi kama vile kuzingatia vina, idadi fulani ya mizani, mishororo na vipande vya mishororo. Kulingana na idadi ya mishororo katika kila ubeti, mashairi huweza kugawika tena katika aina mbalimbali:

1. Tathmina ni shairi lenye mshororo mmoja kwa kila ubeti.
2. Tathnia na shairi lenye mishororo miwili kila ubeti.
3. Tathlitha ni shairi lenye mishororo mitatu kila ubeti.
4. Tarbia Ni shairi lenye mishoro minne kwa kila ubeti.
5. Takhmisa ni shairi lenye mishororo mitano kwa kila ubeti.
6. Tasdisa shairi lenye mishororo sita.

**(b) Ngonjera:**

Ngonjera ni shairi lenye malumbano na majibizano kati ya watu wawili au zaidi.

**(c) Tenzi :**

Tenzi ni aina ya shairi ambayo ni mtungo mrefu wa kishairi unaoelezea historia au kisa fulani na ambao hauna vina vya kati katika mistari yake bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mstari wa mwisho wa ubeti.

Kuna mambo mengine muhimu kuhusu shairi. Mishororo ya shairi huwa na majina maalum.

Mwanzo huwa ni mshororo wa kwanza wa ubeti.

Mloto huwa ni mshororo wa pili wa ubeti.

Mlea huwa ni mshororo wa tatu wa ubeti

Kituo huwa ni mshororo wa mwisho wa ubeti.

Kuna aina mbili za vituo ambazo ni kituo kimalizio na ktuo kibwagizo. Kituo kimalizio ni kituo ambacho hakirudiwi mwishoni mwa kila ubeti katika shairi. Kituo kibwagizo ni kituo kinachorudiwarudiwa mwishoni mwa kila ubeti.

Vipande au sehemu za mishororo ni vifuatavyo:

Ukwapi : Ni kipande cha kwanza cha mshororo.

Utao: Ni kipande cha pili cha mshororo.

Mwandamizi : Ni kipande cha tatu cha mshororo.

### 1.5.2. Maelekezo ya ziada kwa mwalimu

***Maekelekezo haya yamependekezwa kwa sababu tofauti. Kwanza, yameandaliwa kwa ajili ya kukamilisha au kuimarisha kazi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Pili, yamefikiriwa kwa madhumuni ya kubadilisha kazizilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi ambazo zimetathminiwa kutofaa katika nafasi zilimowekwa. Kwa hiyo, ni sharti kwa mwalimu kuchagua kazi anayoiona kuwa ya lazima au muhimu baadhi ya kazi zilizopendekezwa ama katika kitabu cha mwanafunzi au katika kitabu hiki cha mwalimu.***

- ✓ **Kazi za kuandika ziongezewe katika kila somo husika kama ifuatavyo** :

**Utanzu wa hadithi fupi** :

***Zoezi la kuandika:*** *Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge hadithi fupi kulingana na sifa za hadithi fupi. Mwalimu amkumbushe sifa zifuatazo:*

1. Hadithi fupi huwa na wahusika wachache. Huwa na mhusika mmoja mkuu ambaye humwongoza msomaji.
2. Hadithi fupi huwa fupi na inaweza kusomeka katika kikao kimoja.
3. Hadithi fupi hushughulikia tukio moja kuu katika maisha ya mhusika mkuu.
4. Hadithi fupi huwa haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo ikilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi andishi.
5. Hadithi fupi huhusisha usimulizi wa moja kwa moja.

**Utanzu wa riwaya:**

***Zoezi la kuandika:*** *Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge riwaya kulingana na sifa za riwaya katika Kiswahili. Mwalimu amkumbushe sifa zifuatazo :*

- Riwaya ni utanzu wa fasihi andishi.
- Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo huchukua muda mrefu kuandikwa na huwa na wahusika wengi na wa aina nyingi (wakuu na wadogo).
- Mhusika mkuu ndiye huwakilisha mawazo muhimu ya mwandishi.
- Katika riwaya, matukio mara nyingi huwa ni tata.
- Mtunzi wa riwaya hajui maoni ya wasomaji, yaani anajitenga na hadhira.
- Riwaya huwa na maneno mengi sana, zaidi ya kurasa sitini.

*Pia, mwalimu ataje kiwango cha idadi ya kurasa.*

**Utanzu wa tamthiliya:**

***Zoezi la kuandika:*** *Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge tamthiliya kulingana na sifa za tamthiliyya katika Kiswahili. Mwalimu amkumbushe sifa zifuatazo :*

1. Tamthilia huwa na maelezo ya jukwaa yanayoeleza namna jukwaa/ eneo la onyesho lilivyo.
2. Tamthilia hutawaliwa na mazungumzo na majibizano.
3. Tamthilia hutoa maelezo kuhusu wahusika – hisia zao, mavazi na matendo yao.
4. Tamthilia hugawika katika maonyesho/sehemu mbalimbali kutegemea matendo na matukio.
5. Tamthilia hushirikisha hadhira.
6. Tamthilia huhusisha mgogoro fulani hasa katika upeo wake.
7. Tamthilia huweza kutumia mtindo wa kishairi.
8. Utendaji wa tamthilia huambatana na miondoko - yaani, ni vipi viungo vya mwili vya mtendaji, kama vile: kichwa, mikono na miguu vinavyosongezwa.

**Utanzu wa ushairi:**

***Zoezi la kuandika:*** *Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge shairi lenye beti tatu au zaidi kwa kuzingatia kanuni za utungaji wa shairi. Mwalimu amkumbushe mwanafunzi mambo muhimu yafuatayo:*

Shairi ni kazi ya sanaa ya lugha teule na lugha ya kisanaa inayotumia mpangilio na uteuzi maalum wa maneno na sauti ili kupitisha ujumbe fulani huitwa shairi.

Shairi huwa na vipashio vifuatavyo:

- Vina - silabi za mwisho wa kila kipande katika mshororo.
- Mizani - idadi ya silabi katika maneno ya kila mshororo.
- Mshororo - mstari mmoja wa maneno katika ubeti wa shairi.
- Ubeti - kifungu cha mishororo kadhaa.
- Mloto - mshororo wa pili katika ubeti
- Kimalizio/Kiishio - mshororo wa mwisho katika ubeti usiorudiwarudiwa katika kila ubeti.
- Kibwagizo - mshororo wa mwisho katika ubeti unaorudiwarudiwa kila ubeti.
- Mshairi hufupisha au hurefusha maneno ili kutosheleza idadi ya mizani.

## 1.6 TATHMINI YA MADA YA KWANZA

*Tathmini hii ipendekezwe kuwa jaribio la jumla. Kwa kazi binafsi, kila mwanafunzi anapaswa kujibu maswali yote aliyopewa kwa kutumia karatasi. Inambidi mwalimu kuyaanda majibu awali pamoja na vipimo vya tathmini kwa kila jibu.*

**Tanbihi:** Mwalimu halazimishwi kutoa jumla ya maswali yote kwa wanafunzi.

Majibu ya tathmini ya mada ya 1

**Zoezi la 1, (uk. 46)**

a) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa riwaya:

1. Riwaya ni utanzu wa fasihi andishi.
2. Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo huchukua muda mrefu
kuandikwa na huwa na wahusika wengi na wa aina nyingi (wakuu na
wadogo).
3. Mhusika mkuu ndiye huwakilisha mawazo muhimu ya mwandishi.
4. Katika riwaya, matukio mara nyingi huwa ni tata. Migogoro mingi
hujengwa ili kukuza maudhui na mtiririko.
5. Mtunzi wa riwaya huwa hayafahamu maoni ya wasomaji, yaani hujitenga

na hadhira.

6. Riwaya huwa na maneno mengi sana, zaidi ya kurasa sitini.
7. Riwaya huwa na maelezo ya simulizi kulingana na vile hadithi inavyotokea kiwakati na kimasafa.
8. Riwaya huwa na maelezo ya wahusika kuhusu wasifu wao, mavazi yao, tabia zao, sifa na dosari, matendo yao yanavyoathiri nafsi zao na kuwaathiri wahusika wengine.
9. Riwaya huwa na urefu wa kutosha kuyashughulikia mahitaji ya mtunzi.
10. Riwaya huchunguza kwa kina jamii inavyosawiriwa.

b) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa ushairi:

1. Utanzu wa ushairi huwa na muundo maalum.
2. Shairi hufumbata ujumbe mpana kwa kutumia maneno machache teule.
3. Ushairi hutumia tamathali za semi kwa wingi zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi andishi.
4. Utanzu wa ushairi huzingatia sheria (arudhi) maalum katika utunzi wake.
5. Ushairi ni kazi ya kubuni kwa kutumia lugha teule.

c) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa tamthilia:

1. Tamthilia hutawaliwa na mazungumzo na majibizano.
2. Tamthilia huwa na maelezo ya kumwelekeza msomaji ambayo huwa kwenye mabano na ambayo aghalabu hupendekeza jukwaa litakavyoonekana wakati wa maigizo.
3. Tamthilia hugawika katika sehemu (matendo na maonyesho) mbalimbali kutegemea matendo na matukio husika.
4. Tamthilia hushirikisha hadhira.
5. Tamthilia huwa na mgogoro fulani unaotanda katika hadithi nzima.

d) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa hadithi fupi:

1. Huwa ni fupi inayoweza kusomeka katika kikao kimoja.
2. Huwa na wahusika wachache.
3. Huwa na mhusika mmoja mkuu ambaye humwongoza msomaji.
4. Hushughulikia tukio moja muhimu katika maisha ya mhusika mkuu.
5. Huwa haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo kwa kulinganisha na tanzu nyingine za fasihi andishi.
6. Hadithi fupi huhusisha usimulizi wa moja kwa moja.

7. Hadithi fupi hulenga sana kuibua hisia za msomaji kuliko kuchochea fikira zake.
8. Hadithi fupi huenda haraka kimatendo, kiwakati, kimasafa na kimatukio.

**Zoezi la 2, (uk. 46)**

1.a) Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo huchukua muda mrefu kuandikwa na huwa na wahusika wengi na wa aina nyingi (wakuu na wadogo) ilhali hadithi fupi huwa haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo kwa kulinganisha na huwa na wahusika wachache. Hadithi fupi huweza kusomeka katika kikao kimoja kinyume na riwaya.

b) Tamthilia hutawaliwa na mazungumzo na majibizano ilhali shairi hufumbata ujumbe mpana kwa kutumia maneno machache teule yaliyopangwa kwenye beti kadhaa.

2. Maudhui ni ujumbe au mawazo makuu ya mtunzi kwa wasomaji wake ilhali dhamira ni sababu, lengo au nia ya mtunzi kubuni kazi yake ya kifasihi.

**Zoezi la 3, (uk. 47)**

a. Mtoto mrefu ameshinda mbio.
   ‘ameshinda mbio’ ni kirai kitenzi
b. Nataka unipe kisu kikali.
   ‘kisu kikali’ ni kirai nomino
c. Sima na wali ni chakula kitamu.
   ‘sima na wali’ ni kirai nomino
   ‘chakula kitamu’ ni kirai nomino
d. Kalamu yenye rangi ya kijani iko wapi?
   ‘yenye rangi ya kijani’ ni kirai kivumishi
e. Wazee wenye kondoo hawa wamekuja.
   ‘wenye kondoo hawa’ ni kirai kivumishi
f. Wanafunzi waliondoka alfajiri na mapema.
   ‘alfajiri na mapema’ ni kirai kielezi
g. Mama alikuwa amelala.
   ‘alikuwa amelala’ ni kirai kitenzi

**Zoezi la 4, (uk.  47)**

a. Mama alifika leo alasiri.
   ‘Mama alifika leo alasiri’ ni kishazi huru.
b. Mjomba alifika asubuhi lakini hakutuletea mkate.

'Mjomba alifika asubuhi' ni kishazi huru.

'hakutuletea mkate' ni kishazi huru.

c. Wachezaji ambao ni shupavu walishinda.

'Wachezaji walishinda' ni kishazi huru.

'ambao ni shupavu' ni kishazi tegemezi.

d. Waziri alifika baada ya watu kuondoka.

'Waziri alifika' ni kishazi huru.

'baada ya watu kuondoka' ni kishazi tegemezi.

e. Tunda lililo tamu litaliwa.

'Tunda litaliwa' ni kishazi huru.

'lililo tamu' ni kishazi tegemezi.

**Zoezi la 5, (uk.  47)**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi, kwa mfano:

Fasihi huelimisha, huonya, huburudisha, huhifadhi historia ya jamii, hupongeza, hufunza maadili na kadhalika.

**Zoezi la 6, (uk. 48)**

a. Siyo sentensi kamili kwa sababu haina kitenzi.
b. Siyo sentensi kamili kwa sababu haina kitenzi.
c. Ni sentensi kamili kwa sababu ina kitenzi 'ni'.
d. Siyo sentensi kamili kwa sababu haina kitenzi.
e. Ni sentensi kamili kwa sababu ina kitenzi 'huli'.

**Zoezi la 7, (uk. 48)**

a) 'Mwanafunzi mwerevu na mpole' ni kiima na 'ametuzwa na mwalimu mkuu' ni kiarifu.
b) 'Shule yetu ya sekondari' ni kiima na 'ina wanafunzi wengi sana' ni kiarifu.
c) 'Choo chao' ni kiima na 'kimesafishwa na topasi yule' ni kiarifu.
d) 'Mama na baba' ni kiima na 'wanatazama runinga waliyonunuliwa jana' ni kiarifu.
e) 'Mimi na yeye' ni kiima na 'tuna bidii katika masomo yetu' ni kiarifu.

## 1.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI

### 1.7.1 Kazi za urekebishaji

1. Fasihi andishi ni nini?
2. Taja tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili
3. Jadili umuhimu wa fasihi andishi
4. Kwa kutemea sentensi ifuatayo, onesha vifungu vyake na kuvitolea maana.

Kazi za fasihi andishi huimarisha uchumi wa jamii.

**Majibu**

1. Fasihi andishi ni mojawapo ya tanzu za fasihi ya lugha yoyote. Ni sanaa changa ukilinganisha na fasihi simulizi ambayo hutumia maandishi au hati mbalimbali.
2. Tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili ni zifuatazo :
   - Hadithi fupi
   - Riwaya
   - Tamthiliya
   - Nyimbo na mashairi
   - Aina tofauti za insha
3. Umuhimu wa fasihi andishi :

- Fasihi andishi huiongoza na kuielekeza jamii: Fasihi andishi ni wenzo muhimu ya kuwaelekeza watu na kuwakanya dhidi ya kufanya jambo fulani. Kwa mfano, kupitia kwa mashairi andishi, tabia ambazo hazikubaliki katika jamii huweza kukejeliwa.
- Fasihi andishi huhifadhi historia ya jamii fulani: Kwa kusoma hadithi zinazohusu matukio halisi ya kihistoria katika jamii na pia kuhusu mila na tamaduni za jamii husika, historia ya jamii hiyo huhifadhiwa.
- Huakisi na kuonyesha imani, itikadi na msimamo wa jamii fulani kuhusu mambo mbalimbali.

4. - Huburudisha wanajamii: Mashairi mengi husomwa kwa ajili ya burudani. Halikadhalika, riwaya na hadithi fupi pia husomwa kama njia ya kujiburudisha.

- Hukuza na kuendeleza stadi za lugha miongoni mwa wanajamii: Kutokana na mbinu mbalimbali za uandishi ambazo hutumiwa na wasanii wengi, ukuzaji wa stadi ya utungaji na uandishi hukuzwa.
- Hukuza na kuimarisha uhusiano kati ya wanajamii mbalimbali.

5. Kazi za fasihi andishi huimarisha uchumi wa jamii.

Sentensi hii imeundwa na sehemu kuu mbili ambazo ni kiima na kiarifu. Kiima ni neno au kundi la maneno yanayoonyesha mtenda na huja kabla ya kitenzi katika sentensi. Kiarifu ni sehemu ya sentensi inayoanzia kwenye kitenzi pamoja na maneno yanayofuata kitenzi hicho.

### 1.7.2 Kazi za uimarishaji

**Maswali :**

1. Eleza faida za fasihi andishi
2. Ni tofauti gani iliyopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi
3. Kwa kutumia mifano, bainisha tanzu za fasihi andishi
4. Kwa kutemea sentensi ifuatayo, tenganisha kishazi huru na kishazi tegemezi.

Kazi za fasihi andishi ni muhimu kwa sababu zinaimarisha uchumi wa jamii.

**Majibu:**

1. Uandishi wa tanzu za fasihi andishi kama vile hadithi fupi, riwaya, tamthiliya pamoja na nyimbo na mashairi ni njia moja ya kujitegemea kwa waandishi wa kazi hizo. Wanaweza kuuza kazi zao katika shule, maktabani, kwenye mitandao ya intaneti, mashirika yanayohudumia elimu, kwa watu binafsi, n.k. Wanaweza pia kupewa zawadi kutoka mashindano ya uandishi wa tanzu hizo. Hali kadhalika, washairi, waimbaji na waigizaji wa tamthiliya huchukuliwa kama waajiriwa wengine kwa sababu kazi zao huwa zinathamaniwa sana.
2. Fasihi simulizi ni fasihi ya zamani iliyotangulia na kuwepo kwa binadamu. Fasihi hii huwasilishwa kwa mdomo na majina asili ya wasanii wake hayajulikani mpaka leo. Kinyume na haya, fasihi andishi ni fasihi changa inayotumia maandishi. Majina ya wasanii wa fasihi hupatikana wazi kwa sababu huwa yameandikwa na kuhifadhiwa kwa njia ya kiteknolojia.

Tazama maelezo ya ziada :

| Fasihi Simulizi | Fasihi Andishi |
|---|---|
| ✓ Huwasilishwa kwa njia ya mdomo na/au matendo. | Huwasilishwa kwa njia ya maandishi |
| ✓ Ni mali ya jamii. | Kazi andishi ni mali ya mwandishi (na mchapishaji) |
| ✓ Msimulizi anaweza kubadilisha sehemu fulani | Kitabu kilichoandikwa hakiwezi kubadilishwa |
| ✓ Huhifadhiwa akilini na kusambazwa kwa njia ya masimulizi. | Huhifadhiwa kwa maandishi na kusambazwa kwa njia ya maand |
| ✓ Kazi simulizi hubadilika na wakati | Kazi andishi haibadiliki na wakati |
| ✓ Huhitaji msimulizi na hadhira yake wawe mahali pamoja wakati wa masimulizi | Msomaji anaweza kusoma kitabu cha hadithi peke yake, mahali popote, wakati wowote |
| ✓ Umri: Ina umri mkubwa kuliko fasihi andishi. Pengine huitwa fasihi kongwe. | Ina umri mfupi kuliko fasihi simulizi. Hii inatokana na ukweli kuwa maandishi yamegunduliwa hivi karibuni. |

3. Fasihi andishi hujigawa katika tanzu kuu muhimu kama ifuatavyo :
   - Hadithi fupi. Mfano: Mtoto yatima na mama wakambo
   - Riwaya. Mfano : Utengano, Adili na Nduguze, n.k
   - Tamthiliya. Mfano : Hawala ya Fedha, Kijiba cha Moyo, n.k
   - Mashairi. Mfano : Tuyalinde mazingira
4. Kazi za fasihi andishi ni muhimu kwa sababu zinaimarisha uchumi wa jamii.

Sentensi hii imeundwa na vishazi viwili ; yaani kishazi huru na kishazi tegemzi. ‘Kazi za fasihi andishi ni muhimu’ ni kishazi huru kwa sababu sehemu hii imeunda sentensi kamili yenye

maana inayojitoshereza. ‘kwa sababu zinaimarisha uchumi wa jamii’ ni kishazi tegemezi kwa sababu sehemu hii haiundi setensi kamili. Maana inategemea sehemu ya kwanza ili ikamilike.

### 1.7.3 Kazi kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

**Maswali :**

1. ‘Hadithi simulizi, methali na nahau hupatiakana leo kwa maandishi. Kwa hiyo, vipera hivi ni baadhi ya kazi za fasihi andishi’. Je, unakubaliana na kauli hii? Tetea msimamo wako.
2. Mazingaombwe ni baadhi ya michezo ya kuigiza. Jadili.

**Majibu:**

1. Ingawa hadithi, methali na nahau hupatikana leo kwa maandishi, hatuwezi kupotoshwa na ukweli huu ili tuainishe kazi hizi katika utanzu wa fasihi andishi. Ni lazima tukumbuke kuwa asili ya kazi hizi ni mdomo au masimulizi. Pia, asili ya majina ya wasanii wa kazi hizi na enzi zao haijulikani rasmi. Kwa mfano, huwezi kutoa jina la mtu aliyebuni ‘akili ni mali’ kama methali au kuhakikisha methali hii ilianza kutumiwa lini.
2. Kwa kawaida, michezo ya kuigiza hulazimisha kuwepo kwa waigizaji, jukwaa pamoja na hadhira. Mazingaombwe, kama mchezo au mambo ya kudanganya macho ili yaone kisichokuwepo ama yasione kilichopo, huhusisha pia mwigizaji au mchezaji, mandhari kama jukwaa pa kuchezea pamoja na watazamaji au hadhira.

## MADA KUU YA 2 : FASIHI KATIKA KISWAHILI

## MADA NDOGO YA 2: UHAKIKI WA TANZU ZA FASIHI ANDISHI

### 2.1. Uwezo upatikanao katika mada

Kuhakiki kitaaluma kazi mbalimbali za fasihi andishi na kunyambua vitenzi vya Kiswahili.

### 2.2. Ujuzi wa awali

Neno ‘uhakiki’ au ‘uchambuzi’ si dhana mpya kwa wanafunzi wa kidato cha sita. Katika kidato cha nne na cha tano, wanafunzi waigusia nadharia ya uhakiki au uchambuzi wa kazi za fasihi simulizi kupitia mada kama ifuatavyo:

- Uhakiki wa hadithi simulizi katika Kiswahili (Kidato cha nne: Muhtasari, Fani na Maudhui)
- Uhakiki na Uwasilishaji katika Kiswahili (Kidato cha tano: Uhakiki wa fani na maudhui katika Kiswahili)

## 2.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake

### 2.3.1. Kidokezo cha mada

Katika mada ya iliyopita 'Ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi', ilionekena wazi kuwa kila kazi ya fasihi andishi hutengana na nyingine kulingana na sifa zake.Fikiria tena sifa muhimu za hadithi fupi, riwaya, tamthiliya na mashairi. Ili kuhakikisha kufaulu kwa msanii, ni mambo gani yanayostahili kuchunguzwa?

### 2.3.2. Maelekezo ya kidokezo cha mada

Kwa njia ya mbinu ya 'fikiri-jozi-changia', mwalimu awaelekeze wanafunzi kwenye matokeo ya mambo muhimu ya kuhakiki kazi ya fasihi ambayo ni fani, maudhuipamoja na mtindo wa lugha uliotumiwa.

## 2.5. Orodha ya masomo

| | **Kichwa cha somo** | **Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema)** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|
| **1** | Tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake | **Maarifa na ufahamu:** Kuonesha tanzu za fasihi simulizi ya Kiswahili na vipera vyake.<br><br>**Stadi:** Kutofautisha tanzu za fasihi simulizi na vipera vyake.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuheshimu maonyo kutoka tanzu za fasihi simulizi katika kuimarisha ustawi wa jamii. | 10 |
| **2** | Dhana ya hadithi simulizi | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza | 12 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | dhana ya hadithi simulizi<br><br>**Stadi**: Kutunga hadithi simulizi.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuthamini kazi ya utungaji wa hadithi simulizi kama njia ya kurekebisha mwenendo. | |
| **3** | Dhana ya methali za Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya methali za Kiswahili<br><br>**Stadi**: Kutumia methali za Kiswahili na kuzihusisha na maisha ya kila siku katika jamii.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujenga busara inayopatikana katika methali. | 12 |
| **4** | Dhana ya nahau na misemo ya Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya nahau na misemo katika Kiswahili<br><br>**Stadi :** Kutumia nahau na misemo ya Kiswahili katika vifungu vya habari mbalimbali<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuimarisha thamani ya lugha kwa kutumia nahau na misemo | 14 |
| **5** | Dhana ya vitendawili vya Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kutaja vitendawili mbalimbali vya kiswahili. | 6 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | **Stadi**: Kutega na kutegua vitendawili mbalimbali katika Kiswahili.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kukuza fikra na kutatua tatizo haraka. | |
| **6** | Dhana ya ushairi simulizi wa Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:**Kueleza dhana ya ushairi simulizi wa Kiswahili katika fasihi simulizi na taratibu za utungaji.<br><br>**Stadi:** Kughani na kutunga mashairi.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuendeleza kipaji cha utungaji wa mashairi. | 14 |
| **-** | Sarufi: Aina za sentensi za Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha aina za sentensi za Kiswahili<br>**Stadi:** Kutunga na kuchambua sentensi mbalimbali kwa kuzingatia aina zake.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kujenga tabia ya kufanya mambo kwa mpango au mwelekeo unaopendekezwa. | - |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Vipindi vyote vya mada ya kwanza** | | | 72 |

**Maelekezo kuhusu uandaaji wa masomo yaliyoonyeshwa hapo juu**

- **Vipengele vya muundo wa somo**

Kila somo hujengwa na vipengele vifuatavyo:

1. Kusoma na ufahamu vifungu vya habari
2. Msamiati kuhusu vifungu vya habari vilivyosomwa
3. Matumizi ya lugha
4. Kusikiliza na kuzungumza
5. Sarufi
6. Kuandika

- **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila kipengele cha somo**

**(a) Kusoma na ufahamu kifungu cha habari**

- **Kusoma:**Kwa kutegemea kitabu cha mwanafunzi au nakala ya vifungu vya habari, wanafunzi washirikishwe kwenye kazi ya kusoma kifungu husika kwa njia tofauti: kusoma kimya au kusoma kwa sauti. Mwalimu ashirikishe wanafunzi wote kwenye kazi hii kwa kutumia njia moja au nyingine. Ili kurahisisha kazi hii na kufaulu kuwashirikisha wanafunzi wote, kazi hii huweza kufanyika katika makundi madogomadogo au katika jozi.
- **Ufahamu:** Ufahamu wa kifungu cha habari huweza kufikiwa kwa njia nyingi kama vile kufasiri michoro au picha zilizotumiwa katika kifungu cha habari husika; kuuliza maswali ya ufahamu, kutoa dhamira kuu zilizosisitiziwa katika kifungu cha habari, kutoa muhtasari wa habari iliyozungumziwa, n.k. Kwa hiyo, inambidi mwalimu achagua njia moja au zaidi baadhi ya hizi au nyingine ambayo haikutajwa hapa juu.

### (b) Matumizi ya msamiati

Katika kipengele hiki, mwalimu anastahili kujenga kwa wanafunzi tafakuri tunduizi, yaani kuwaongoza wanafunzi kugunduwa wao wenyewe maana ya msamiati husika kwa kutegemea muktadha wa kifungu cha habari kwa ujumla. Si vizuri kupendekeza matumizi ya kamusi kama hatua ya kwanza ya kutoa maana ya msamiati. Kadhalika, maana ya msamiati huweza kupatikana kwa kutumia michoro au picha husika. Vifaa hivi huweza kuandaliwa na mwalimu lakini ni vizuri kuwashirikisha wanafunzi katika zoezi la kuchora michoro kulingana na maana ya msamiati husika. Pia, mbinu ya kutoa kinyume au kisawe cha msamiati husika huwa muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati.

### (c) Matumizi ya lugha

Ni wajibu wa mwalimu kuhusisha kifungu cha habari na maisha ya kila siku ya wanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima wanafunzi wapewe kazi zinazostahili kuamsha akili ili kutafuta njia ya utatuzi wa matatizo yanayoweza kuikumba jamii wanamoishi.

### (d) Kusikiliza na kuzungumza

- Kusikiliza: Wanafunzi wanaweza kukuza uwezo wa kusikiliza kwa njia tofauti: kusomewa kwa sauti kifungu cha habari, kusikiliza habari au hotuba zilizorekodiwa, kusikiliza hadithi au habari kwenye redio, televisheni au tarakilishi. Kwa hiyo, inambidi mwalimu kutumia njia hizi tofauti za kukuza stadi za kusikiliza kwa wanafunzi.
- Kuzungumza: Kuna njia nyingi za kukuza stadi za kuzungumza kwa wanafunzi. Baadhi ya hizi kuna midahalo na mijada, maigizo, uwasilishaji darasani, nyimbo, michezo, mazungumzo, masimulizi, mhadhara, n.k. Katika kazi zake za ujifunzaji, mwanafunzi ashirikishwe kikamilifu katika kazi mbalimbali kwa kuchanganya mbinu zilizotajwa hapo juu.

### (e) Sarufi

Sarufi inayotarajiwa katika uwezo mahsusi wa mada **haifundishwikamasomo la kujitegemea baada ya mada** bali hujitokeza mwishoni au kati kati ya kila somo. Kwa hiyo vipera vya sarufi hii hujigawa kulingana na idadi ya masomo yanayoiunda mada nzima.

### (f) Kuandika

Wakati wa kazi zinazofanyika katika makundi madogomadogo, wakati wa maelezo ya mwalimu, wakati wa uwasilishaji wa kazi darasani, wakati wa kutoa muhtasari wa somo na hasa wakati wa majaribio na mitihani au katika kuziandaa kazi za nyumbani, inambidi mwalimu awashirikishe na kuwahimiza wanafunzi kuandika. Pia, mwalimu asisahau imla kwa wanafunzi katika kazi zao za ujifunzaji.

## SOMO LA 1: DHANA YA UHAKIKI WA KAZI ZA FASIHI ANDISHI

### i) Malengo ya ujifunzaji

Kujadili dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi pamoja na mbinu za uhakiki.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za kazi za fasihi andishi zilizohakikiwa
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Vielelezo vya uhakiki wa kazi za fasihi andishi
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenyematatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Maswali ya ufahamu(Uk. 52)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasoma kifungu cha habari kuhusu tanzu za fasihi andishi na kutoa majibu sahihi kwa maswali husika. Majibu yanayopendekezwa ni haya yafuatayo:*

1. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kama malighafi yake makuu kwa lengo la kueleza maisha ya binadamu kwa njia ya usanii na ufundi unaoathiri na kusisimua msomaji na mtazamaji.
2. Fasihi simulizi na fasihi andishi
3. Hadithi za kubuni na hadithi za kihistoria.
4. Nyimbo, maghani, sifo na ngonjera.
5. Tanzu za fasihi andishi ni: a) Riwaya: hii ni hadithi ndefu iliyoandikwa kwa maandishi ya nathari, aghalabu inayoeleza ukweli fulani wa maisha. b) Tamthilia: ni utungo uliotungwa kwa lengo la kuigizwa jukwaani. c) Ushairi: ni utungo unaotumia maneno machache teule yaliyopangwa na kuwasilishwa kisanaa. d) Hadithi fupi: ni hadithi inayoshughulikia suala fulani kwa muhtasari.
6. Huandikwa kwa njia ya nathari, huwa ndefu, ina wahusika wengi na walioelezewa kwa kina, mandhari mapana na matumizi mengi ya lugha kutokana na maudhui yake mengi.
7. Fasihi huwazindua wanajamii kupigania haki zao, huhimiza uzalendo na uananchi kwa wanajamii, huhifadhi historia na utamaduni wa jamiihukosoa na kuwakanya wanajamii dhidi ya tabia zisizokubalika katika jamii, huburudisha na hukuza umoja na ushirikiano baina ya watu katika jamii.
8. Ni jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi.
9. Ni viumbe katika kazi ya fasihi wanaosema na kutenda matendo kwa niaba ya jamii husika.
10. Wao huzungumza kwa niaba ya mwandishi au jamii. Usimulizi huwahusu wao pamoja na tabia zao ili kudhihirisha mafunzo yanayolengwa na mtunzi wa fasihi husika.

**Msamiati kuhusu fasihi katika Kiswahili**

**Zoezi la 1 (uk.52)**

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, watafute msamiati mpya kutoka katika kifungu cha habari walichosoma hapo awali kisha waeleze maana zake na watunga sentensi sahihi kwa kutumia maneno hayo. Wazingatie muktadha wa kifungu hicho. Wanaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

**Zoezi la 2(uk. 53)**

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wachague jibu sahihi kutoka kwa yaliyo hapa chini kujazia nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi zinazofuata:uongozi mzuri, fasihi, fasihi andishi, kuhakiki, vina, mizani, wahusikaMajibu yanayopendekezwa:*

1. fasihi
2. fasihi andishi
3. kuhakiki
4. vina, mizani
5. Wahusika

**Matumizi ya lugha (Uk.53)**

*Tazama kazi zilizopendekezwa katika kazi za ziada za ufundishaji (2.5.2)*

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.54)**

*Zingatia kazi iliyotolewa katika kazi za ziada za ufundishaji (2.5.2)*

**Zoezi la 3 (Uk.54)**

*Zingatia kazi iliyotolewa katika kazi za ziada za ufundishaji (2.5.2)*

**Sarufi (uk.55)**

***Zoezi la makundi***

*Katika jozi, wanafunzi watambue kauli ya vitenzi vilivyopigiwa mstari na kuviweka baadaye katika kauli ya chunguza vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi zilizotolewa na kutambua kauli ya kutendea. Linganisha matokeo ya wanafunzi na haya yafuatayo.*

a) Vitenzi ‘pika, shona, chora, andika na soma vipo katika kauli ya kufanya au kutenda

b) Mama anampikia mtoto chakula.

c) Mimi ninamshonea dadangu nguo.

d) Mwanafunzi anamchorea babake picha.

e) Kaka anamwandikia mjomba wake barua.

f) Ngabo anamsomea mwalimu kitabu

**Zoezi la 5 (uk. 56)**

*Katika makundi ya wanafunzi,wachunguze mabadiliko katika vitenzi vilivyotolewa katika jedwali. Wajaze nafasi zilizoachwa wazi kwa jibu sahihi. Majibu ni haya yafuatayo:*

1. letea
2. soma
3. chezea

**Zoezi la 6 (uk. 56)**

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, wabadilishe vitenzi vilivyotolewa viwe katika kauli ya kufanyia/kutendea. Majibu ya zoezi hili ni:*

1. fumia
2. vutia
3. kimbilia

4. futia
5. pangusia

**Zoezi la 7 (uk. 57)**

*Kwa kazi binafsi, mwanafunzi abadilishe vitenzi husika katika kauli ya kutenda au hali ya kutendea. Majibu ya zoezi hili ni:*

1. Msichana anamchorea mtoto picha.
2. Gasimba anakimbilia shuleni.
3. Mama anamfumia Mutoni fulana.
4. Mimi ninamwandikia babangu barua.
5. Nitalifutia darasa letu ubao kesho

**Zoezi la 8**

*Katika jozi, wanafunzi waeleze maana ya sentensi iliyoathiriwa na vitenzi vilivyotumiwa. Linganisha matokeo ya wanafunzi na mapendekezo haya.*

a) Mama anachota maji kwa niaba ya baba.
b) Nitaupiga mpira badala yako.
c) Nyanya anaandaa chakula ili tukile.
d) Sitaandika barua kwa niaba yenu.
*e)* Ubao wa mwalimu unafutwa na kiranja *wa darasa*.

**SOMO LA 2: UHAKIKI WA HADITHI FUPI**

**i) Malengo ya ujifunzaji**

Kuhakiki hadithi fupi kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki husika.

**ii) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za hadithi fupi zilizohakikiwa
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Vielelezo vya vipengele vya uhakiki wa haditi fupi
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenyematatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu: Hadithi fupi kuhusu urithi wa mali**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome kifungu cha habari husika na kutoa majibu sahihi kwa maswali ya ufahamu. Majibu yanayopendekezwa ni haya yafuatayo:*

1. Sululu alitaka kupewa kasma yake ambayo ni kipande cha ardhi. Hakuwa na ucheshi kwa kuwa aliendа kwa babake ili kudai kasma yake kwa hasira nyingi.

2. Ndoa ya Sululu ilikuwa ya kuvumiliana. Sululu na mkewe waliishi kwa uchochole mwingi na hali hii haikumpa raha. Mkewe alikuwa mnyenyekevu kwake na walikuwa wamepitia mambo mengi (mazuri kwa mabaya) pamoja.

3. Nyumba hiyo ilikuwa imeezekwa kwa mabati ambayo yalikuwa yamepiga kutu. Kuta za nyumba hiyo zilikuwa zimejengwa kwa matofali yaliyoshikamanishwa na udongo.

4. Sululu ni mwenye hasira. Anaondoka kwake na kwenda kwa wazazi wake akiwa amebeba upanga. Anapofika huko, anazua fujo kwa kufoka akiitisha kipande cha ardhi na kutishia kumwua babake. Sululu pia ni mjinga kwa kuwa alikataa kusoma hata baada ya kupelekwa katika shule nzuri na kulipiwa karo. Baada ya kukataa kusoma, anarudi kwa wazazi wake na kuitisha urithi.

5. Kwa sababu aliacha masomo na akawa hana jambo muhimu la kufanya kutokana na umaskini uliomkumba.

6. Mwalimu atathmini ulinganisho wa wanafunzi kuhusu namna urithi wa ardhi umeshughulikwa na unavyofanywa katika jamii zao.

7. Toili Kauka, Ayubu Kauka na Matayo Kauka.

8. Mamake Sululu ni mvumilivu. Licha ya kuwa Sululu anamjia na upanga na matusi, yeye anatulia na kujaribu kuzungumza naye Sululu kwa upole bila kumkaripia. Yeye pia ni mwenye hekima. Mamake Sululu anajaribu kusema na mwanawe kwa kumkumbusha kuwa hata kipande cha ardhi ambacho amejenga nyumba yake ni urithi kutoka kwa babake. Anaendeleakwa kumfahamisha kuwa hawezi akapewa ekari kumi za ardhi ilhali kaka zake hawana urithi wao na hivyo ni bora wagawane wote. (Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi)

9. a) Utamaduni: maudhui haya yanadhihirishwa kutokana na dhana kuwa ni sharti mtoto wa kiume apewe urithi kutoka kwa wazazi wake. Sululu anadai urithi ambao anautaja kama kasma yake yaani haki yake. b) Elimu: elimu ni ngao ya maisha ya binadamu yeyote. Katika hadithi hii, babake Sululu anasoma na kuwa mwalimu. Ni kupitia kwa elimu aliyopata ndipo anaweza kuhifadhi pesa ambazo anazitumia kununua mashamba yake. Kaka zake Sululu pia wanatilia maanani elimu na wanafaulu katika maisha yao hadi hawaoni haja ya kupewa urithi. Sululu, kinyume na wenzake, anaamua kuachia masomo njiani na kujiingiza katika ulevi. Yeye haoni ubora wa elimu.

10. Mwandishi amekusudia kuwasihi wasomaji wa hadithi hiyo kuwa kuna ubora katika elimu. Mbali na hayo, mwandishi amekusudia kuwaonya watu wenye pupa kama ya Sululu kuzingatia upole na ustaarabu katika kila jambo wanalofanya.

**Matumizi ya msamiati**

**Zoezi la 1 (uk. 63)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi washirikiane kwa kutafuta msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi husika. Majibu yanayopendekezwa:*

1. ulitweta - ulihema kwa nguvu.
2. alimpapasa - alimgusagusa kwa njia ya kumbembeleza.
3. kaptura - vazi kama suruali lakini fupi na linaloishia magotini; bombo.
4. ucheshi - tabia ya kuwa mchangamfu na kuwafurahisha watu.
5. kero - jambo linaloudhi.
6. zinazipiku - zinazizidi.
7. hamaki - hasira.
8. kutu - kitu cha rangi nyekundu kinachoota juu ya chuma na kukiharibu kipatapo maji.
9. msonge - nyumba yenye umbo la duara na paa la umbo la pia.
10. aliachama - aliweka kinywa wazi kwa mshangao.

**Matumizi ya lugha:Aina mbalimbali za wahusika**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunziwajadilini:*
*1. Aina mbalimbali za wahusika katika fasihi andishi.*

Majibu:

1. Aina za wahusika

i) **Wahusika wakuu**: Hawa ni wahusika ambao wanahusishwa na takribani visa vyote katika kazi ya kifasihi. Wahusika hawa huhusishwa kutoka mwanzo hadi mwisho.

ii) **Wahusika wasaidizi** Hawa ni wahusika wanaosaidia kumjenga mhusika mkuu. Hujitokeza mara nyingi katika hadithi. Wahusika wasaidizi wanaweza kuwa na visa vyao. Kwa mfano: wanaweza wakawa ni marafiki na aila za wahusika wakuu.

iii) **Wahusika wadogo** Ni wahusika ambao wanafanya kazi ndogo sana katika fasihi kama vile kujenga maudhui au mandhari. Wahusika hawa wakitolewa, hadithi inaweza kuendela bila kubadilika sana.

iv) **Wahusika bapa** Hawa ni wahusika wasiobadilika kutoka mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano, mhusika mbaya anabakia kuwa mbaya kutoka mwanzo hadi mwisho. Sifa za wahusika bapa huweza kutambulika mwanzoni mwa hadithi. Wahusika bapa hawawakilishi sifa halisia za binadamu. Nia yao ni kujenga tabia moja tu. Kuna aina mbili za wahusika bapa:

- Wahusika bapa-sugu - huonyesha msimamo wao kulingana na masimulizi ya msanii.

- Wahusika bapa-vielelezo - msimamo wao hutambulika kulingana na majina yao. Msanii hutumia mbinu ya majazi au lakabu kuwapatia wahusika majina yanayolingana na sifa zao.

v) Wahusika duara Wahusika duara hubadilika kitabia katika fasihi. Hawana msimamo thabiti. Hubadilika kulingana na maudhui na mazingira. Kwa mfano, msichana aliyeanza kama mpole na mwadilifu anapobadilika na kuwa mtovu wa nidhamu, kahaba na asiyeshirikiana na mtu yeyote.

vi) Wahusika wafoili Hawa huwa katikati ya wahusika bapa na wahusika duara. Wanaweza kuchukua msimamo fulani katika masuala fulani lakini pia wanaweza kubadilisha msimamo huo wakati mwingine kulingana na hali. Wahusika hawa hutegemea wahusika duara na wahusika bapa ili kutoa sifa zao. Kwa mfano, wakiishi na mhusika bapa, wanaweza kuchukua msimamo wa mhusika huyo lakini wakikaa sana namhusika mwengine, wanabadilika. Wahusika hawa aghalabu huwakilisha uhalisi wa binadamu.

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi washirikishwe kwenye kazi ya uhakiki wa hadithi fupi 'Kasma Yangu' au* ***hadithi fupi nyingine iliyopendekezwa na mwalimu*** *kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki wa hadithi fupi vilivyoelezwa hapo juuu. Mwalimu awe huru katika*

*uchaguzi wa hadithi fupi ya kuhakikiwa; asije akawa mtumwa wa mfano wa hadithi fupi iliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi.*

Jibu lililopendekezwa:

a) **Sululu** ni mwenye hasira. Anaondoka kwake na kwenda kwa wazazi wake akiwa amebeba upanga. Anapofika huko, anazua fujo kwa kufoka akiitisha kipande cha ardhi na kutishia kumwua babake. Sululu pia ni mjinga kwa kuwa alikataa kusoma hata baada ya kupelekwa katika shule nzuri na kulipiwa karo. Baada ya kukataa kusoma, anarudi kwa wazazi wake na kuitisha urithi.

b) **Mamake Sululu** ni mvumilivu. Licha ya kuwa Sululu anamjia na upanga na matusi, yeye anatulia na kujaribu kuzungumza naye Sululu kwa upole bila kumkaripia. Yeye pia ni mwenye hekima. Mamake Sululu anajaribu kusema na mwanawe kwa kumkumbusha kuwa hata kipande cha ardhi ambacho amejenga nyumba yake ni urithi kutoka kwa babake. Anaendelea kwa kumfahamisha kuwa hawezi akapewa ekari kumi za ardhi ilhali kaka zake hawana urithi wao na hivyo ni bora wagawane wote.

c) **Mkewe Sululu** ni mnyenyekevu kwa mumewe. Yeye pia ni mvumilivu kwani wamepitia mambo mengi (mazuri kwa mabaya) katika ndoa yake na Sululu.

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.64)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili aina mbalimbali za wahusika pamoja na tabia na sifa zao kwa kusoma riwaya moja teule, kwa mfano riwaya ya 'Siku Njema' (iliyoandikwa na Ken Walibora). Kila kundi liwasilishe ufupisho wa majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

Mwelekeo wa jibu:

Mada 'Siku Njema' inaambatana kabisa na maudhui katika riwaya yenyewe kutokana na dhana kuwa kuna wahusika wengi akiwemo mhusika mkuu ambaye ni Kongowea Mswahili ambao walipitia changamoto nyingi maishani lakini hatimaye mambo yaliwanyookea hivyo siku zao njema ziliwadia. Maudhui kama vile ya umaskini, upweke na dhuluma kwa baadhi ya wahusika kama vile Kongowea Mswahili yanamalizika siku njema inapofika.

**Zoezi la 3 (Uk.64)**

*Katika jozi, wanafunzi wajadili uhusiano wa mada au kichwa cha riwaya ya SIKU NJEMA na maudhui yaliyoangaziwa katika riwaya hiyo.*

Jibu linalopendekezwa:

Mada 'Siku Njema' inaambatana kabisa na maudhui katika riwaya yenyewe kutokana na dhana kuwa kuna wahusika wengi akiwemo mhusika mkuu ambaye ni Kongowea Mswahili ambao walipitia changamoto nyingi maishani lakini hatimaye mambo yaliwanyookea hivyo siku zao njema ziliwadia. Maudhui kama vile ya umaskini, upweke na dhuluma kwa baadhi ya wahusika kama vile Kongowea Mswahili yanamalizika siku njema inapofika.

**Sarufi (Uk.55)**

***Zoezi la makundi***

*Katika jozi, wanafunzi watambue kauli ya vitenzi vilivyopigiwa mstari na kuviweka baadaye katika kauli ya chunguza vitenzi vilivyopigiwa mstari katika sentensi zilizotolewa na kutambua kauli ya kutendea. Linganisha matokeo ya wanafunzi na haya yafuatayo.*

a) Vitenzi 'pika, shona, chora, andika na soma vipo katika kauli ya kufanya au kutenda

b) Mama anampikia mtoto chakula.

c) Mimi ninamshonea dadangu nguo.

d) Mwanafunzi anamchorea babake picha.

e) Kaka anamwandikia mjomba wake barua.

f) Ngabo anamsomea mwalimu kitabu.

**Zoezi la 5 (uk. 66)**

*Kwa kazi binafsi, mwanafunzi abadilishe vitenzi husika katika kauli ya kutenda au hali ya kutendea. Majibu ya zoezi hili ni:*

1. letea
2. soma
3. chezea

**Zoezi la 6( uk. 66)**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wakamilishe jedwali walilopewa kwa kutumia vitenzi vilivyo katika kauli ya kufanya/kutenda au kufanyika/kutendeka.Majibu ya zoezi hili:*

1. fumia
2. vutia
3. kimbilia
4. futia
5. pangusi

**Zoezi la 7 (uk. 67)**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, watunge sentensi kumi sahihi katika kauli ya kufanyiwa/kutendewa na kauli ya kufanyika/kutendeka kwa kutumia vitenzi walivyopewa.Majibu ya zoezi hili ni:Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi*

*kisarufi na zihusishe vitenzi katika kauli ya kufanyiwa na kufanyika. Kwa mfano:*

1. a) Mama alisafishiwa vyombo na Neza.

b) Vyombo vilisafishika.

2. a) Maji yote yalinywewa na wageni wachache.

b) Maji yalinyweka.

3. a) Wagonjwa wote watatibiwa na daktari wa akiba.

b) Wagonjwa wote watatibika.

4. a) Mfalme ataendeshewa gari na dereva wake.

b) Gari litaendesheka.

5. a) Mpishi alionjewa mchuzi na dadake.

b) Mchuzi ulionjeka.

**SOMO LA 3: UHAKIKI WA MASHAIRI**

**i) Malengo ya ujifunzaji**

Kuhakiki mashairi kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki husika.

**ii) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za mashairi
- Mashairi yaliyorekodiwa
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenyematatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

### iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

### iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi

**Kusoma na ufahamu : Shairi kuhusu ukulima**

**Maswali ya ufahamu(Uk. 69)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasoma shairi husika na kutoa majibu sahihi kwa maswali yaliyotolewa. Majibu yanayopendekezwa ni haya yafuatayo:*

1. Mishororo ishirini
2. Vina vya kati ni ‘ka’ na ‘la’. Vina vya mwisho ni ‘ma’ na ‘nga’.
3. a) Jembe ndilo chanzo cha kipato kwa baba na mama. b) Jembe linashauriwa kuwa tayari kulima baada ya shamba kufyekwa.
4. Kifaa muhimu kwa wakulima kinachotumiwa katika kutayarisha mashamba kwa upanzi.
5. Jembe ndiwe mtawala, tangu enzi za wahenga. Kibwagizo kinamaanisha kuwa jembe limetumika tangu zamani.
6. a) Mbinu ya mazida - tunausema b) Mbinu ya inkisari - usende
7. Mizani 320 kwani kila mshororo ura mizani 16 na kila ubeti ukawa na mizani 64.
8. Mwalimu atathmini ikiwa maana zinazotolewa na wanafunzi ni sahihi. a) mtima – moyo b) kukongoka – kuzembea c) mrama – visivyo d) pasi – bila
9. Shairi linalisifu jembe pamoja na kulitia moyo wa kuzidi kufanya kazi. Mtunzi wa shairi analisihi jembe kutochoka katika utendakazi wake kwa wakati wowote ule. Pia, analiombea jembe maisha marefu na yasiyo na vikwazo. (Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi).

10. Ubeti wa kwanza ulisihi jembe limfariji mtunzi wa shairi hili ili naye aliweke liishi zaidi. Hii ni kwa sababu jembe ni kifaa muhimu ambacho kinaenziwa na watu wengi. Jembe ni chanzo cha kipato kwa watu wote na limekuwepo tangu zamani.

**Matumizi ya msamiati (Uk.70)**

***Zoezi la 1:****Katika jozi, wanafunzi watoe maana ya msamiati uliopigiwa mstari na kuutumia katika sentensi fupifupi. Majibu yanayopendekezwa ni yafuatayo.*

1. uzima - hali ya kuwa na afya njema; uhai.
2. taji - ubingwa anaopewa mtu au kitu baada ya ushindi.
3. dhima - wajibu.
4. mpaji - mwenye kutoa kitu kwa wengine; mwenye kuwapa wengine.
5. mtawala - mwenye madaraka ya juu kati ya watu.
6. tutafyeka - tutasafisha kwa kukata chaka na miti.
7. mtama - punje ndogondogo zitokazo mmea wa nafaka wenye bua refukama mhindi lenye kutoa masuke nchani.
8. masika - msimu wa mvua nyingi ambayo hunyesha mfululizo.
9. homa - joto kali la mwili linalosababishwa na maradhi mbalimbali.
10. mrama - kombokombo; visivyo

**Mifano ya sentensi**

1. Wagonjwa wote wanatamani uzima.
2. Baba alipewa taji la kuwa mkulima bora wa viazi vitamu.
3. Mashairi yana dhima ya kuburudisha.
4. Tunamwabudu Mungu kwa kuwa yeye ni mpaji wa vyote.

5. Mtawala wa mkoa wa Kati atatutembelea.
6. Tutafyeka uwanja wetu ili tulime na kupanda nyasi.
7. Mama anavuna mtama leo.
8. Mafuriko yamesababishwa na mvua ya masika.
9. Nimeugua homa kwa muda mrefu sana.
10. Mambo yalianza kwenda mrama alipoanza kunywa pombe.

**Matumizi ya lugha (Uk.71)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili: 1. Maudhui yaliyoangaziwa katika shairi walilosoma. 2. Dhamira ya mtunzi wa shairi walilosoma.*

Majibu yanayopendekezwa :

1. Shairi tulilosoma limeangazia maudhui ya maadili katika jamii. Kwa kufananishwa na jembe, binadamu wanafaa kuwa wenye bidii katika kazi zao kama lifanyavo jembe wakati wa ukulima.
2. Dhamira ya mtunzi wa shairi hili ni kuwahimiza binadamu kuwajibika katika kazi zao.

**Kusikiliza na kuzungumza**

**Zoezi la 2(Uk.71)**

*Katika makundi jozi, ghani darasani shairi 'Jembe'. Mwalimu ahakikishe kuwa mahadhi mbalimbali ya kughani mashairi yametumiwa.*

**Sarufi : Kauli ya kufanyisha/kutendesha**

**Zoezi la 3, (Uk. 72 )**

*Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge sentensi sahihi katika kauli ya kutendesha/kufanyisha. Mwalimu atathmini sentensi zilizotungwa na wanafunzi. Sharti ziwe sahihi na ziwe na vitenzi katika kauli ya kutendesha.*

Kwa mfano:

1. Mama anamlisha mtoto wali.
2. Mbwa alimkimbiza mgeni.
3. Nyanya atamkaribisha mjomba.
4. Njia hii itatufikisha mbali.
5. Yeye amemchezesha mgeni wa heshima.

**Zoezi la 4 (uk. 73)**

*Katika jozi, wanafunzi wachunguze mabadiliko ya vitenzi vilivyotolewa katika kauli ya kutenda na kauli ya kutendeana kisha wjaze nafasi zilizoachwa wazi kwa jibu sahihi.*

Kwa mfano :

1. ruka
2. andikiana
3. Pita
4. imbiana
5. samehea
6. tembeleana
7. itana
8. beba
9. pikiana
10. tembeza
11. laliana

**Zoezi la 5 (uk. 74)**

*Kwakazi binafsi, mwanafunzi atunge sentensi tano sahihi katika kauli ya kutendeana/kufanyiana. Inambidi mwalimu kuchunguza usahihi wa sentensi zilizotungwa na kuzitolea marekebisho au mapendekezo.*

**Zoezi la 6 (uk.74)**

*Katika jozi, wanafunzi watunge sentensi tano sahihi katika kauli ya kufanyisha/kutendesha kwa kutumia vitenzi vilivyotolewa. Inambidi mwalimu kuchunguza usahihi wa sentensi zilizotungwa na kuzitolea marekebisho au mapendekezo.*

Kwa mfano :

1. Kaka alipandisha mizigo garini.
2. Mimi nitamnywesha mtoto uji.
3. Mwalimu alimpigisha mwanafunzi magoti.
4. Mbwa wakali huniogofya.
5. Sara hatanionjesha peremende yake.

**SOMO LA 4: UHAKIKI WA TAMTHILIYA**

**i) Malengo ya ujifunzaji**

Kuhakiki tamthiliya kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki husika.

**ii) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za mashairi
- Tamthiliya zilizorekodiwa
- Tarakilishi
- Redio rekoda au simu mahiri
- Picha au michoro ya waigizaji wa tamthiliya na jukwaa
- Ubao, chaki
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenyematatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu:Sura moja ya tamthilia yenye mandhari mbalimbali**

**Maswali ya ufahamu(Uk. 78)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome dondoo kutoka tamthiliya 'Kijiba cha Moyo', Onyesho la 4&5 na kujibu maswali ya ufahamu yaliyopendekezwa. Mwalimu awaongoze wanafunzi kurejelea majibu haya.*

1. Nyumbani kwake Sele.

2. Sele anaonekana mwenye mawazo ila ni mtulivu. Anajipepea kwa kuwa kuna joto jingi.

3. Bi. Rahma alitaka kumjulia Sele hali.

4. Bi. Rahma alipata tetesi kuwa Sele ni mgonjwa.

5. Kwa sababu ya mawazo mengi baada ya kusimamishwa kazini.

6. Hospitalini

7. Ili damu ifanyiwe uchunguzi wa kutambua mgonjwa anaugua nini.

8. Jamila ni muuguzi wake Sele.

9. Kipimajoto

10. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Wanaweza kutoa hoja kama vile:

a) Afya: Hali ya kiafya ya Sele ndiyo imepelekea kuwepo kwa maonyesho haya mawili. Sele amedhoofika kiafya kutokana na kusimamishwa kazi. Anapelekwa hospitalini ili afanyiwe uchunguzi wa kiafya.

b) Kazi: Kama njia ya kujikimu kimaisha, ni sharti binadamu wafanye kazi. Sele pamoja na wenzake wanasimamishwa kazi kufuatia agizo lililotolewa. Hali hii ya kukosa kazi inampa Sele mawazo mengi ambayo yanaathiri hali yake ya afya na kumfanya apelekwe hospitalini.

**Matumizi ya msamiati**

**Zoezi la 1 (Uk. 79)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi zilizotolewa na tungapeke yao sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo. Haya ni majibu yaliyopendekezwa.*

1. kochini - kwenye kiti chenye sehemu ya kuwekea mikono na kilichowekwa mito katika sehemu ya kukalia na kuegemea.

2. mtulivu - mtu mpole asiyewasumbua na kuwakera wengine.

3. tetesi - uvumi; habari ambayo haijathibitishwa.
4. alikata tamaa - alitamauka.
5. aliachishwa kazi - alikoseshwa kazi au ujira.
6. kunguru - aina ya ndege anayetumiwa kama ishara ya woga; mtu mwoga.
7. akitafakari - akiwaza.
8. akijipepea - akijitikisia kipepeo ili kupata upepo.
9. uvundo - harufu mbaya.
10. nawathamini - nawaenzi.

**Mfano wa sentensi:**

1. Babu amelala kochini.
2. Paka wa bibi ni mtulivu sana.
3. Kuna tetesi kuwa watu walioathirika na ukame ni wengi sana.
4. Mwalimu alikata tamaa wanafunzi wake walipofeli mtihani wa kitaifa.
5. Mkurugenzi mkuu wa benki ameachishwa kazi na serikali.
6. Kunguru hawapatikani katika mbuga ya Akagera.
7. Mwanafunzi alibaki akitafakari jawabu la swali la Hisabati.
8. Mwigizaji alikuwa akijipepea mchezo ulipokamilika.
9. Matunda yaliyoharibika yameleta uvundo katika nyumba ya shangazi.
10. Mimi nawathamini wauguzi wote.

**Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu mandhari(uk. 79)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili mandhari mbalimbali ambako maonyesho ya tamthilia yoyote ile yanaweza kutendekea. Wanaweza kurejelea tamthilia zozote ambazo wamewahi kuzisoma. Kila kikundi kiwasilishe majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili mandhari mbalimbali ambako maonyesho ya tamthilia yoyote ile yanaweza kutendekea. Wanaweza kurejelea tamthilia zozote ambazo waliwahi kuzisoma. Kila kundi liwasilishe majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

*Mwalimua atathmini maelezo ya wanafunzi katika majadiliano yao. Wanafunzi wataje mandhari kama vile: nyumbani, sokoni, mahakamani, shuleni au kwenye kituo cha mabasi. Wanaweza pia kutaja muda kwa kuzingatia, saa na nyakati kama vile: jioni, asubuhi, mchana na usiku. Wanapoeleza mandhari, ni vyema maelezo hayo yaelekee kujenga taswira ya mandhari hayo akilini mwa msomaji. Wanaweza wakatoa maelezo ya vitu vilivyo katika maeneo hayo.*

**Kusikiliza na kuzungumza, (uk. 80)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadilimandhari mbalimbali, dhamira, wahusika pamoja na ujumbe vinavyojitokeza katika tamthiliakutoka Urunana. Kila kundi liwasilishe matokeo yao mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Maelekezo :**

*Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kuhusu matumizi ya mandhari mbalimbali katika tamthilia ya 'Urunana' au katika tamthilia yoyote ambayo mwalimu ataiteua kulingana na kupatikana kwake. Wanafunzi wataje mahali pa kutendeka kwa matukio mbalimbali pamoja na wakati wa kutendeka kwa matukio hayo. Haya yote ndiyo yanayounda mandhari katika kazi ya kifasihi.*

**Sarufi**: **Kauli ya kufanywa/kutendwa**

**Zoezi la 2 (Uk.80)**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, watunge sentensi sahihi katika kauli ya kutendwa/kufanywa.Yafuatayo ni majibu ya zoezi hili:*

1. Kazi ya ziada itafanywa na wanafunzi wote.
2. Gunia la viazi litabebwa na wavulana wanne.
3. Picha ya rais itachorwa na msanii huyu chipukizi.
4. Tamthilia itaigizwa na wanafunzi wa shule ya Amahoro.
5. Mila potovu zimepitwa na wakati.

**Zoezi la 3, (uk. 81)**

*Katika makundi ya wanafunzi watatu watatu, watunge sentensi tano sahihi katika kauli ya kufanywa/kutendwa kwa kutumia vitenzi vilivyotolewa:*

1. Mbegu za mihogo zitapandwa na nyanya.
2. Gari la askari lilipitwa na pikipiki yetu.
3. Mwalimu wetu aliombwa kusafiri na afisa wa elimu.
4. Kambi ya wakimbizi ilichomwa jana na waandamanaji.
5. Mbuzi anavutwa kwa kamba na mfugaji.

**Zoezi la 4, (uk. 82)**

*Katika makundi ya wanafunzi wawili wawili, wajaze nafasi zilizo wazi kwa kutumia kitenzi sahihi kutoka kwenye mabano katika hali ya kutendwa/ kufanywa. Yafuatayo ni majibu:*

1. Gari liliendeshwa vibaya na dereva yule.
2. Nyama ilikatwa vipande vidogovidogo.
3. Kwa nini sebule yenu imepangwa hivi?
4. Barua ya kuomba msamaha iliandikwa na mwanafunzi.
5. Mungu huombwa na binadamu wote.

## SOMO LA 5: UHAKIKI WA RIWAYA

### i) Malengo ya ujifunzaji

Kuhakiki riwaya kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki husika.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za riwaya zilizohakikiwa
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Vielelezo vya vipengele vya uhakiki wa riwaya
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenyematatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

### iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu: Sura moja ya riwaya yenye mbinu za lugha**

**Maswali ya ufahamu (Uk. 86 )**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome dondoo kutoka riwaya ‘Utengano’ na kujibu maswali ya ufahamu. Yafuatayo ni majibu yanayopendekezwa.*

1. Maimuna, Mama Jeni, Bi Farashuu na Dora.

2. Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi.

Kwa mfano:

a) Uhuru: Maimuna anatoroshwa kwao kwa sababu anataka uhuru. Anatamani kufanya atakavyo na ndiyo sababu yake ya kutoka kwao.

b) Uchumi: Katika eneo la Pumziko, tunaelezwa kuhusu majengo ya kibiashara yalivyojengwa na namna shughuli za biashara zinavyoendeshwa na Wahindi. Kuna biashara nyingi ambazo zinaendeshwa katika eneo hilo. Biashara hizi zinahusisha zile halali na zile zisizo halali.

3. Kutufahamisha na kutuelimisha kuhusu namna watu wanavyoishi katika jamii. Pia, amekusudia kutuonya na kututahadharisha dhidi ya matendo yasiyokubalika katika jamii.

4. Pandikizi la nyama - kumaanisha mtu mkubwa zaidi.

5. Majumba makubwa ya kisasa, vilabu, nyumba za siri, hoteli kubwa na mandhari yaliyojaa ghasia na zogo kila wakati.

6. Maisha ya Pumziko yalikuwa yenye ghasia, mbio, zogo na pupa wakati wote. Watu walikuwa mbioni mchana na usiku ili kujipatia kipato.

7. Majazi ni mbinu ya kuwapa wahusika na vitu katika kazi ya fasihi majina kwa kutegemea tabia, maumbile na hali zao. Pumziko ni jina la mahali katika riwaya hii. Mahali hapo pamepewa jina hilo kimakusudi kwa sababu ya watu kukimbilia sehemu hiyo ili kujipumzisha kutoka kwa pilkapilka za kila siku kama alivyofanya Maimuna. Toweni striti ni jina la kimajazi. Limetumika kuashiria kuwa kunatolewa shughuli za kibiashara katika eneo

hilo kwa namna ambavyo maduka yamepangwa na barabara katikati ambapo watu wanapishana wakitoa huduma zao.

8. Kwikwi za kilio

9. Alitaka kupata uhuru wa kufanya atakavyo/apendavyo.

10. Utohozi ni mbinu ya kifani ambayo mwandishi huswahilisha maneno ya lugha nyingine. Baadhi ya maneno yaliyotoholewa katika riwaya hii ni: striti kutokana na street, rafu kutokana na rough na teksi kutokana na taxi. Hayo ni maneno ya Kiingereza ambayo yametoholewa na kufanywa kuwa ya Kiswahili.

**Matumizi ya msamiati**

**Zoezi la 1 (Uk.87)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi zilizotolewa na tungapeke yao sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo. Haya ni majibu yaliyopendekezwa.*

1. alipohisi - alipofahamu/alipotambua kupitia milango ya fahamu kama vile: macho, ulimi, n.k.
2. alimnyatia - alimwendea polepole bila kutoa kelele.
3. alimkaripia - alimsemesha kwa ukali; alimgombeza.
4. kubiruliwa - kugeuzwa ndani nje.
5. tunasakwa - tunatafutwa.
6. zogo - hali ya ukosefu wa utulivu.
7. uliotutumka - uliovimba kwa unene.
8. wananong’ona - wanasemezana kwa sauti za chini.
9. ndewe -sehemu ya chini ya sikio iliyo duara.
10. teksi - gari linalotoa huduma za uchukuzi kwa kutoza kiasi fulani cha pesa.

**Mfano wa sentensi:**

1. Mama alipohisi kuwa ninamdanganya, aliondoka kwa hasira.
2. Paka alimnyatia panya na kumla.
3. Mwalimu alimkaripia mwanafunzi aliyevunja chaki yake.
4. Watu wengi huchukia kubiruliwa midomo.
5. Tulipoambiwa tunasakwa na makachero, tulishtuka.
6. Washambuliaji walizua zogo katika kambi ya wakimbizi.
7. Mtoto mwenye mwili uliotutumka amewasili.
8. Wanafunzi watundu wananong'ona bwenini mwao.
9. Nimeweka kipuli kwenye ndewe ya sikio la mtoto wangu.
10. Leo nitaabiri teksi kwenda nyumbani.

**Matumizi ya lugha (Uk.87)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili mbinu mbalimbali za lugha ambazo zimetumika katika sehemu ya riwaya ya 'Utengano' waliyoisoma hapo awali. Kwa kutoa mifano, waelezane: 1. Matumizi ya tanakali za sauti. 2. Matumizi ya semi. 3. Matumizi ya mbinu ya majazi. 4. Matumizi ya mbinu ya kuchanganya ndimi. 5. Matumizi ya mbinu ya uhaishaji.*

Mfano wa uhakiki wa mtindo wa lugha katika dondoo la 'Utengano'

- **Tanakali za sauti**: ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kurejelea sauti inayoigiza jinsi kitu fulani kinavyotendeka. Katika riwaya ya 'Utengano', mwandishi ametumia tanakali za sauti kama vile: alivuta **kwikwi** za kilio kuashiria sauti aliyoitoa Maimuna.

- **Semi:** ni mafungu ya maneno yanayotumiwa kuleta maana nyingine badala ya maana halisi ya maneno yaliyotumika.

Kuna fani mbili za semi: **nahau** - ni semi zenye kitenzi na **misemo** - ni semi zisizokuwa na vitenzi. Katika riwaya ya 'Utengano' kuna semi kama vile: pandikizi la nyama. Huu ni msemo

wa kuashiria ukubwa wa Mama Jeni. **Majazi** ni mbinu ya kuwapa wahusika au viumbe katika kazi ya fasihi majina kulingana na tabia, hulka au maumbile yao. *Pumziko* ni jina la mahali katika riwaya hii. Mahali hapo pamepewa jina hilo kimakusudi kwa sababu ya watu kukimbilia sehemu hiyo ili kujipumzisha kutoka kwa pilkapilka za kila siku kama alivyofanya Maimuna. *Toweni striti* ni jina la kimajazi. Limetumika kuashiria kuwa kunatolewa shughuli za kibiashara katika eneo hilo kwa namna ambavyo maduka yamepangwa na barabara katikati ambapo watu wanapishana wakitoa huduma zao. *Kuchanganya ndimi* ni mbinu itumikayo katika kazi za kifasihi ili kuwasilisha ujumbe kwa zaidi ya lugha moja. Katika riwaya ya ‘Utengano’, mwandishi.

Sura ya Pili ametumia maneno ya Kiingereza katika kazi yake. Kwa mfano: *darlin na drive ins*. **Uhaishaji** ni mbinu ya kuvipa viumbe visivyo na uhai sifa za viumbe hai. Kupitia mbinu hii, viumbe hivyo huweza kutenda, kusema na hata kuwaza kama wafanyavyo viumbe walio hai. Kwa mfano: mwandishi amesema kuwa ‘Maimuna alizamisha uso wake kwenye mto akaunywesha machozi’. Hapa, mto umepewa sifa za kibinadamu za kuwa na uwezo wa kunywa.

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.88)**

*Katika makundi madogomadogo, jadili matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha (fani) yanayojitokeza katika riwaya ya ‘Siku Njema’. Kila kundi liwasilishe muhtasari wa matokeo yao mbele ya wanafunzi wenzao. Inambidi mwalimu kushughulikia yeye mwenyewe uhakiki huu kabla ya kazi hii kutolewa kwa wanafunzi kwa madhumuni ya kuepuka upotovu mbele ya wanafunzi.*

Ifuatayo ni mojawapo ya mbinu zilizotumiwa katika riwaya ya ‘Siku Njema’.

1. Matumizi ya **methali**:

Hii ni kauli fupi ambayo hutumiwa katika jamii kutoa ukweli fulani wenye lengo la kuonya, kufundisha, kuhukumu n.k. Katika riwaya ya ‘Siku Njema’, methali zimetumika kwingi kwenye riwaya nzima, kama vile, ukurasa 2 (Dau la mnyonge haliendi joshi), ukurasa 18 (Ukweli una nguvu kuliko uongo), ukurasa 79 (Mui huwa mwema) miongoni mwa methali nyingine nyingi.

2. **Kinaya**: Hali ya kuonyesha kinyume cha matarajio ya msomaji. Kwa mfano, kutokana na riwaya ya 'Siku Njema', mamake Kongowea Mswahili alikuwa na sifa tele ila alikuwa maskini. Msomaji anatarajia Zainabu Makame awe tajiri kadri ya sifa alizokuwa nazo.

3. **Chuku**: Hii ni mbinu ya kutia maelezo chumvi zaidi ya yanavyofaa kuwa. Kwa mfano, katika ukurasa 15 tunapoambiwa kuwa 'mazishi ya Zainabu Makame yalikuwa yamejaa watu hata hapakuwa na nafasi ya kutema mate wala nzi kupita'.

Mbinu nyingine ambazo wanafunzi wanaweza kujadili ni: uhaishaji, matumizi ya maswali ya balagha, jazanda, taharuki, utohozi, kuchanganya ndimi, majazi, uzungumzi nafsia, matumizi ya tashbihi miongoni mwa nyingine.

**Sarufi (Uk.89 – 90)**

**Zoezi la 2 na la 3 yaambatanishwe**

*Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge sentensi zenye vitenzi vya hali ya kutendua au kufanyua kwa kutumia vitenzi hivi: kufunua, kubandua, kupangua. Hakikisha kuwa sentensi zilizotungwa na wanafunzi ni sahihi.*

**Mfano wa sentensi**

1. Mtoto alifunua chakula.

2. Mwalimu alibandua chati ukutani.

3. Nitapangua vikapu vya nyanya leo jioni.

**Zoezi la 4**

*Katika jozi, wanafunziwaeleze maana inayojitokeza katika sentensi hizi.*

*Mapendekezo ya majibu:*

a) Fundi anaachanisha nyuzi zilizotumika kufuma fulana ya mteja wake.

b) Neza anaharibu/ anavuruga kwa maksudi mpangilio wa viti sebuleni.

c) Nyanya aliyaweka wazi mafumbo yote.

d) Siwezi kuiondoa mizigo kwenye gari kwa kuwa ni mizito.

## 2.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 2.5.1. Maelezo ya Ziada kwa Mwanafunzi

☞ **Somo la 1 : Dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi**

**Matumizi ya lugha (Uk.53)**

**Dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi**

Uhakiki ni kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalum. Kwa kiwango cha elimu ya sekondari mhakiki hufanya kazi ya uhakiki ili kuonesha mambo yanayojitokeza kama vile, dhamira, migogoro, ujumbe, falsafa, mtazamo, msimamo n.k

Kwa hiyo, mhahiki kama mtaalamu wa kutathimini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalum, huwa na nafasi kubwa katika kazi za fasihi. Mhakaki ndiye anayefafanua kazi ya fasihi ili hadhira iweze kumwelewa vizuri mtunzi wa kazi hiyo. Kwa hiyo hapa mhakiki anasaidia kurahisisha mawasiliano kati ya hadhira na mtunzi. Vilevile mtunzi huwaonyesha watunzi ubora na udhaifu wa kazi zao. Kwa kufanya hivyo huwawezesha watunzi kufanya kazi bora zaidi.

**Dhima ya uhakiki wa kazi za fasihi**

- Husaidia wasomaji kuilewa kazi ya fasihi kwa urahisi:
- Watunzi wa kazi za fasihi hutofautiana katika matumizi ya lugha na taswira, hivyo mhakiki anapofanya kazi ya uhakiki anamsaidia msomaji kuelewa vipengele hivi kwa kuvifafanua kwa lugha rahisi.
- Husaidia ukuaji wa kazi za fasihi:

Mhakiki anapoonyesha ubora na udhaifu wa kazi ya mtunzi fulani, watunzi wengine pia watafunguka kifikra na kutunga kazi iliyobora zaidi.

- Hukuza uelewa wa mhakiki:

Kwa kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi, mhakiki hujiongezea maarifa ya lugha pamoja na mambo yanayotokea katika jamii.

Vilevile mtunzi huwaonyesha watunzi ubora na udhaifu wa kazi zao. Kwa kufanya hivyo huwawezesha watunzi kufanya kazi bora zaidi.

☞ **Somo la 2 : Uhakiki wa hadithi fupi**

**Matumizi ya lugha (Uk.64)**

**VIPERA VYA UHAKIKI WA HADITHI FUPI AU RIWAYA**

❖ **UHAKIKI WA FANI**

Unapohakiki fani katika hadithi fupi vipengele vifuatayo ni muhimu kuzingatiwa:

- Wahusika na tabia zao
- Muundo
- Lugha
- Mtindo
- Mandhari

A. **Wahusika:** ni watu au viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu katika kazi za fasihi.

**Aina za wahusika:** Wahusika wa hadithi fupi au riwaya hujigawa katika makundi makuu mawili:

- **Wahusika wakuu**: Mhusika mkuu ni mhusika mmoja au wawili ambao hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi fupi au riwaya.
- **Wahusika wadogo**: Ni aina ya wahusika muhimu sana ambao humsaidia mhusika mkuu kuipa hadithi au riwaya mwelekeo wa kisanaa na kimaudhui. Baadhi ya makundi haya mawili kunajitokeza aina mbalimbali za wahusika wafuatao:

- Wahusika bapa: Hawa ni wahusika wasiobadilika kutoka mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano, mhusika mbaya anabakia kuwa mbaya kutoka mwanzo hadi mwisho. Sifa za wahusika bapa huweza kutambulika mwanzoni mwa hadithi. Wahusika bapa hawawakilishi sifa halisia za binadamu. Nia yao ni kujenga tabia moja tu. Kuna aina mbili za wahusika bapa:
- Wahusika bapa-sugu - huonyesha msimamo wao kulingana na masimulizi ya msanii.
- Wahusika bapa-vielelezo - msimamo wao hutambulika kulingana na majina yao. Msanii hutumia mbinu ya majazi au lakabu kuwapatia wahusika majina yanayolingana na sifa zao.

- Wahusika duara - hubadilika kitabia katika fasihi. Hawana msimamo thabiti. Hubadilika kulingana na maudhui na mazingira. Kwa mfano, msichana aliyeanza kama mpole na mwadilifu anapobadilika na kuwa mtovu wa nidhamu, kahaba na asiyeshirikiana na mtu yeyote.
- Wahusika wafoili - huwa katikati ya wahusika bapa na wahusika duara. Wanaweza kuchukua msimamo fulani katika masuala fulani lakini pia wanaweza kubadilisha msimamo huo wakati mwingine kulingana na hali. Wahusika hawa hutegemea wahusika duara na wahusika bapa ili kutoa sifa zao. Kwa mfano, wakiishi na mhusika bapa, wanaweza kuchukua msimamo wa mhusika huyo lakini wakikaa sana namhusika mwengine, wanabadilika. Wahusika hawa aghalabu huwakilisha uhalisi wa binadamu.

**B. MUUNDO:** ni namna msanii anavyopanga visa vyake au fikra zake katika hadithi fupi, yaani mtiririko wa visa na matukio.Kinachozingatiwa hapa ni jinsi mwandishi alivyopanga kazi yake; mfano sura na sura, kisa na kisa au tukio na tukio.

**C. LUGHA:** ni kipengele cha lugha ni muhimu sana katika fasihi kwani ndicho hutenganisha fasihi na sanaa nyinginezo. Matumizi ya lugha katika fasihi yapo ya aina mbalimbali: kuna tamathaili za semi, misemo, nahau, methali, lahaja za wahusika, uchaguzi wa msamiati, miundo ya sentensi.

**Mifano ya tamathali za semi:**

- **Tanakali za Sauti:** Ni mbinu ya kutumia maneno yanayoiga sauti au hali fulani au namna kitendo kilivyofanyika.

Mfano: anguka pa!

- **Tashbiha**: Hii ni mbinu ya lugha inayolinganisha vitu au hali mbili tofauti kwa kutumia maneno ya kulinganisha; ‘kama’, ‘mithili ya’, ‘sawa na’.
- **Tashihisi:** Hii ni mbinu ya kupatia kitu kisicho hai sifa za kiumbe mwenye uhai (sifa za kibinadamu).
- **Takriri:** Ni mbinu ya kurudiarudia neno moja au kifungu cha maneno ili kusisitiza ujumbe fulani.
- **Ukinzani:** Ukinzani ni mbinu ya kusisitiza ujumbe kwa kuambatanisha maneno ya kinyume au yanayokinzana.

- **Sitiari:** Ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili moja kwa moja kwa kutumia kiungo ‘ni’ ama ‘kuwa’.
- **Taswira:** Ni matumizi ya lugha/maneno yanayojenga picha ya hali au jambo fulani kwa msomaji.
- **Taashira:** Ni matumizi ya lugha ya ishara kuwakilisha ujumbe fulani. Jina au kitu fulani kinatumika kumaanisha kitu kingine chenye uhusiano na kile kilichotumiwa.
- **Jazanda:** Ni kulinganisha vitu viwili moja kwa moja bila kutumia viunganishi.
- **Majazi:** Majazi ni pale tabia za wahusika zinapoambatana na majina yao halisi.
- **Lakabu:** Ni mbinu ya mhusika kupewa/kubandikwa jina na wahusika wengine ama yeye mwenyewe kujibandika jina linalooana na tabia/sifa zake.
- **Chuku:** Ni kutumia maneno yaliyotiliwa chumvi ili kusisitiza ujumbe fulani au kusifia kitu, kutilia chumvi.

**D. MTINDO:** Mtindo ni namna ambavyo mwandishi huipa hadithi yake sura ya kifani na kimaudhui. Mtindo ndio unaotofautisha wasanii. Katika mtindo tunachunguza sana matumizi ya lugha.

**E. MANDHARI :** Mandhari ni mazingira au mahali tukio la hadithi fupi lilipotokea. Kuna mandhari ya kubuni na mandhari ya kweli.

## ❖ UHAKIKI WA MAUDHUI

**Maudhui** ni jumla ya mawazo yote yanayozungumzwa katika kazi ya fasihi. Hujumuisha mawazo pamoja na mafunzo mbalimbali yaliyomsukuma msanii hadi akatunga na kusainii kazi fulani ya kifasihi. Mawazo na mafunzo haya hayazuki hivihivi tu. Kwa hiyo wakati wa kuyachambua na kuyajadili ni lazima yahusishwe na hali halisi ya kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi zilizopo katika jamii, hali hizi ndizo zilimzaa, zilimlea na kumkuza msanii.

Wakati wa kuchambua kazi za kifasihi mhakiki ni lazima ajiulize amaswali yafuatayo:

- Je, msanii anatueleza nini?
- Je, msanii kamtungia mtu wa tabaka gani?
- Anamtukuza nani?
- Anambeza nani?

- Msanii anataka tuchukue ahatua gani katika utatuzi wa matatizo ayashugulikiayo katika kazi yake?

Maudhui hujengwa na vipengele muhimu vifuatavyo: **Dhamira, ujumbe, migogoro, msimamo wa msanii pamoja na falsafa yake.**

a) **Dhamira:** ni lengo au mawazo makuu yanayojitokeza sana katika kazi ya fasihi. Ni jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo, na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake.

   Kifasihi kuna aina mbili za dhamira yaani dhamira kuu na dhamira ndogondogo

- **Dhamira kuu** ni kiini cha kazi ya fasihi, ni wazo kuu, ni jambo linalomsukuma msanii kuandika kazi yake ili aweze kuufikisha ujumbe wake kwa hadhira.
- **Dhamira ndogondogo** ni mawazo madogomadogo ambayo hujenga dhamira kuu.

b) **Migogoro:** ni hali ya kutokuelewana baina ya pande mbili yaani mtu na mtu, mtu na kikundi au mtu mwenyewe na nafsi yake. Migogoro ni mivutano na misuguano mbalimbali katika kazi za fasihi. Migogoro inaweza kuwa kati ya wahusika, familia zao au matabaka yao**.** Migogoro hii inaweza kuwa ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni, kifalsafa, nk.

c) **Ujumbe:** ni funzo na maadili yaliyokusudiwa na mtunzi yaifikie jamii aliyoilenga kufikisha kazi yake ya fasihi.

d) **Falsafa:** ni imani na mwelekeo wa mwandishi kuhusu maisha katika jamii.

e) **Msimamo wa msanii:** Msimamo wa msanii kuhusu maswala mbalilmbaili ya kijamii hubainishwa na mawazo, mafunzo, lengo na falsafa. Msimamo ndio uwezao kuwatofautisha wasanii wawili au zaidi wanaotunga kazi za fasihi zilizo na kiini na chimbuko moja. Kwa hiyo, msanii huweza kuchukuwa msimamo wa kimapinduzi au wa kiyakinifu kulingana na jinsi anavyoyazingatia maisha ya jamii inayozungumziwa.

☞ **Somo la 3 : Uhakiki wa mashairi**

**Matumizi ya lugha (Uk.71)**

**VIPERA VYA UHAKIKI WA SHAIRI**

Uhakiki wa mashairi huzingatia fani na maudhui.

**a) Fani**

Uhakiki wa fani ya shairi huzingatia muundo wake, yaani jinsi shairi lilivyoundwa kwa kuangazia mizani, vina, mishororo n.k Aidha, ni muhimu kutaja aina na bahari za shairi zinazohusiana na kila sifa uliyoitaja.

- Idadi ya mishororo katika kila ubeti - Tumia idadi ya mishororo kubainisha aina ya shairi hilo.

Kwa mfano: Shairi lina mishororo minne katika kila ubeti, kwa hivyo ni Tarbia

- Idadi ya mizani katika kila mshororo na katika kila kipande cha mshororo.

Kwa mfano: Kila mshororo una mizani kumi na sita: nane katika utao na nane katika ukwapi.

- Idadi ya vipande katika kila mshororo - Taja ikiwa shairi lina kipande kimoja, viwili, vitatu au vinne kisha utaje bahari yake.
- Kituo, kiishio au kibwagizo - Ikiwa mstari wa mwisho umerudiwa rudiwa, basi shairi lina kibwagizo au kiitikio, la sivyo lina kiishio.
- Vina - Zingatia vina vya kati na vya mwisho kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Kisha utaje ikiwa ni Mtiririko, Ukara au Ukaraguni
- Matumizi ya lugha: Mtindo wa lugha hurejelea namna mbalimbali ambazo mshairi anatumia mbinu za lugha. Mshairi anaweza kutumia mbinu za lugha. kama vile: Tanakali za Sauti, Tamathali za semi n.k.

Katika mtindo lugha mhakiki huchunguza uhuru wa msanii, yaani mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika utunzi wa shairi. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lizingatie umbo fulani. Zifuatazo ni njia mbalimbali ambazo mtunzi wa shairi anaweza kutumia kuonyesha uhuru wake.

**b) Maudhui**

Uhakiki wa maudhui ya shairi huzingatia vipengele vikuu ambavyo ni Dhamira (Dhamira kuu na dhamira ndogondogo) pamoja na Ujumbe.

☞ **Somo la 4 : Uhakiki wa Tamthiliya**

**Matumizi ya lugha (Uk.79)**

**VIPERA VYA UHAKIKI WA TAMTHILIYA**

Tamthilia au mchezo wa kuigiza huweza kuhakikiwa jukwaani au kupitia maandishi. Mambo muhimu yanayoongoza uhakiki huu ni yafuatayo.

**i) Uhakiki wa fani**

- **Wahusika**: Wahusika katika tamthilia huwa wengi pamoja na tabia zao mbalimbali.Tamthilia huwa na wahusika halisi ambao wanajitetea jukwaani kimatendo na kitabia wakati.
- **Muundo**: Tamthilia huwa na sehemu tatu : Mwanzo, Katikati na Mwisho. Sehemu zake zinatazamiwa kuingiliana, kujengana na kukamilishana.
- **Mtindo**: Tamthilia huwa na mgawiko wazi wa matendo na matukio kwa mujibu wa sehemu na sura mbalimbali. Majina ya wahusika huandikwa katika upande wa kushoto, kisha koloni, halafu hufuatiwa na maneno halisi yaliyotamkwa na mhusika huyo.
- **Lugha**: Tamthilia inatawaliwa na lugha ya mazungumzo katika majibizano au hata mazungumzo pweke. Ucheshi, porojo au mizaha, tamathali za usemi na onomatopia hutumiwa sana
- **Mandhari**: Wakati, hali au mahali ambapo tukio linaelezewa kutokea katika fasihi huitwa mandhari. Mandhari yanaweza kuwa ya kihalisia (ya kweli) kama vile: njiani, sokoni, hospitalini, nyumbani, shambani, barabarani n.k. Mandhari pia yanaweza kuwa ya kidhahania (ya kufikiria tu) kama vile: mbinguni, hewani, angani, kuzimuni, kwenye jua n.k. Mandhari katika tamthiliya huitwa jukwaa.

**ii) Uhakiki wa maudhui**

Dhamira, ujumbe, migogoro, msimamo wa msanii pamoja na falsafa yakehushughulikiwa.

### 2.5.2. Maelekezo kwa Mwalimu

**Matumizi ya lugha (Uk.53)**

1. *Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi. Katika uwasilishaji wao, wanafunzi wayagusie majibu yafuatayo:*

Uhakiki ni kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalum. Kwa kiwango cha elimu ya sekondari mhakiki hufanya kazi ya uhakiki ili kuonesha mambo yanayojitokeza kama vile, dhamira, migogoro, ujumbe, falsafa, mtazamo, msimamo n.k

Kwa hiyo, mhahiki kama mtaalamu wa kutathimini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalum, huwa na nafasi kubwa katika kazi za fasihi. Mhakaki ndiye anayefafanua kazi ya fasihi ili hadhira iweze kumwelewa vizuri mtunzi wa kazi hiyo. Kwa hiyo hapa mhakiki anasaidia kurahisisha mawasiliano kati ya hadhira na mtunzi. Vilevile mtunzi huwaonyesha watunzi ubora na udhaifu wa kazi zao. Kwa kufanya hivyo huwawezesha watunzi kufanya kazi bora zaidi.

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.54)**

*Kwa kutumia redio rekoda, simujanja au uso bapa wa televisheni au kompyuta, washirikishe wanafunzi kwenye kazi ya kusikiliza maelezo kuhusu dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi(k.m. rekodi ya kifungu cha habari uk.50). Baadaye, kila mwanafunzi atoe muhtasari wa yaliyozungumziwa. Mambo ya kuzingatia katika kazi hii:*

1. *Maana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi*
2. *Dhima ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi*

**Matumizi ya lugha (Uk.64)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili vipera vya uhakiki wa hadithi fupi. Katika uwasilishaji wao, wanafunzi wayagusie majibu yafuatayo:*

Vipengele vya FANI

- Wahusika na tabia zao

- Muundo
- Lugha
- Mtindo
- Mandhari

Vipengele vya MAUDHUI

- Dhamira
- Migogoro
- Falsafa
- Ujumbe
- Msimamo wa msanii

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.64)**

*Kwa kutumia redio rekoda, simu janja au uso bapa wa televisheni au kompyuta, wanafunzi washirikishwe kwenye kazi ya kusikiliza maelezo kuhusu dhana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi. Baadaye, kila mwanafunzi atoe muhtasari wa yaliyozungumziwa. Mambo ya kuzingatia katika kazi hii:*

- *Maana ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi*
- *Dhima ya uhakiki wa kazi za fasihi andishi*

**Zoezi la makundi (Uk.64)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili dhima ya uhakiki wa kazi za kifasihi. Waongoze wanafunzi kuyagusia maoni yafuatayo:*

- Husaidia wasomaji kuilewa kazi ya fasihi kwa urahisi:
- Watunzi wa kazi za fasihi hutofautiana katika matumizi ya lugha na taswira, hivyo mhakiki anapofanya kazi ya uhakiki anamsaidia msomaji kuelewa vipengele hivi kwa kuvifafanua kwa lugha rahisi.
- Husaidia ukuaji wa kazi za fasihi:

Mhakiki anapoonyesha ubora na udhaifu wa kazi ya mtunzi fulani, watunzi wengine pia watafunguka kifikra na kutunga kazi iliyobora zaidi.

- Hukuza uelewa wa mhakiki:

Kwa kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi, mhakiki hujiongezea maarifa ya lugha pamoja na mambo yanayotokea katika jamii.

Vilevile mtunzi huwaonyesha watunzi ubora na udhaifu wa kazi zao. Kwa kufanya hivyo huwawezesha watunzi kufanya kazi bora zaidi.

**Kuandika: Kipengele hiki cha somo la 'Uhakiki wa hadithi fupi' kiongezwe.**

*Kwa kazi binafsi, mwalimu awachagulia hadithi fupi kisha wafanye uhakiki wa hadithi fupi hiyo kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki husika. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameshirikishwa katika kazi ile ya uhakiki.*

**Matumizi ya lugha (Uk.71)**

*1. Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili vipengele vinavyozingatiwa katika uhakiki wa shairi.*

**Mwelekeo wa jibu**

Uhakiki wa mashairi huzingatia fani na maudhui.

**a) Fani**

Uhakiki wa fani ya shairi huzingatia muundo wake, yaani jinsi shairi lilivyoundwa kwa kuangazia mizani, vina, mishororo n.k. Aidha, ni muhimu kutaja aina na bahari za shairi zinazohusiana na kila sifa uliyoitaja.

- Idadi ya mishororo katika kila ubeti - Tumia idadi ya mishororo kubainisha aina ya shairi hilo.

Kwa mfano: Shairi lina mishororo minne katika kila ubeti, kwa hivyo ni Tarbia

- Idadi ya mizani katika kila mshororo na katika kila kipande cha mshororo.

Kwa mfano: Kila mshororo una mizani kumi na sita: nane katika utao na nane katika ukwapi.

- Idadi ya vipande katika kila mshororo - Taja ikiwa shairi lina kipande kimoja, viwili, vitatu au vinne kisha utaje bahari yake.

- Kituo, kiishio au kibwagizo - Ikiwa mstari wa mwisho umerudiwarudiwa, basi shairi lina kibwagizo au kiitikio, la sivyo lina kiishio.

- Vina - Zingatia vina vya kati na vya mwisho kutoka ubeti mmoja hadi mwingine. Kisha utaje ikiwa ni Mtiririko, Ukara au Ukaraguni

- Matumizi ya lugha: Mtindo wa lugha hurejelea namna mbalimbali ambazo mshairi anatumia mbinu za lugha. Mshairi anaweza kutumia mbinu za lugha. kama vile: Tanakali za Sauti, Tamathali za semi n.k.

Katika mtindo lugha mhakiki huchunguza uhuru wa msanii, yaani mshairi hafungwi na kanuni za kisarufi za lugha katika utunzi wa shairi. Anaweza kufanya makosa ya kisarufi kimakusudi ili shairi lizingatie umbo fulani.

**b) Maudhui**

Uhakiki wa maudhui ya shairi huzingatia vipengele vikuu ambavyo ni Dhamira (Dhamira kuu na dhamira ndogondogo) pamoja na Ujumbe.

*2. Katika makundi madogomadogo, wanafunzi washirikishwe kwenye uhakiki wa shairi 'Jembe' kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki wa shairi (fani na maudhui).* ***Inambidi mwalimu kufanya yeye mwenyewe uhakiki wa shairi husika ili kuwaongoza iwezekanavyo wanafunzi katika uhakiki wao na kulinganisha matokeo yao na yake.***

**Kuandika: Kipengele hiki cha somo la 'Uhakiki wa shairi' kiongezwe.**

*Kwa kazi binafsi, mwalimu awachagulia shairi kisha wafanye uhakiki wa shairi hilo kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki husika. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameshirikishwa katika kazi ile ya uhakiki.*

**Matumizi ya lugha (Uk.79)**

*1. Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili vipengele muhimu vinavyotarajiwa kuzingatiwa katika uhakiki wa tamthiliya.*

Tamthilia au mchezo wa kuigiza huweza kuhakikiwa jukwaani au kupitia maandishi. Mambo muhimu yanayoongoza uhakiki huu ni yafuatayo.

**a) Uhakiki wa fani**

- **Wahusika**: Wahusika katika tamthilia huwa wengi pamoja na tabia zao mbalimbali.Tamthilia huwa na wahusika halisi ambao wanajitetea jukwaani kimatendo na kitabia wakati.
- **Muundo**: Tamthilia huwa na sehemu tatu : Mwanzo, Katikati na Mwisho. Sehemu zake zinatazamiwa kuingiliana, kujengana na kukamilishana.
- **Mtindo**: Tamthilia huwa na mgawiko wazi wa matendo na matukio kwa mujibu wa sehemu na sura mbalimbali. Majina ya wahusika huandikwa katika upande wa kushoto, kisha koloni, halafu hufuatiwa na maneno halisi yaliyotamkwa na mhusika huyo.
- **Lugha**: Tamthilia inatawaliwa na lugha ya mazungumzo katika majibizano au hata mazungumzo pweke. Ucheshi, porojo au mizaha, tamathali za usemi na onomatopia hutumiwa sana
- **Mandhari**: Wakati, hali au mahali ambapo tukio linaelezewa kutokea katika fasihi huitwa mandhari. Mandhari yanaweza kuwa ya kihalisia (ya kweli) kama vile: njiani, sokoni, hospitalini, nyumbani, shambani, barabarani n.k. Mandhari pia yanaweza kuwa ya kidhahania (ya kufikiria tu) kama vile: mbinguni, hewani, angani, kuzimuni, kwenye jua n.k. Mandhari katika tamthiliya huitwa jukwaa.

**b) Uhakiki wa maudhui**

Dhamira, ujumbe, migogoro, msimamo wa msanii pamoja na falsafa yakehushughulikiwa.

*2. Katika makundi madogomadogo, wanafunzi washirikishwe kwenye uhakiki wa tamthiliya 'Kijiba cha Moyo' kwa kuongozwa na vipengele muhimu vya uhakiki wa tamthiliya.* ***Mwalimu anastahili kutayarisha uhakiki wake mwenyewe bila kutegemea tu matokeo ya wanafunzi.***

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.80)**

*Mwalimu achague tamthiliya moja iliyorekodiwa na kuwaomba wanafunzi wasikilize. Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atoe muhtasari wa aliyoyasikiliza, wahusika pamoja na ujumbe unaolengwa katika tamthiliya hiyo.*

**Kuandika: Kipengele hiki cha somo la 'Uhakiki wa tamthiliya' kiongezwe.**

*Kwa kazi binafsi, mwalimu awachagulietamthiliya kisha wafanye uhakiki wa tamthiliya hiyo kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki husika. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameshirikishwa katika kazi ile ya uhakiki.*

**Uhakiki wa riwaya (Uk.87): Habari muhimu kwa mwalimu kuhusu riwaya 'Utengano' ya *Said A. Mohamed***

**(a) Muhtasari wa riwaya**

Jamaa ya Maksuudi inawakilisha migogoro katika jamii baada ya kutimuliwa kwa utawala wa kikoloni. Maksuudi ni Shekhe na Bi Tamima ni mkewe, Mussa ni mwanao wa kiume na Maimuna mwanao wa kike.

Bwana Maksuudi anamwendea kinyume mkewe kwa kushiriki mapenzi na wanawake wengine. Kitendo hiki kinampcleka pale kwa Kazija ambapo anamfumania mwanave Mussa. Bi Tamima na Maimuna bintiye hawaruhusiwi na Bwana Maksuudi kutoka nyumbani jambo ambalo Maimuna analichukia.

Biti Kocho amejitolea kupinga vi'endo vyake Mr-ksuudi. Biti Kocho anampinga Maksuudi pale anapompiga Bi Tamima akiwa kwenye maumivu baada ya uzazi. Biti Kocho anapinga pia kitendo cha Bwana Maksuudi kutowaruhusu Bi Tamima na Maimuna kutoka nje kama wanawake wengine.

Biti Kocho na Farashuu wanapanga njama na kumtorosha Maimuna kutoka kwao. Pia Bi Tamima naye anahama kwake baada ya kudhulumiwa kwa kupigwa na Bwana Maksuudi. Kutoroka kwa Maimuna akiutafuta uhuru kunampeleka kuingilia maisha ya ukahaba.

Kazija, anauchochea urama dhidi ya Maksuudi katika uwanja wa uhuru kitendo ambacho hatimaye kinapelekea kukamatwa na kufungwa kwa Maksuudi kifungo cha miaka miwili gerezani. Kazija anaugeuza mtazamo wa wananchi kisiasa na kuelekeza mkondo wa uchaguzi kwa kuangazi maovu ya wagombeaji kura kama vile Maksuudi na Zenga.

Mwisho Maimuna amesawiriwa akiacha maisha ya ukahaba na kuolewa na Kabi kijana ambaye ni mwanaye Maksuudi na Bi Mwanasururu aliyetalikiana naye na mwishowe akafa.

**(b) Wahusika wakuu na tabia zao**

**- Maksuudi:**Kwa upande wa familia, Makusudi ni kiongozi asiyehishimu madaraka yake; ni mwingi wa hadaa na udanganyifu. Makusudi alikuwa mtu dhalumu, afiriti na mwingi wa maovu.

Makusudi anajielewa kuwa afanyayo siyo na ni kinyume na maadili ya jamii. Anajali sana nafsi yake, Anajali ile nafsi ya ujitajirisha mwenyewe. Imani ya Makusudi juu ya wanawake ni jambo litishalo. Kwake mwanamke si kitu. Imani hii ndio iliyomfanya kumtesa Mwanasururu. Kwa upande wa uongozi, Maksuudi alikuwa mmoja wa waanzilishi wa chama cha Mwafrika kilichodai uhuru wa Mwafrika na kumuondoa mkoloni. Alikuwa kiongozi shupavu mwenye nia thabiti. Alipigania uhuru wananchi yake nia moja. Licha ya yote hayo makusudi alikuwa mwalimu wa dini. Uhuru ulipopatikana Makusudi alipewa madaraka kama mkuu wa wilaya. Baada ya kuyapata madaraka aliisaliti ile nia thabiti ya kutetea wananchi. Aakapata nafasi ya kunyanganya wananchi. Katika wale wengi aliowadhulumu, kuwahini na kuwafanya watumwa walikuwa wanawake. Matendo yake maovu yalimpeleka jela.

**Maimuna:** ni mwanamke mtawa. Anatawishwa na kuekwa ndani na baba yake Bwana Makusudi. Kutawishwa huku kunamnyima haki na uhuru Maimuna. Maimuna ni muhusika anayeonewa na anaefungiwa ndani kutumika kiutumwa. Kufungiwa huku kunamfanya Maimuna kuwa mtoro. Utoro wake una nia njema, yaani anataka kujinyakulia uhuru wake, apate kuishi akiwa uuru na awe na hadhi ya kiutu. Maimuna ni mtiifu kwa sababu yenyewe ni kwamba muda mrefu wa utawa, Maimuna yu radhi kusononeka na kuumia badala ya kuivunja miko ya baba yake. Maimuna si mjinga; anaufahamu udhalimu wa baba yake. Maonevu wayapatayo wanawake na mnyanyaso wa wanaume dhidi ya wanawake. Maimuna katika utumwa wake hakupata kutoka nje pasi na ruhusa ya baba yake na kufungiwa huku kulimwathiri sana Maimuna na kumfanya boza. Mara nyingi alilia na kuona kama ametengwa na jamii. Maimuna aliamua kujitafutia uhuru wake na akaamua kutoka nje na kuangukia kwenye balaa la zinaa. Haya yalimfanya kila siku kujikinga na hujuma za wanaume waovu. Maimuna hakuzoea fujo wala zogo. Shida alizopata Maimuna zilimfanya awe jasiri na kumwerevusha na mambo ya dunia.

**Kazija:** Ni muhusikamwenye chuki na kisasi kwa wanaume. Kazija anafahamu kwamba mwanamkedaima yumo katika utumwa wa kulazimishwa. Utumwa ambao umemdhalilisha mwanamke na kumwacha kiumbe dhaifu kisichokua na Maisha. Kazija nimwanamke aliyepevuka kikweli katika kuidai haki yake pamoja na maslahi yawanawake. Hana kificho katika kuwaambia wanaume udhalimu wao. Kazija nimuhusika wa kike wa kwanza anaetambua kuwa mwanamke anayenyimwa uhuru iliawe rahisi kutawaliwa. Kazija alijifunza kupigania na kudai haki yake kwaujasiri. Kazija ni mtambuzi wa udanganyifu, kiburi na unafiki wa viongozi.

Kazija si mjinga hapo alipo na baada ya kuutambua unafiki wa viongozi anujua wajibu wakekatika kuutilia kikomo unafiki huo. Anaudhihirisha unafiki wa Makusudi na Zanga. Huyu ni mwanamke anayefahamu nafasi yake katika jumuia yake.Kupitia muhusika huyu mwandishi anatwambia si wanawake wote wasiotambuawajibu wao wanawake kama Kazija ndio wanaotegemewa katika vita vya ukomboziwa wanawake. Labda pia mwandishi anasema wanawake kama hawa ni nadra sanakupatikana. Jambo linalomtambulisha Kazija niule ujasiri wake katika kukataamadhila na kuikabili dunia kama mtu akitakacho.

**Farashuu:** ni mkunga wa kienyeji anayeishi katika mtaa wa Madongo Mporomokomtaa wa wanapoishi wachochole na makabwela. Farashuu ni myonge anayetokanana tabaka la chini. Anaishi kwa kuuza vitumbua na wakati mwingine huitwa kwakufanya ukunga. Zamani alikuwa mkwewe Bwana Makusudi ambaye alimtesabintiye Farashuu-Mwanasururu na kusababisha kifo chake. Kifo cha Mwanasururukilichochea kisasi moyoni mwa Farashuu tunamuona ni mwanamke mwenye kisasikwa Makusudi. Ni mwanamke mpole na mtulivu mwenye kisasi kwa yeyoteamtendaye maovu.Hataki kufanya kazi yeyote ya ujeuri; jambo ambalo limekuza imani fulani katikamawazo yake kwamba. Labda umuhimu mkubwa wa Farashuu katikariwaya hii mbali na kuwakilisha wanyonge. Yeye ndie chanzo cha utengano wafamilia ya Makusudi. Farashuu ndiye aliemtia maneno binti Kocho na kumtoanyumbani kwao na kumtenga na wazazi wake. Kuharibika kwa Maimunakunaweza kuhusishwa na farashuu moja kwa moja. Talaka ya Tamima nayo inawezakuhusishwa na Farashuu moja kwa moja. Na kuharibika kwa Maimunakunahusishwa na mkabala huohuo. Alishirikiana na Kazija kumwandalia fumaniziMakusudi na mwanawe Mussa. Yeye ndiye aliyemtosa Maimuna katika zinaa. Jambo ambalo linatukumbusha umuhimu wa Farashuu ni kisasi. Visasi vilivyo
katika riwaya hii ambapo tukichunguza sana vinahusiana na muhusika huyu.

**Mussa:** Mussa ni mtoto wa kiume wa Bwana Makusudi ambaye akiwa katika umri mdogoMussa ananza kuiga mambo mabaya ya baba yake Makusudi. Mambo yenyewe nikama uafiriti na ukware wake unaonekana pale anapomwandama Kazija. Kazija nimtu mzima rika labda la mama yake Mussa. Lakini Mussa haoni taabukumwandama. Mussa ni mlevi anayachapa maji kikweli kweli. Tena katika kufananana baba yake anaiga hata mawazo yake yaani hata yeye anawadharau wanawakeMwandishi pia, amemnyima nafasi ya kukua.Baada lile fumanizi na baba yake.Mussa anatoweka bila kujulikana alipotelea wapi. Baada ya kifungo cha baba yake

Mussa alikuwa yuko mwaka wa tatu chuo kikuu, amekuwa msomi, tena daktarin aliamua kuyaacha machafu yote aliyokuwa nayo. Makusudi alipokuwa anamtafutaMaimuna anakutana na Mussa. Makusudi pindi alipopata maradhi anatibiwa naMussa na anaamua kutoa damu na kumsaidia baba yake, damu hii inaondoa uhasamauliopo wa Mussa na baba yake. Mussa anageuka mtu mwenye imani na kumhurumiaMaimuna mdogo wake pamoja na Tamima mama yake. Mussa anaungana na babayake kuukata utengano uliopo na aila yao Mussa ni muhusika asiyefahamika kwaurahisi.

**(c) Dhamira**

- Dhamira kuu: Usawa wa kijinsia
- Dhamira ndogo:

**1. Nafasi ya Mwanamke**

Huenda dhamiri au lengo la mtunzi likawa ni kuonyesha nafasi ya mwanamke katikajamii. Pengine amedhamiria kuonyesha kuwa mwananamke ni sawa na mwanamme.Ni juu ya mhakiki kuona kama kweli mwanamke amechorwa kama mwenye nafasisawa na mwanamme katika kazi hiyo. Mathalani, tuchukue jinsi Said A. Mohamedalivyoonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii ya wanaume wakatilikama vile Maksuudi. Mtunzi huyu amemuonyesha Maksuudi kama mwanaumemkatili anayejipenda sana, lakini hatimaye anaangushwa na mwanamke (Kazija).Vile vile twapata kwamba pale nyumbani kwa Maksuudi pametolewa amri fulani za kufuatwana, kama vile kutawishwa kwa bintiye na bibi kutohudumiwa na mkunga.

Lakini amri hii yapuuzwa na kuvunjwa kwa juhudi za mwanamke. Hivyo basitwaweza kutaja kwamba mtunzi alidhamiria kuonyesha kuwa hata mwanamke ananafasi katika jamii ya wanaume wenye kiburi na taasubi nyingi. Lakini dhamiri hiihaishikilii hadi mwisho wa hadithi kwani Kazija anatoweka hadithini naye Maimuna(ambaye ni mhusika muhimu) anaokolewa na mwanamme (Kabi)

**2. Uongozi Mbaya**

Hii ni dhamira inayojitokeza katika kazi nyingi za kifasihi, jamii nyingi za kiafrikazinaathirika na kadhia hii ya uongozi mbaya katika jamii zake. Dhana ya uongozimbaya ni kikwazo na

kipingamizi kikubwa cha maendeleo katika jamii nyingi zakiafrika. Katika riwaya ya Utengeno msanii ameidhihirisha waziwazi dhana hii kwakumchora Bwana Makusudi kama kielelezo cha uongozi mbaya katika jamii. BwanaMakusudi aliyatenda mambo mengi ambayo kwa nafasi yake katika utawalahakupaswa kuyatenda kwa raia wenziwe,alithubutu kusaliti nyumba yake,aliwanyanyasa wanawake na pia alishindwa kulipa fidia ya imani aliyopewa na raiawenziwe wakati wa kutetea uhuru wa nchi yake. Makusudi aligombaniauhuru wa nchi yake kwa tamaa kwamba wakitoka wale watu weupe,yeye atakuwammoja wapo atakae kamata nafasi zao.

**3. Usaliti**

Katika riwaya hii,msanii Said A.Mohamed amemchora Bw.Makusudi kama alama ya kiongozi msalitikwa jamii yake, alikuwa mstari wa mbele katika harakati za ukombozi zakumuondoa mtawala mweupe, lakini kumbe alikuwa na malengo ya paukwa pakawa,alitaka nafasi ya mtawala mweupe akae yeye.

**4. Ujumbe:**

Usawa wa kijinsia ni msingi wa maendeleo ya jamii. Mwanamke au msichana ni lazima awe haki sawa na mwanamume au mvulana. Msanii hana budi kudai kwamba unyonge wa mwanamke husababishwa na mfumo wa kijamii na hali hii inaweza kurekebishwa kwa kusambaza kiwango sawa cha elimu kwa watoto wote wasichana kwa wavulana. Wanapopokea elimu bora, wasichana au wanawake watakuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kupigania haki zao na pia kugombea nafasi mbalimbali katika jamii kwa kiwango sawa na wanaume. Kwa hiyo, inawabidi wasichana au wanawake kupigania haki zao ambazo kwa sasa zinatwaliwa na wanaume.

Kwa mfano, katika riwaya hii, suala la ukosefu wa elimu miongoni mwa wanawake limepewa nafasi kubwa. Madhila yanayowakumba wahusika wengi wa kike katika riwaya hii yanasababishwa na ukosefu wa elimu. Kazija anamlalamikia Mussa kuhusu jinsi wanawake walivyonyimwa nafasi za elimu huku wanaume wakinufaika:

*Nyinyi mliosoma elimu yenn bure. Hamjui mnakotoka wala*

*mnakokwenda....kh, usinisemeekisungu miye. Si ndivyo mlivyotuweka? tusisome tuwe wajinga .Mtutawale na kutuparamia maisha, ao sivyo*?

Kazija ametambua kwamba ukosefu wa nafasi za elimu kwa upande wa wanawake kumesababishwa na mfumo wa kijamii unaotawaliwa na taasubi ya kiume. Wanaume wanapewa nafasi za kusoma huku wanawake wakinyimwa nafasi kama hizo. Pengine, mwandishi ametuonyesha hali kama hii kupitia kwa wahusika Mussa na Maimuna. Musaanapelekwa shuleni huku Maimuna akifungwa nyumbani pamoja na mamake. Hali hii inaonyesha jinsi wavulana wanavyopendelewa katika jamii na wasichana kupuuzwa. Wavulana wanapewa nafasi ya kusoma huku wasichana wakikaa kizuzu bila kujielewa wala kuelewa jamii. Kwa sababu ya kukosa elimu, Maimuna haielewi jamii ndiyo maana anapoamua kutoroka kwao anatumbukia kwenye shimo la ukahaba. Kama Maimuna angekuwa na elimu, labda elimu hii ingemsaidia ajielewe na labda kuchagua maisha mema kuliko kuingilia mambo ya ukahaba. Mwandishi pia amedhihirisha kwamba msichana anaposomeshwa huwa ni kwa bahati tu.

Ili usawa wa kijinsia uweze kutimizwa na kuimarishwa, ni lazima mwanamke ashirikishwe kielimu, kiuchumi, kisiasa, kisheria, n.k.

**(d) Migogoro :**

Riwaya nzima imeongozwa na mgogoro wa kijinsia. Mgogoro huu umetegemea mambo mbalimbali kama vile :

- **Dhuluma katika ndoa**

Mwandishi ametumia ndoa kumsawiri mwanamke kama mtumwa wakumhudumia mwanaume, mwanamke hana uhuru wa kujiamulia kuhusu jambo lolotemaishani.

- **Mwanamke kama kahaba**

Maimuna anatoroka maisha ya kiutumwa katika nyumba yao. Kwa vilehajawahi kutoka nyumbani na kutambua jinsi maisha yalivyo. Anapotoroka, Maimuna anatumbukia kwenye shimo la ukahaba si ye kiuchumi bali uhuru aliyonyimwa na babake Bwana Makusuudi. Pia

mwandishi anatumia mhusika Kazija, kuoneshjinsi alivyoendeleza ukahaba. Kujipamba kwake Kazija, kujitia manukato yenye harufi ya kuvutia sana, maumbile ya mwili yake iliwavutia vijana na wazee ingawa kwake hii ilikuwa njia mojawapo ya yeye kupata riziki ya maisha.

- **Ukandamizaji na unyonyaji**

Ukandamizaji umedhihirishwa na unyanyasaji wa haki za wanawake kwa kunyimwa fursa ya kupata elimu. Unyonyaji au dhuluma iliyoendelezwa ma Maksuudi iliiangamiza sana jamii na kuingusha katika maendeleo yake.

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.88)**

*Mwalimu achague dondoo la riwaya lililorekodiwa; wanafunze wasikilize dondoo hilo kisha waeleze maudhui (dhamira na ujumbe) yaliyotarajiwa.*

**Kuandika: Kipengele hiki cha somo la ‘Uhakiki wa riwaya’ kiongezwe.**

*Kwa kazi binafsi, mwalimu awachagulieriwayakisha wafanye uhakiki wa riwaya hiyo kwa kuzingatia vipengele vya uhakiki husika. Mwalimu ahakikishe kuwa kila mwanafunzi ameshirikishwa katika kazi ile ya uhakiki.*

**2.6. TATHMINI YA MADA YA PILI**

- ☞ **(Uk. 91 – 92)**

*Tathmini hii ipendekezwe kuwa jaribio la jumla. Kwa kazi binafsi, kila mwanafunzi anapaswa kujibu maswali yote aliyopewa kwa kutumia karatasi. Inambidi mwalimu kuyaandaa majibu awali pamoja na vipimo vya tathmini kwa kila jibu.*

**Tanbihi:**Mwalimu halazimishwi kutoa jumla ya maswali yote kwa wanafunzi. Inambidi awe huru katika kuchagua maswali anayoona kuwa ni muhimu kuliko mengine.

Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa kurejelea.

**Zoezi la 1**

1. Shairi ni mtungo wenye muundo na lugha ya kisanii unaofuata utaratibu wa vina na mizani, hisi au tukio juu ya maisha au jambo na hufuata utaratibu maalumu wa urari na muwala unaozingatia kanuni za utunzi wa mashairi yanayohusika.

2. Muundo wa shairi huhusisha: aina ya shairi, bahari ya shairi, idadi ya mishororo, jumla ya beti, kibwagizo (iwapo kipo), mpangilio wa vina, mpangilio na idadi ya mizani na vipande vya shairi.
3. a) Mishororo ni mistari katika ubeti wa shairi. b) Mizani ni silabi zinazotamkika katika mshororo wa shairi. c) Vina ni silabi za namna moja zinazopatikana katikati na/au mwishoni mwa mishororo. d) Kibwagizo ni mshororo wa mwisho unaorudiwarudiwa katika kila ubeti. Kibwagizo hubeba kiini cha shairi.

**Zoezi la 2**

| Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendeka |
|---|---|
| kimbilia | kimbilika |
| chomea | chomeleka |
| lia (chakula) | lika |
| pandia | pandika |
| kalia | kalika |

**Zoezi la 3**

| Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendeka | Kauli ya kutendewa | Kauli ya kutendua |
|---|---|---|---|
| pakia | pakika | pakiwa | pakua |
| chomea | chomeka | chomewa | chomoa |
| tendea | tendeka | tendewa | tendua |
| fyatia | fyatika | fyatiwa | fyatua |
| chimba | chimbika | chimbiwa | chimbua |

**Zoezi la 4**

1. Tamthilia ni utungo uliotungwa kwa lengo la kuigizwa jukwaani na huwa kwa muundo wa mazungumzo baina ya wahusika. Pia, huitwa mchezo wa kuigiza.

2. Sifa za tamthilia:

a) Huwa na mazungumzo na majibizano.

b) Huwa na maelezo ya jukwaani yanayopendekeza jukwaa litakavyokuwa.

c) Huwa na maelezo kuhusu wahusika: mavazi yao, hisia na matendo.

d) Hugawika katika maonyesho/matendo mbalimbali kutegemea matukio.

e) Huhusisha mgogoro fulani hasa katika upeo wake.

f) Utendaji wa tamthilia huambatana na miondoko – viungo vya mwili kusogezwa.

g) Hushirikisha hadhira.

3. Tofauti kati ya riwaya na tamthilia

a) Riwaya huwa ndefu kuliko tamthilia.

b) Riwaya huandikwa kinathari ilhali tamthilia huwa katika muundo wa mazungumzo na majibizano.

c) Riwaya ina wahusika wengi kuliko tamthilia.

**Zoezi la 5**

1. Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni iliyoandikwa kinathari, aghalabu inayoeleza ukweli fulani wa maisha.

2. Sifa za riwaya:

a) Huwa na vipengele vifuatavyo: ploti/msuko, hadithi, usimulizi, uhusika, mazingira, wakati, mitazamo na mazungumzo ya wahusika.

b) Huwa na maelezo ya simulizi kulingana na vile hadithi inavyotokea kiwakati na kimasafa.

c) Huwa na maelezo ya wahusika kuhusu: wasifu wao, mavazi yao, tabia zao, sifa na dosari, matendo yao yanavyoathiri nafsi zao na kuwaathiri wahusika wengine.

d) Huwa na urefu wa kutosha kushughulikia mahitaji ya mtunzi.

e) Huchunguza kwa kina jamii inayosawiriwa.

3. Wahusika hutumiwa kama vyombo vya kuuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa riwaya kwa wasomaji.

**Zoezi la 6**

1. Ni hadithi inayoshughulikia suala fulani kwa muhtasari.

2. Sifa za hadithi fupi:

a) Huwa fupi na inayoweza kusomeka kwa mkao mmoja.

b) Huwa na wahusika wachache.

c) Huwa na mhusika mkuu mmoja ambaye humwongoza msomaji.

d) Hushughulikia tukio moja kuu katika maisha ya mhusika mkuu.

e) Haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo.

3. a) Hadithi fupi huwa na wahusika wachache sana ilhali riwaya huwa na wahusika wengi.

b) Hadithi fupi huhusisha visa vifupi vifupi ilhali riwaya huwa usimulizi wa matukio marefu.

**Zoezi la 7**

| **Fasihi simulizi** | **Fasihi andishi** |
|---|---|
| i) Umri: Ina umri mkubwa kuliko fasihi andishi. Huitwa fasihi kongwe. | Ina umri mfupi kuliko fasihi simulizi. Hii inatokana na ukweli kuwa maandishi yamegunduliwa hivi karibuni |

| | |
|---|---|
| ii) Uhifadhi: Inahifadhiwa kwenye kichwa cha msimulizi na kusambazwa kwa njia ya masimulizi/kimapokeo. | Inahifadhiwa kwa maandishi na kusambazwa kwa njia ya kusoma maandishi. |
| iii) Tanzu: Ina tanzu mbalimbali lakini ni tanzu nyingi kuliko zile za fasihi andishi. Kwa mfano: mazungumzo, ushairi, hadithi, semi, ngomezi, miviga n.k. | Ina tanzu nne tu: ushairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya. |
| iv) Uwasilishaji: Huwasilishwa kwa njia ya simulizi ya mdomo. Hutegemea sauti. | Huwasilishwa kwa njia ya maandishi. |
| v) Mabadiliko: Hubadilika kulingana na mfumo wa kihistoria. Aidha, fanani/msimulizi anaposimulia hadithi anaweza kuongeza au kupunguza jambo kila anapowasilisha sanaa yake. Pia, fanani akifa, kazi yake nayo italazimika kubadilika kutokana na yule atakayechukua nafasi yake. | Haibadiliki baada ya kuandikwa ila mwandishi anapoandika upya |
| vi) Umiliki: Jamii nzima ndiyo inayohusika katika kuimiliki fasihi hii | Mtunzi wa kazi hiyo ndiye mmiliki wa kazi yake. |
| vii) Muda wa utunzi: Baadhi ya tanzu za fasihi simulizi huibuka papo hapo. Kwa mfano: semi. | Huhitaji muda kutunga. |

## 2.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI

### 2.7.1. Kazi za urekebishaji

1. Uhakiki wa kazi za fasihi ni nini?
2. Tuzungumziapo fani katika hadithi fupi au riwaya, tunahusisha vipera gani?
3. Jadili vipengele muhimu vya uhakiki wa maudhui katika fasihi andishi

4. Kwa kutegemea mifano, toa aina nne za kauli ya vitenzi.

**Majibu**

1. Uhakiki ni kitendo cha kutathmini, kueleza, kuainisha na kutoa maoni juu ya kazi fulani ya fasihi kwa kuongozwa na kaida maalum. Kwa kiwango cha elimu ya sekondari mhakiki hufanya kazi ya uhakiki ili kuonesha mambo yanayojitokeza kama vile, dhamira, migogoro, ujumbe, falsafa, mtazamo, msimamo n.k

2.

- Wahusika na tabia zao
- Muundo
- Lugha
- Mtindo
- Mandhari

3. Maudhui hujengwa na vipengele vifuatavyo:

- Dhamira
- Migogoro
- Falsafa
- Ujumbe
- Msimamo wa msanii

4. Kauli katika Kiswahili

- Kauli ya kutenda. Mfano : Mwanafunzi anajifunza Kiswahili
- Kauli ya kutendea. Mfano : Nilimwandikia rafiki yangu barua ndefu.
- Kauli ya kutendewa. Mfano: Tumeambiwa habari nzuri
- Kauli ya kutendeka. Mfano : Jaribio la Kiswahili litafanyika kesho.

### 2.7.2. Kazi za uimarishaji

**Maswali :**

1. Eleza umuhimu wa uhakiki wa kazi za fasihi
2. Kwa kutegemea mfano, eleza jukwaa katika tamthiliya
3. Jadili sifa za hadithi fupi
4. Weka vitenzi vya sentenzi zifuatazo katika kauli ya kutendua

a) Tulificha mali yetu mahali pale

b) Amefunga mlango kwa kufuri

c) Tumevaa sare zetu

**Majibu:**

1. Husaidia wasomaji kuilewa kazi ya fasihi kwa urahisi:

a) Watunzi wa kazi za fasihi hutofautiana katika matumizi ya lugha na taswira, hivyo mhakiki anapofanya kazi ya uhakiki anamsaidia msomaji kuelewa vipengele hivi kwa kuvifafanua kwa lugha rahisi.

b) Husaidia ukuaji wa kazi za fasihi:

Mhakiki anapoonyesha ubora na udhaifu wa kazi ya mtunzi fulani, watunzi wengine pia watafunguka kifikra na kutunga kazi iliyobora zaidi.

c) Hukuza uelewa wa mhakiki: Kwa kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi, mhakiki hujiongezea maarifa ya lugha pamoja na mambo yanayotokea katika jamii.

2. Jukwaa ni mandhari au mahali pa kuchezea tamthiliya. Kuna aina mbili za jukwaa : Jukwaa halisi na jukwaa la akilini.
3. Sifa za hadithi fupi:

a) Huwa fupi na inayoweza kusomeka kwa mkao mmoja.

b) Huwa na wahusika wachache.

c) Huwa na mhusika mkuu mmoja ambaye humwongoza msomaji.

d) Hushughulikia tukio moja kuu katika maisha ya mhusika mkuu.

e) Haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo.

4. Fasihi andishi hujigawa katika tanzu kuu muhimu kama ifuatavyo :
   - Hadithi fupi. Mfano: Mtoto yatima na mama wakambo
   - Riwaya. Mfano : Utengano au Adili na Nduguze
   - Tamthiliya. Mfano : Hawala ya Fedha au Kijiba cha Moyo
   - Mashairi. Mfano : Tuyalinde mazingira
5. 

a) Tulifichua mali yetu mahali pale
b) Amefungua mlango kwa ufunguo
c) Tumevua sare zetu

**2.7.3. Kazi kwa wanafunzi wenye kipawa na kipaji**

**Maswali :**

1. Unajua nini kuhusu Said A. Mohamed ?
2. Jadili tabia za mhusika Maksuudi katika riwaya ya Utengano.
3. Badili vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kufanywa

a) Baba yangu amemchinja ng'ombe
b) Simba amemwua twiga
c) Mwizi amemwiba mama yule pesa zake

**Majibu:**

1. Profesa Said Ahmed Mohamed alizaliwa katika mtaa wa Limbani, Wete Pemba, tarehe 12 Disemba, 1947. Kutoka kitabu chake cha kwanza cha riwaya ya Asali Chungu hadi sasa,Said ameandika jumla ya vitabu sitini na saba vikiwemo riwaya, hadithi fupi, mashairi na heshima za lugha na Isimu. Vitabu vya hivi karibuni ni Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006), Nyuso za Mwanamke (2010), Atamlilia Nani (2009), Vipawa vya Hasina (2009), Mkama Ndume (2013), Masikini Bibi Yangu (2009), Kimya Kimya, Mashetani Wamerudi. Riwaya hizi zina mwelekeo mpya wa usasa baadaye tofauti na riwaya kabla ya hizi. Riwaya na kazi nyengine za fasihi ni pamoja na Sikate Tamaa (2001), Kina cha Maisha (1984) na Jicho la Ndani (2000). Riwaya zake nyingine ni Posa za Bi Kisiwa (2007), Asali Chungu (1977), Dunia Mti Mkavu (1980), Kiza katika Nuru (1988) na Tata za Asumin (1990).Utengano ni mojawapo ya riwaya alizotunga. Riwaya hii inajadili mambo ya usawa wa jinsia ambapo wanawake wastahili kuitikia mwito wa kutetea haki zao.
2. Maksuudi ni mhusika mkuu katika riwaya ya Utengano. Mhusika huyu ameonekana kuwa na tabia tofauti. Kwa upande wa familia, Makusudi ni kiongozi asiyehishimu madaraka yake; ni mwingi wa hadaa na udanganyifu. Makusudi alikuwa mtu dhalumu, afiriti na mwingi wa maovu. Makusudi anajielewa kuwa afanyayo siyo na ni kinyume na maadili ya jamii. Anajali

sana nafsi yake, Anajali ile nafsi ya ujitajirisha mwenyewe. Imani ya Makusudi juu ya wanawake ni jambo litishalo. Kwake mwanamke si kitu. Imani hii ndio iliyomfanya kumtesa Mwanasururu. Kwa upande wa uongozi, Maksuudi alikuwa mmoja wa waanzilishi wa chama cha Mwafrika kilichodai uhuru wa Mwafrika na kumuondoa mkoloni. Alikuwa kiongozi shupavu mwenye nia thabiti. Alipigania uhuru wananchi yake nia moja. Licha ya yote hayo makusudi alikuwa mwalimu wa dini. Uhuru ulipopatikana Makusudi alipewa madaraka kama mkuu wa wilaya. Baada ya kuyapata madaraka aliisaliti ile nia thabiti ya kutetea wananchi. Aakapata nafasi ya kunyanganya wananchi. Katika wale wengi aliowadhulumu, kuwahini na kuwafanya watumwa walikuwa wanawake. Matendo yake maovu yalimpeleka jela.

3. Vitenzi katika kauli ya kutendwa

a) Ng’ombe amechinjwa na baba yangu.
b) Twiga ameuawa na simba.
c) Mama yule ameibiwa pesa zake na mwizi.

## MADA KUU YA 3 : UBUNAJI

## MADA NDOGO YA 3: HOTUBA NA UFUPISHO

### 3.1. Uwezo upatikanao katika mada

Kutunga hotuba na kufupisha hati mbalimbali za Kiswahili na kuchambua vitenzi kwa njia ya uambishaji.

### 3.2. Ujuzi wa awali

Katika kidato cha nne, wanafunzi walishughulikia somo la muhtasari pamoja na insha mbalimbali. Vilevile, dhana ya ufupisho iligusiwa katika kidato cha tano. Haya yamethibitishwa na mada mada zifuatazo:

Mada za Kidato cha nne:

- Muhtasari, fani na maudhui katika fasihi simulizi; somo la 14
- Insha za masimulizi na kubuni na uandishi wa ripoti.

Mada za Kidato cha tano:

Ufahamu na Ufupisho

### 3.3. Kidokezo cha mada na maelekezo yake

#### 3.3.1. Kidokezo cha mada

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali yafuatayo:

- Ujumbe unaotolewa na Rais wa Jamhuri kwa raia huitwa nini?
- Mtangazaji habari hutumia mbinu gani katika kutangaza ujumbe huo uliotolewa na Rais?

### 3.3.2. Maelekezo ya kidokezo cha mada

Mwalimu anaweza kuchagua rekodi ya hotuba moja iliyotolewa na kiongozi mmoja na kuwaomba wanafunzi wasikilize hotuba hiyo na kutambua hatibu ni nani, ni nini kinachozungumziwa. Pia, anaweza kutumia rekodi ya ripoti ya mtangazaji Habari fulani na kuwaomba wanafunzi wategе sikio na kutambua jinsi mtangazaji habari alivyomnukuu hatibu.

### 3.3. Orodha ya masomo

| | Kichwa cha somo | Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema) | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|
| **1** | Dhana ya hotuba na mwongozo wa utungaji wake | **Maarifa na ufahamu:** Kutoa dhana ya hotuba na mwongozo wa utungaji wake<br>**Stadi :** Kueleza dhana ya hotuba na mwongozo wa utungaji wake.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuimarisha tabia ya kuwa wazi katika hotuba na kutumia msamiati maalum. | 4 |
| **2** | Uchambuzi wa hotuba | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha taratibu za uchambuzi wa hotuba<br>**Stadi** : Kuchambua hotuba kwa kuzingatia taratibu muhimu za uchambuzi.<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuheshimu mawazo makuu ya mtu aliyehotubu bila kuyapotosha | 8 |
| **3** | Dhana ya ufupisho na sifa zake | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya ufupisho na sifa zake | 6 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | **Stadi**: Kujadili dhana ya ufupisho na sifa zake<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kujenga nia ya kulinganisha habari tofauti na ufupisho wake | |
| **4** | Mbinu za ufupisho | **Maarifa na ufahamu:** Kutambua mbinu za ufupisho wa habari<br><br>**Stadi :**Kufupisha habari kwa kuzingatia mbinu za ufupisho.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kutegemea mbinu za ufupisho ili kuepuka tabia ya kunakiri sentensi | 6 |
| **-** | Sarufi: Uambishaji wavitenzi | **Maarifa na ufahamu:** Kubainisha viambishi vya uambishaji wa vitenzi katika Kiswahili<br><br>**Stadi :** Kuambisha vitenzi kwa kuzingatia kanuni za uambishaji.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kukuza maarifa kwa kujishughulisha na mazoezi ya uambishaji wa vitenzi katika Kiswahili. | - |
| **Tathmini ya mada** | | | 2 |
| **Jumla ya vipindi vya mada ya kwanza** | | | 26 |

**Maelekezo kuhusu uandaaji wa masomo yaliyoonyeshwa hapo juu**

- **Vipengele vya muundo wa somo**

Kila somo hujengwa na vipengele vifuatavyo:

1. Kusoma na ufahamu vifungu vya habari

2. Msamiati kuhusu vifungu vya habari vilivyosomwa

3. Matumizi ya lugha
4. Kusikiliza na kuzungumza
5. Sarufi
6. Kuandika

- **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila kipengele cha somo**

**(a) Kusoma na ufahamu kifungu cha habari**

- **Kusoma:** Kwa kutegemea kitabu cha mwanafunzi au nakala ya vifungu vya habari, wanafunzi washirikishwe kwenye kazi ya kusoma kifungu husika kwa njia tofauti: kusoma kimya au kusoma kwa sauti. Mwalimu ashirikishe wanafunzi wote kwenye kazi hii kwa kutumia njia moja au nyingine. Ili kurahisisha kazi hii na kufaulu kuwashirikisha wanafunzi wote, kazi hii huweza kufanyika katika makundi madogomadogo au katika jozi.
- **Ufahamu:** Ufahamu wa kifungu cha habari huweza kufikiwa kwa njia nyingi kama vile kufasiri michoro au picha zilizotumiwa katika kifungu cha habari husika; kuuliza maswali ya ufahamu, kutoa dhamira kuu zilizosisitiziwa katika kifungu cha habari, kutoa muhtasari wa habari iliyozungumziwa, n.k. Kwa hiyo, inambidi mwalimu achagua njia moja au zaidi baadhi ya hizi au nyingine ambayo haikutajwa hapa juu.

**(b) Matumizi ya msamiati**

Katika kipengele hiki, mwalimu anastahili kujenga kwa wanafunzi tafakuri tunduizi, yaani kuwaongoza wanafunzi kugunduwa wao wenyewe maana ya msamiati husika kwa kutegemea muktadha wa kifungu cha habari kwa ujumla. Si vizuri kupendekeza matumizi ya kamusi kama hatua ya kwanza ya kutoa maana ya msamiati. Kadhalika, maana ya msamiati huweza kupatikana kwa kutumia michoro au picha husika. Vifaa hivi huweza kuandaliwa na mwalimu lakini ni vizuri kuwashirikisha wanafunzi katika zoezi la kuchora michoro kulingana na maana ya msamiati husika. Pia, mbinu ya kutoa kinyume au kisawe cha msamiati husika huwa muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati.

**(c) Matumizi ya lugha**

Ni wajibu wa mwalimu kuhusisha kifungu cha habari na maisha ya kila siku ya wanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima wanafunzi wapewe kazi zinazostahili kuamsha akili ili kutafuta njia ya utatuzi wa matatizo yanayoweza kuikumba jamii wanamoishi.

**(d) Kusikiliza na kuzungumza**

- Kusikiliza: Wanafunzi wanaweza kukuza uwezo wa kusikiliza kwa njia tofauti: kusomewa kwa sauti kifungu cha habari, kusikiliza habari au hotuba zilizorekodiwa, kusikiliza hadithi au habari kwenye redio, televisheni au tarakilishi. Kwa hiyo, inambidi mwalimu kutumia njia hizi tofauti za kukuza stadi za kusikiliza kwa wanafunzi.
- Kuzungumza: Kuna njia nyingi za kukuza stadi za kuzungumza kwa wanafunzi. Baadhi ya hizi kuna midahalo na mijada, maigizo, uwasilishaji darasani, nyimbo, michezo, mazungumzo, masimulizi, mhadhara, n.k. Katika kazi zake za ujifunzaji, mwanafunzi ashirikishwe kikamilifu katika kazi mbalimbali kwa kuchanganya mbinu zilizotajwa hapo juu.

**(e) Sarufi**

Sarufi inayotarajiwa katika uwezo mahsusi wa mada **haifundishwikamasomo la kujitegemea baada ya mada** bali hujitokeza mwishoni au kati kati ya kila somo. Kwa hiyo vipera vya sarufi hii hujigawa kulingana na idadi ya masomo yanayoiunda mada nzima.

**(f) Kuandika**

Wakati wa kazi zinazofanyika katika makundi madogomadogo, wakati wa maelezo ya mwalimu, wakati wa uwasilishaji wa kazi darasani, wakati wa kutoa muhtasari wa somo na hasa wakati wa majaribio na mitihani au katika kuziandaa kazi za nyumbani, inambidi mwalimu awashirikishe na kuwahimiza wanafunzi kuandika. Pia, mwalimu asisahau imla kwa wanafunzi katika kazi zao za ujifunzaji.

## SOMO LA 1: DHANA YA HOTUBA NA MWONGOZO WA UTUNGAJI WAKE

### i) Malengo ya ujifunzaji

Kutoa na kueleza dhana ya hotuba na mwongozo wa utungaji wake.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za hotuba
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Hotuba zilizorekodiwa
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

**Tanbihi**: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenye matatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

### iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

### iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi

**Kusoma na ufahamu:Hotuba kuhusu usafi( Uk.96)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasoma kifungu cha habari husika na kutoa majibu sahihi kwa maswali husika. Majibu yanayopendekezwa ni haya yafuatayo:*

a. Mkuu wa Mkoa wa Kusini, wazazi, walimu, wanafunzi na wageni waalikwa.

b. Afisa wa Afya katika Mkoa wa Kusini.

c. Mazingira safi husababisha kuwepo kwa hewa safi ya kupumua, maji safi ya kutumiwa na mahali safi pa kuishi.

d. Kumwaga kemikali na uchafu kwenye vianzo vya maji.

2. Usafi wa mwili huzuia harufu mbaya kwa binadamu na huzuia magonjwa ya tumbo.

3. Mbu na chawa. Mbu husababisha malaria na chawa hufyonza damu.

4. Kuoga kila siku, kupiga mswaki kila siku, kunyoa nywele zinazofaa kunyolewa na kuchana zile za kichwani, kuvaa nguo safi kila siku, kukata kucha na kulala kwenye malazi safi.

5. Inatoa utambulisho wa waliohudhuria, mzungumzaji na pia mada ya hotuba.

6. Nafsi ya kwanza, umoja.

7. Kwa kuwashukuru wote waliohudhuria.

**Matumizi ya msamiati**

**Zoezi la 1(Uk.97 )**

*Katika jozi, wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi husika, kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kama ulivyotumika katika hotuba waliyosoma kuhusu usafi. Majibu yanayopendekezwa ni yafuatayo.*

1. waalikwa - watu walioalikwa kuhudhuria hafla fulani

2. natumai - natarajia

3. mkoa - eneo la kijiografia linalotawaliwa na mkuu wa mkoa

4. mkutano - shughuli fulani maalumu yenye watu wanaojadiliana jambo au kuisikiliza hotuba

5. madhara - jambo lenye kuleta maangamizi au uharibifu

6. kemikali - dawa yenye uwezo wa kubadilisha kitu kikemikali

7. mitaro - mifereji mirefu ya kupitisha bomba la maji

8. majaa - mahali maalumu palipotengwa kutupia taka

9. maadili - tabia njema

10. vianzo - maeneo ambayo ni asili ya kitu fulani

**Mifano ya sentensi:**

1. Wageni waalikwa watakaa kwenye hema.
2. Natumai umeoga ukaacha kunuka.
3. Mkoa wa Kati umeathirika na kiangazi.
4. Nitaomba kwenye mkutano ujao.
5. Madhara ya ukosefu wa maji safi ni mengi.
6. Kuna kemikali hatari kwenye lango la kiwanda hiki.
7. Mitaro iliyochimbwa juzi imezibwa.
8. Takataka katika jiji hutupwa kwenye majaa.
9. Maadili mema ya mtoto ni furaha ya kila mzazi.
10. Kulikuwa na samaki kwenye vianzo vya maji yale.

**Zoezi la 2 (Uk.97 - 98)**

*Katika katika jozi, wanafunzi wachunguze picha zilizotolewa na kueleza madhara yake kwa binadamu na wanyama wengine. Tazama majibu yanayopendekezwa.*

A. Wanyama wakinywa maji machafu watapatwa na ugonjwa. Pia, wanyama hawa wakikanyaga ndani ya maji na kuacha samadi yao humo basi huweza kuyachafua maji na kuyafanya kuwa hatari kwa binadamu.

B. Kemikali zinazomwagwa na viwanda ni hatari kwa afya ya binadamu, mimea na wanyama.

C. Utupaji wa taka ovyo husababisha harufu mbaya ambayo huathiri afya ya binadamu. Baadhi ya wadudu ambao huvutiwa na takataka huweza kusababisha magonjwa mbalimbali kwa binadamu.

**Matumizi ya lugha (Uk.98).**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili sehemu kuu za hotuba kwa kurejelea mfano wa hotuba waliyosoma hapo awali kuhusu usafi. Kila kikundi kiwasilishe matokeo ya majadiliano yao mbele ya darasa. Hakikisha kuwa wanafunzi wameyagusia maoni yafuatayo.*

Sehemu za hotuba ni:

a) Mada au kichwa cha hotuba  Mada ya hotuba hutambulisha jambo linalozungumziwa na mara nyingi huwa haizidi maneno manane.

b) Utangulizi au mwanzo wa hotuba  Utangulizi wa hotuba mara nyingi huwa ni aya moja tu. Huhusisha kuwatambua wanaokusikiliza pamoja na kutoa salamu. Mzungumzaji hujitambulisha hapa.

c) Mwili wa hotuba  Sehemu hii hubeba ujumbe kamili wa hotuba nzima. Aya kadhaa huandikwa hapa kwa namna ya kutiririsha maudhui yanayozungumziwa kutoka mwanzo hadi mwisho wa hotuba.

d) Hitimisho au mwisho wa hotuba  Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyozungumziwa katika mwili wa hotuba. Mzungumzaji huwashukuru wasikilizaji na kuwaaga.

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.99)**

*Kwa kazi binafsi, wanafunzi watunge hotuba kuhusu mada yoyote kwa kuzingatia sehemu za hotuba walizojadili hapo awali. Kila kundi liwasilishe hotuba yake mbele ya wanafunzi wenzao.*

Mwalimu atathmini namna wanafunzi watakavyotoa hotuba mbele ya wanafunzi wenzao. Awahimize wazingatie ujasiri wakati wa kuongea mbele ya watu pamoja na matumizi ya lugha rasmi na sahihi kisarufi.

**Kuandika (Uk. 99)**

*Katika jozi, wanafunzi wabuni hotuba kuhusu umuhimu wa maji kwa binadamu na wanyama kwa kuzingatia sehemu kuu za hotuba pamoja na sifa za hotuba mlizofundishwa hapo awali.*

*Mwalimu atathmini hotuba za wanafunzi. Sharti zizingatie muundo kamili wa kuandika hotuba.*

*Kwa mfano:*

**Hotuba kuhusu Umuhimu wa Maji kwa Binadamu na Wanyama**

*Mwenyekiti wa chama cha mazingira, walimu na wanafunzi, hamjambo? Leo nina furaha kuwa hapa ili niwape hotuba yangu kuhusu umuhimu wa maji kwa binadamu na wanyama. Kwanza kabisa, maji ni muhimu kwetu sisi binadamu kwa sababu maji ni uhai. Sisi hunywa maji ili kukata kiu.*

*Maji hutumika katika shughuli zetu za nyumbani. Ili kuosha nguo zetu, sisi hutumia maji. Pia, maji hutumika kusafisha vyombo na nyumba. Sharti binadamu waishi katika mazingira safi. Hii ndiyo maana sisi hutumia maji kudumisha usafi. Mbali na usafi wa mazingira yetu, kuna usafi wa mwili ambao huhitaji maji. Sisi hutumia maji kuoga ili tuonekane nadhifu.*

*Binadamu pia hutumia maji katika shughuli za kilimo. Mimea yetu haiwezi kunawiri bila kunyunyiziwa maji. Sisi huinyunyizia mimea yetu maji ili inawiri na kutupa mazao mengi. Maji pia hutumiwa na binadamu katika kufuga samaki. Kunao binadamu ambao hujenga vidimbwi vya kufugia samaki na wao huhitaji maji. Samaki hao hukua na kuuzwa kisha wakawaletea binadamu pesa za kujikimu kimaisha.*

*Wanyama pia huhitaji maji. Maji ni muhimu kwa wanyama kwa sababu wao hunywa maji ili kukata kiu. Mbali na hayo, wanyama wanaofugwa nyumbani hurushiwa dawa ya kuzuia magonjwa. Dawa hiyo huwa imechanganywa na maji.*

*Wanyama wa majini na samaki huhitaji maji ili kuishi. Wanyama hawa ni kama vile: mamba, viboko na kobe wa majini. Wao hutegemea maji kama makazi yao. Ni wajibu wetu sisi binadamu kuyatunza mazingira na vianzo vya maji ili tuishi maisha mema.*

*Asanteni nyote kwa kuhudhuria na kunisikiliza. Mungu awabariki.*

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili mwongozo wa kutunga hotuba na kuwasilisha kazi yao mbele yad arasa.*

*Maoni yanayopendekezwa :*

Mwongozo wa kuandika hotuba:

1. Aya ya kwanza huhusu kutambulisha kitakachozungumziwa, salamu na kujitambulisha kwa msemaji.
2. Hotuba huandikwa katika nafsi ya kwanza na huwa katika usemi asili.
3. Hotuba huandikwa katika wakati uliopo.
4. Aya kadhaa zinazofuata utangulizi huhusu ujumbe wa hotuba nzima.
5. Aya ya mwisho huhitimisha hotuba kwa kutoa shukrani na kuwaaga wasikilizaji.
6. Lugha sahihi kisarufi na inayoeleweka hutumika.

**Sarufi**: **Uambishaji wa vitenzi (100 – 101)**

**Zoezi la 3**

*Katika jozi, wanafunzi waonyeshe sehemu zinazounda maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi zilizotolewa.*

*Jibu:*

1. (atachora) = a+ta+chor+a
2. (anakimbia) = a+na+kimbi+a

3. (alipanda) = a+li+pand+a

4. (anawafundisha) = a+na+wa+fund+ish+a

**Zoezi la 4**

*Kwa kazi binafsi, wanafunzi wachunguze vitenzi katika jedwali lililotolewa kwa kuonyesha silabi zinazoviunda. Jazeni kwa usahihi nafasi zilizoachwa wazi.*

*Jibu linalopendekezwa :*

| Kitenzi | Kiambishi cha nafsi | Kiambishi cha wakati | Mzizi wa kitenzi | Kimalizio |
|---|---|---|---|---|
| alicheza | a | li | chez- | a |
| ataimba | a | ta | imb- | a |
| tutatembea | tu | ta | tembe- | a |
| watapanda | wa | ta | pand- | a |

**Zoezi la 5**

*Katika jozi, wanafunzi waonyeshe mizizi ya vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zilizotolewa kama ifuatavyo :*

1. -shon

2. -som

3. -sameh, -kosok- (- sameh-, - kose-)

4. –angali

5. -andik

**Zoezi la 6**

*Katika jozi, wanafunzi waainishe vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi husika kwa kuonyesha viambishi vinavyoviunda.*

Jibu :

1. a+na+chor+a (nafsi ya tatu umoja, wakati uliopo, mzizi, kimalizio)

2. a+na+kimbi+a (nafsi ya tatu umoja, wakati uliopo, mzizi + kimalizio)

3. a+na+fum+a (nafsi ya tatu, umoja, wakati uliopo, mzizi + kimlizio)

4. ni+na+andik+a (nafsi ya kwanza umoja, wakati uliopo, mzizi, kimalizio)

5. ni+ta+fut+a (nafsi ya kwanza umoja, wakati ujao, mzizi, kimalizio)

## SOMO LA 2: UCHAMBUZI WA HOTUBA

### i) Malengo ya ujifunzaji

Kuchambua hotuba kwa kuzingatia taratibu muhimu za uchambuzi.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za hotuba
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Hotuba zilizorekodiwa
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

**Tanbihi:** Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenye matatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

### iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu:Hotuba kuhusu ushirikiano wa kijinsia( Uk.104)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome kwa makini kifungu cha habari husika na kujibu maswali ya ufahamu.*

Majibu yanayopendekezwa:

1. Ili kujadili umuhimu wa kushirikiana kijinsia ili kuboresha maisha.
2. Mgeni wa heshima, wageni waalikwa, machifu, manaibu wa machifu, mwenyekiti wa baraza la wazee, wazee wa kijiji na wananchi.
3. Kuwatambua waliohudhuria na kutaja madhumuni ya mkutano.
4. Kwa ushirikiano.
5. Shughuli za ukulima na ufugaji.
6. Wanaume hudhani kuwa wanawake hawana uwezo wa kufanya kile ambacho wao hufanya. Wao huwaona wanawake kama viumbe dhaifu. (Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi).
7. Ndiyo. Mwanamke ana faida katika jamii kwa kuwa yeye hushiriki katika takribani shughuli zote za kuendeleza jamii. (Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi).
8. Usafishaji wa mazingira.
9. Himizo kwa wananchi wote kujitahidi kadri ya uwezo wao ili kuishi vyema na watu wa jinsia zote bila kuwabagua wala kuwadharau wengine. 10. Mungu alituumba kwa kutumia vifaa sawa.

**Matumizi ya msamiati**

**Zoezi la 1(Uk.105)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi husika kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo. Wazingatie matumizi ya msamiati huo katika muktadha wa hotuba waliyosoma. Wanaweza kutumia kamusi inapohitajika.*

1. mwenyekiti - mtu anayeteuliwa kuongoza mkutano
2. mwito - taarifa ya kumtaka mtu aende mahali fulani; mwaliko
3. dhahiri shahiri - wazi kabisa
4. unyanyapaa - tabia ya kumtenga mtu kwa hali aliyo nayo
5. jinsia - hali ya mtu kuwa mwanamume au mwanamke
6. alituhimiza - alitushawishi
7. malalamiko - matamko ya kuonyesha kutopendezwa na yale uliyofanyiwa
8. potovu - -enye kuenda kinyume na maadili
9. mkurugenzi - mkuu wa idara kuu ya wizara, shirika au taasisi
10. ubaguzi - hali ya upendeleo katika kuwahudumia watu

**Mifano ya sentensi**:

1. Mwenyekiti wa mkutano ameondoka.
2. Tuliitikia mwito wa kuhudhuria kongamano la mwaka.
3. Ni dhahiri shahiri kuwa usawa wa kijinsia hauzingatiwi Afrika.
4. Unyanyapaa dhidi ya wanawake ni jambo baya.
5. Wanafunzi wa jinsia ya kike ni wengi kuliko wale wa kiume.
6. Mwalimu alituhimiza kuzingatia uakifishaji wakati wa kuandika hotuba.
7. Malalamiko ya wanawake yatasikilizwa na afisa mkuu.
8. Dhana kuwa wanawake ni dhaifu ni potovu.
9. Mkurugenzi wa shirika la kahawa atatuongelesha.
10. Ubaguzi wa rangi hufanyika sana Ulaya.

**Matumizi ya lugha (105)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili sifa za hotuba kwa kurejelea hotuba waliyosoma hapo awali kuhusu ushirikiano wa kijinsia. Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya darasa.*

**Kusilikiza na kuzungumza (106)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili athari za unyanyasaji wa kijinsia katika jamii na taifa zima kwa ujumla. Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya wanafunzi wenzao.*

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi wakati wa majadiliano yao. Wanaweza kutaja hoja kama vile:

1. Unyanyasaji wa kijinsia husababisha vita miongoni mwa wanajamii.
2. Huleta kutoelewana baina ya watu wanaohusika.
3. Huwafanya wanaonyanyaswa kukosa ari ya kushirikiana kikazi na wenzao.
4. Huathiri uchumi wa jamii.

**Kuandika (Zoezi la 2)**

*Kwa kazi binafsi, mwanafunzi atunge hotuba kuhusu umoja wa Wanyarwanda kwa kueleza shughuli kadhaa ambazo huchangia katika kuwepo kwa umoja huo miongoni mwa Wanywarwanda wote, wadogo kwa wakubwa. Kila kikundi kitoe hotuba yake mbele ya darasa.*

**Sarufi: Uambishaji wa vitenzi (Uk. 107 – 109)**

**Zoezi la 3**

1. Aliyonunuliwa

a) ‘a-’ ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu umoja

b) ‘-li-’ ni kiambishi cha wakati uliopita

c) ‘-yo-’ ni kiambishi kinachoashiria kitendwa

d) ‘-nunu-’ ni mzizi wa kitenzi
e) ‘-liw’ ni kiishio cha kauli ya kufanyiwa
f) ‘-a’ ni kimalizio

2. Alichimbua
a) ‘a-’ ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu, umoja
b) ‘-li-’ ni kiambishi cha wakati uliopita
c) ‘-chimb’ ni mzizi wa kitenzi
d) ‘-u-’ ni kiishio cha kauli ya kufanyua
e) ‘-a’ ni kimalizio

3. Unaniangalia
a) ‘u-’ ni kiambishi awali cha nafsi ya pili, umoja
b) ‘-na-’ ni kiambishi cha wakati uliopo
c) ‘-ni-’ ni kiambishi cha mtendewa
d) ‘-angali’ ni mzizi wa kitenzi
e) ‘-a’ ni kimalizio

4. Anafundisha
a) ‘a-’ ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu, umoja
b) ‘-na-’ ni kiambishi cha wakati uliopo
c) ‘-fundish’ ni mzizi wa kitenzi
d) ‘-a’ ni kimalizio

5. Aliwahutubia
a) ‘a-’ ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu, umoja
b) ‘-li-’ ni kiambishi cha wakati uliopita
c) ‘-wa-’ ni kiambishi cha watendewa
d) ‘-hutubi’ ni mzizi wa kitenzi
e) ‘-a’ ni kimalizio

6. Halijafunguliwa

a) ‘ha-’ ni kiambishi awali cha ngeli ya LI-YA

b) ‘-li-’ ni kiambishi cha ngeli ya Li - Ya

c) ‘-ja-’ ni kiambishi kikanushi

d) ‘-fungu’ ni mzizi wa kitenzi

e) ‘-liw-’ ni kimalizio cha kauli ya kufanyiwa

f) ‘-a’ ni kimalizio

7. Sitapiga

a) ‘si-’ ni kiambishi awali cha ukanusho wa nafsi ya kwanza, umoja

b) ‘-ta-’ ni kiambishi cha wakati ujao

c) ‘-pig’ ni mzizi wa kitenzi

d) ‘-a’ ni kimalizio

8. Hakijasomwa

a) ‘ha-’ ni kiambishi awali cha ukanusho wa nafsi ya tatu, umoja

b) ‘-ki-’ ni kiambishi cha ngeli ya KI-VI

c) ‘-ja-’ ni kiambishi cha ukanusho wa wakati uliotimilika

d) ‘-som’ ni mzizi wa kitenzi

e) ‘-w-’ ni kimalizio cha kauli ya kufanywa

f) ‘-a’ ni kimalizio

9. Anamwandikia

a) ‘a-’ ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu, umoja

b) ‘-na-’ ni kiambishi cha wakati uliopo

c) ‘-mw-’ ni kiambishi cha mtendewa

d) ‘-andik’ ni mzizi wa kitenzi

e) ‘-i-’ ni kimalizio cha kauli ya kufanyia

f) ‘-a’ ni kimalizio

10. Tutasafiri

a) ‘tu-’ ni kiambishi awali cha nafsi ya kwanza wingi
b) ‘-ta-’ ni kiambishi cha wakati ujao
c) ‘-safir’ ni mzizi wa kitenzi
d) ‘-i’ ni kimalizio

**Zoezi la 4 (Uk.108)**

*Katika jozi, wanafunzi watunge sentensi zenye vitenzi vilivyo na viambishi vilivyotolewa.*

**Mfano wa sentensi**

1. Mwalimu ananifundisha Hisabati.
2. Kalamu iliyonunuliwa imepotea.
3. Mama ataniletea mkate.
4. Nyinyi msinisumbue.
5. Chumbani humo mmefagiliwa.

## SOMO LA 3: DHANA YA UFUPISHO NA SIFA ZAKE

### i) Malengo ya ujifunzaji

Kujadili dhana ya ufupisho na sifa zake.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za ufupisho wa vifungu vya habari

- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Hati zilizorekodiwa
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

**Tanbihi:** Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenye matatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu:Hotuba kuhusu umuhimu wa maadili ( Uk. 115-118 )**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome kwa makini kifungu cha habari husika na kujibu maswali ya ufahamu yaliyotolewa. Hakikisha kuwa wanafunzi wameyagusia majibu kama ifuatavyo.*

1. Mwalimu mkuu wa shule, naibu wa mwalimu mkuu, wazazi, walimu na wanafunzi.
2. Mwalimu wa Kiswahili.
3. Kwa kuwa kumekuwa na visa vingi vya utovu wa maadili vinavyowahusu baadhi ya wanafunzi.
4. Heshima si utumwa. Methali hii inamaanisha kuwa heshima inastahili kutolewa kwa mtu yeyote yule bila ya kuwa na vizingiti vyovyote.
5. Kufukuzwa shuleni au kufungwa jela.
6. Walimu wamewasaidia wanafunzi kadri ya uwezo wao.
7. Wizi, ubakaji na matumizi ya dawa za kulevya.

8. Kuwa na heshima, kuwa, mnyenyekevu, kuwa mkweli, kuwa mwaminifu, kuwa na nidhamu, kuwa na bidii, kuwajibikia shughuli unazopewa, kumcha Mungu na kutumia lugha yenye heshima.
9. Ili kuwasaidia wazazi wao siku za usoni na pia kujiendeleza wenyewe.
10. Kuwa mvivu, kuwa na wivu, wizi, ubakaji, kutozingatia usafi, kutumia dawa za kulevya, kutumia lugha chafu iliyojaa matusi, ubakaji, kutozingatia usafi, kuwa na kiburi, kuzua vita, n.k.

**Matumizi ya msamiati**

***Zoezi la 1*(Uk.119)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zilizotolewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo.*

Majibu yaliyopendekezwa :

1. wamejitolea mhanga - wameamua kufanya jambo fulani kwa mioyo yao yote
2. wamejikaza kisabuni - wametia jitihada sana
3. utovu - ukosefu wa
4. kesi - mashtaka yaliyofikishwa mahakamani
5. hofu - hali ya kuhisi woga fulani
6. kupindukia - kupita kiasi
7. elimu - mafunzo yanayotolewa na jamii kwa watu wake
8. ubakaji - tendo la kumwingilia mwanamke au mwanamume kingono kwa lazima
9. uaminifu – tabia ya mtu kuaminika kwa kusema ukweli
10. wizi - tendo la kuchukua mali ya mtu mwingine bila idhini yake

Mfano wa sentensi:

1. Wazazi wamejitolea mhanga kutulipia karo ya shule.
2. Wanafunzi wa darasa letu wamejikaza kisabuni katika masomo yao.
3. Kuwatusi watu ni utovu wa nidhamu.
4. Uvutaji wa bangi ulimsababishia kesi mahakamani.

5. Nina hofu kuwa mtu yule ametoroka na pesa zangu.
6. Mwanafunzi aliyefukuzwa shuleni alikuwa amelewa kupindukia.
7. Kila binadamu anastahili elimu bora.
8. Mwendawazimu yule alishtakiwa kwa kosa la ubakaji.
9. Mwanafunzi bora alituzwa kwa uaminifu wake.
10. Matapeli wale walishtakiwa kwa wizi wa kimabavu.

**Matumizi ya msamiati (Uk.119)**

**Zoezi la 1**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi zilizotolewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo.*

**Maana ya msamiati :**

1. wamejitolea mhanga - wameamua kufanya jambo fulani kwa mioyo yao yote
2. wamejikaza kisabuni - wametia jitihada sana
3. utovu - ukosefu wa
4. kesi - mashtaka yaliyofikishwa mahakamani
5. hofu - hali ya kuhisi woga fulani
6. kupindukia - kupita kiasi
7. elimu - mafunzo yanayotolewa na jamii kwa watu wake
8. ubakaji - tendo la kumwingilia mwanamke au mwanamume kingono kwa lazima
9. uaminifu – tabia ya mtu kuaminika kwa kusema ukweli
10. wizi - tendo la kuchukua mali ya mtu mwingine bila idhini yake

**Mfano wa sentensi**:

1. Wazazi wamejitolea mhanga kutulipia karo ya shule.
2. Wanafunzi wa darasa letu wamejikaza kisabuni katika masomo yao.
3. Kuwatusi watu ni utovu wa nidhamu.

4. Uvutaji wa bangi ulimsababishia kesi mahakamani.
5. Nina hofu kuwa mtu yule ametoroka na pesa zangu.
6. Mwanafunzi aliyefukuzwa shuleni alikuwa amelewa kupindukia.
7. Kila binadamu anastahili elimu bora.
8. Mwendawazimu yule alishtakiwa kwa kosa la ubakaji.
9. Mwanafunzi bora alituzwa kwa uaminifu wake.
10. Matapeli wale walishtakiwa kwa wizi wa kimabavu

**Matumizi ya lugha (Uk.120)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili:*

*a) Maana ya ufupisho au muhtasari;*

*b) Sifa za ufupisho au muhtasari. Kila kikundi kiwasilishe hoja zake mbele ya darasa.*

Mfano wa jibu linalopendekezwa :

Muhtasari wa mambo muhimu katika taarifa fulani huitwa ufupisho.

Sifa za ufupisho:

- Huwa mfupi ukilinganishwa na taarifa asilia.
- Huhifadhi ujumbe wa taarifa asilia.
- Huandikwa kwa kuzingatia idadi ya maneno yanayotakikana.
- Viunganishi hutumika ili kupunguza idadi ya maneno.

**Zoezi la 2**

*Katika jozi, wanafunzi wafupishe hotuba waliyosoma hapo awali kuhusu maadili kwa kutumia maneno mia moja pekee (100) na kwa kuzingatia sifa za ufupisho. Kila kundi liwasilishe kazi yao mbele ya darasa.*

Mfano wa ufupisho wa hotuba husika :

Kutokana na visa vingi vya utovu wa maadili, mwalimu mkuu aliteua mada kuhusu maadili. Maadili ni mwenendo au tabia njema inayokubalika katika jamii. Huhusu kuwa na heshima, kuwa mnyenyekevu, mwaminifu na mkweli. Wanafunzi wanahimizwa kuwaheshimu watu wote;

wakubwa kwa wadogo. Mwanafunzi asiye na heshima huadhibiwa vikali. Mtu mwongo hana amani kwa kuwa ana hofu ya kugunduliwa. Kufuta alama kwenye karatasi za mitihani ni tabia ya uongo ambayo inafaa kukoma. Wanafunzi wanahimizwa kutia bidii masomoni kwa kuamka mapema na kudurusu ili waweze kufaulu na kuwasaidia wazazi wao siku za usoni. Wizi, ubakaji na matumizi ya dawa za kulevya huweza kusababisha mtu kufungwa jela au kufukuzwa shuleni. Kuzua vita na kuwanyanyasa wanafunzi wengine zimetengewa adhabu kali zaidi. Wanafunzi wanahimizwa kutambua kuwa hakuna mwanafunzi aliye bora zaidi kuliko mwingine. Mwisho, wanafunzi wanahimizwa kujenga msingi bora wa maisha yao na kutia bidii masomoni.

**Kusikiliza na kuzungumza (uk. 120)**

*Kwa kazi binafsi: Tunga hotuba kuhusu 'Umuhimu wa mbuga za wanyamapori nchini Rwanda'.*

- Kila mwanafunzi ahutubie darasa hotuba yake.

**Kuandika (Uk.120)**

*Fupisha hotuba hiyo kwa kutumia maneno mia moja pekee (100). Kwa kutathmini kazi hii, mwalimu azingatie idadi ya maneno iliyoagizwa pamoja na sifa za ufupisho.*

**Sarufi: Uundaji wa nomino kutokana na vitenzi(Uk. 121 - 122)**

**Zoezi la 3**

*Kwa kazi binafsi, mwanafunzi aunde nomino kutokana na vitenzi alivyopewa. Mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa majina yafuatayo :*

1. jadili - mjadala, majadiliano, kujadili
2. adhibu - mwadhibu, adhabu, kuadhibu
3. samehe – msamaha, kusamehe
4. lima - ukulima, mkulima, kulima

5. vua - uvuvi, mvuvi, kuvua
6. andika - mwandishi, maandishi, mwandiko, kuandika
7. kunywa - mnywaji, unywaji, kinywaji
8. kimbia - mkimbiaji, ukimbiaji, mbio, kukimbia
9. pika - mpishi, upishi, kupika
10. chora - mchoraji, uchoraji, kuchora, mchoro

**Zoezi la 3**

*Katika jozi, wanafunzi waunde nomino moja kwa kila kitenzi husika kisha watunge sentensi sahihi kwa kila nomino iliyoundwa. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamefaulu kupata nomino sahihi.*

**Mfano:**

1. okoa - mwokozi, uokoaji.
- Mwokozi ametusamehe dhambi zetu zote.
2. hariri - mhariri, uhariri
- Mhariri alikifanyia kitabu cha riwaya uhariri.
3. okota - uokotaji, mwokotaji
- Uokotaji wa takataka jijini unasafisha eneo hilo.
4. osha - mwosha, uoshaji
- Mwosha amekamilisha kazi yake mapema.
5. penzi - mpenzi, mapenzi

Mapenzi ambayo Mary alipewa na mpenzi wake yalimfurahisha.

**SOMO LA 4: MBINU ZA UFUPISHO**

**i) Malengo ya ujifunzaji**

Kufupisha habari kwa kuzingatia mbinu za ufupisho.

**ii) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za ufupisho wa vifungu vya habari
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu mahiri
- Ubao, chaki
- Hati zilizorekodiwa
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

**Tanbihi:** Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenye matatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu:Hotuba kuhusu manufaa ya elimu( Uk. 123-125 )**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome kwa makini kifungu cha habari husika na kujibu maswali ya ufahamu yaliyotolewa. Hakikisha kuwa wanafunzi wameyagusia majibu kama ifuatavyo.*

1. Waziri wa elimu, afisa wa elimu wa Mkoa wa Kusini, wasimamizi wa shule mbalimbali, walimu wakuu wa shule mbalimbali, wananchi, wanafunzi, mabibi na mabwana.
2. Kujitambulisha, kuwatambua waliohudhuria pamoja na kutaja mada ya hotuba.
3. Elimu ya gumbaru ni mafundisho ya kimsingi yanayotolewa kwa watu waliopitisha umri wa kuwa shuleni.

4. Kila kitu katika ulimwengu wa sasa hufanyika kwa kuandika na kusoma. Kwa mfano: kusoma taarifa za magazeti, kusoma vitabu, maelezo ya bidhaa dukani kutumia teknolojia n.k.
5. Wafanyabiashara huweza kuendeleza shughuli zao kwa urahisi. Miradi huweza kudhibitiwa kwa urahisi pamoja na kuihusisha na teknolojia. Maarifa na namna ya kuepuka kupata hasara hupatikana kupitia elimu.
6. Wahalifu huwakosesha wananchi amani na kuwa kero kubwa kwa jamii.
7. Elimu imewasaidia wafanyabiashara kuendesha mitambo na mashine mbalimbali ambazo husaidia kurahisisha shughuli za kibiashara.
8. Ajira humwezesha mtu kupata mshahara wa kujikimu kimaisha kwa kupata chakula, mavazi na mahali pa kuishi. Elimu huwezesha nchi kupata wataalamu kama vile: madaktari, makarani, manahodha n.k.
9. Mtu asiyeelimika hana uwezo wa kusoma na kuandika na hivyo, mawasiliano na watu wengine hutatizika. Mtu huyu hupata ugumu wa kushiriki katika biashara na kufaulu kwa sababu ya matatizo ya kuwasiliana na wateja na wauzaji na pia kutodhibiti hesabu zake. Huwa vigumu kwa mtu huyu kupata ajira hasa zinazohitaji maarifa maalumu. Watu hawa huishia kuwa maskini na wengine hujiingiza katika uhalifu na kuwaathiri wananchi wengine.
10. Kwa kuwahimiza watu wote kufahamu kuwa elimu ina manufaa mengi, kuwahimiza watu wote kupata elimu na pia kuwashukuru wote waliohudhuria mkutano

**Matumizi ya msamiati (Uk. 126)**

**Zoezi la 1**

*Kwa kutumia mbinu ya fikiri – jozi - shiriki, wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi husika kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo. Matumizi ya kamusi ya Kiswahili sanifu unakubaliwa.*

Majibu yaliyopendekezwa :

1. jazila - nyingi
2. Rabana - Mungu

3. masimulizi - maelezo yanayotolewa kama hadithi
4. tusife moyo - tusikate tamaa
5. anahisi - anapata fahamu kupitia viungo vyake kama vile: masikio, pua.
6. mshahara - malipo anayopata mtu mwishoni mwa mwezi baada ya kufanya kazi fulani
7. ajira - kazi ya kulipwa mshahara
8. wahandisi - watu wenye elimu na ujuzi wa kuhudumia mitambo, majengo na madaraja
9. waashi - mafundi wa kujenga nyumba kwa mawe au matofali
10. marubani - watu wenye ujuzi wa kuongoza ndege angani

**Mfano wa sentensi :**

1. Mzungumzaji alitupa shukrani jazila kwa kuwa makini mkutanoni.
2. Tusisahau kumwomba Rabana kila siku.
3. Masimulizi ya bibi hutufurahisha.
4. Afisa wa elimu alituambia tusife moyo katika juhudi zetu za kila siku.
5. Mgonjwa anahisi maumivu kwenye tumbo.
6. Nitautumia mshahara wangu wa mwezi huu kununua runinga.
7. Maria amepata ajira ya kuwa karani wa wizara.
8. Tulifanya mkutano na wahandisi wawili pekee.
9. Hospitali kuu ya mkoa imejengwa na waashi maarufu.
10. Ndege zitakazowasafirisha wanajeshi zitakuwa na marubani wawili wawili.

**Matumizi ya lugha (Uk. 126)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili mwongozo wa kuandika ufupisho. Katika uwasilishaji wao, mwalimu awaongoze kwenye taratibu zifuatazo:*

Taratibu za kuandika ufupisho:

1. Soma taarifa uliyopewa kwa mfululizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.
2. Soma taarifa hiyo kwa mara ya pili huku ukidondoa hoja muhimu na kuziandika.
3. Chunguza iwapo kuna hoja ambazo zimesahaulika katika taarifa asilia.

4. Unganisha hoja zako kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.
5. Soma hoja ulizounganisha kuhakikisha zina mtiririko mzuri.
6. Hariri makala yako kuondoa makosa ya kisarufi.
7. Zingatia idadi ya maneno yanayostahili.

**Kuandika: Zoezi la 2 (Uk.127)**

*Kwa kazi binafsi, wanafunzi wasome tena hotuba kuhusu manufaa ya elimu kisha waifupishe kwa kutumia maneno mia moja pekee (100). Mwalimu ahakikishe kuwa mwongozo wa kuandika ufupisho umezingatiwa.*

Mfano wa ufupisho wa ‘Manufaa ya elimu’.

Elimu ni mafunzo ambayo hutolewa na jamii kwa watu wake, darasani au mahali pasipokuwa darasani. Enzi za mababu zetu, maarifa yalipitishwa kupitia masimulizi ya hadithi, vitendawili na misemo. Elimu humpa mtu uwezo wa kusoma na kuandika. Ni himizo kwa kila mtu kupata elimu hata wale waliopitisha umri wa kuwa shuleni wanahimizwa kuhudhuria kupitia mradi wa elimu ya gumbaru. Elimu pia humwezesha aliyeelimika kupata ajira ambayo humwezesha kupata mshahara wa kujikimu kimaisha. Shughuli za kibiashara huboreshwa na elimu kwani wafanyabiashara huweza kuendeleza biashara zao kwa urahisi na kuendesha mitambo au mashine mbalimbali ambazo husaidia kurahisisha shughuli za biashara. Elimu huwapa waandishi na watunzi maarifa ya kuandika tungo kama vile: riwaya, tamthilia na hadithi fupi, wakulima pia hupata maarifa ya kuendesha ukulima wao na pia uhusiano wetu na watu wa mataifa mengine huboreshwa. Madhara ya kutoelimika ni pamoja na: mtu asiyeelimika kukosa uwezo wa kusoma na kuandika, kupata ugumu katika kushiriki biashara, kukosa ajira na kuishia kuwa maskini wa kuombaomba kisha kujiingiza katika uhalifu. Ni himizo kwa wote kuwa elimu ina manufaa mengi.

**Kusililiza na kuzungumza (Uk.127)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi: a) watunge hotuba kuhusu mada yoyote wanayochagua wao wenyewe ; b) wafupishe hotuba hiyo kwa kutumia maneno themanini tu (80). Kila kikundi kiwasilishe mbele ya wanafunzi wenzao hotuba waliyotunga pamoja na ufupisho wake.*

Mwalimu atathmini hotuba ambazo wanafunzi wameandika pamoja na ufupisho wa hotuba zenyewe. Ahakikishe kuwa wamezingatia mambo muhimu katika uandishi wa hotuba pamoja na ufupisho.

**Sarufi: Uundaji wa vitenzi jina(Uk. 127-128)**

**Zoezi la 3**

*Katika jozi, wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia nomino za vitenzi-jina zilizotolewa. Mwalimu atathmini usahihi wa sentensi zilizotungwa.*

Mfano wa sentensi :

1. Kuchonga vinyago kwake hunifurahisha.
2. Kusafisha kwa mama huleta harufu nzuri.
3. Kulima kwa mkulima huyu ni kwa manufaa.
4. Kufuga kwake mifugo kumemsaidia sana.
5. Kukimbia kwa Gasimba kumemletea mali nyingi.
6. Kusali kwetu kumetuondolea balaa.
7. Kushona kwa fundi huyu hunipendeza.
8. Kutembea kwa wakimbizi kunashtua.
9. Kulala kwa mtoto mchanga ni kwa manufaa kwake.
10. Kula kwetu hapa ni muhimu.

## 3.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 3.5.1 Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi

***Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi ni maelezo ambayo yameandaliwa kuongezea au kukamilisha yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima yazingatiwe katika ufundishaji wa mada hii.***

☞ **Somo la 12 : Sifa za hotuba**

**Matumizi ya lugha (Uk.105)**

**a) Hotuba ni nini ?**

Insha ya hotuba ni insha ambayo hutoa maneno halisi ya mzungumzaji/hatibu/kiongozi anapozungumzia hadhira, kuhusu jambo fulani. Insha ya hotuba huandikwa katika hali ya usemi halisi na mwandishi hatakiwi kuweka alama za kunukuu anapoanza insha yake.

Hotuba inaweza kutolewa na kiongozi wa kisiasa, utawala, kidini, kikundi, shirika fulani, daktari, n.k. Hadhira katika hotuba husheheni wageni waalikwa, wanachama, wafuasi, wananchi, n.k ambao wanahusishwa katika mada inayorejelewa katika hotuba hiyo. Mengi ya maswala yanayojitokeza katika insha za hotuba ni maswala ibuka katika jamii k.v upangaji wa uzazi, usalama, n.k

**b) Muundo wa Hotuba**

**1. Anwani**

Anwani, mada au kichwa cha hotuba huchukua herejelea hatibu pamoja na mada ya hotuba. Pia mada inaweza kutaja hadhira.

Hotuba ya Waziri wa Afya kuhusu madhara ya ukimwi kwa wananchi.

Hotuba ya Mwalimu Mkuu kwa Wazazi

2. **Utangulizi**

- Anza hotuba yako kwa kuwatambua waliohudhuria mkutano (hadhira).
- Wataje kwa majina/vyeo vyao kuanzia yule wa cheo cha juu hadi wa chini, mabibi na mabwana (Kumbuka kwamba huhitajiki kuwasalimia. Kuwatambua kwa majina pekee kunatosha)
- Jitambulishe kwa hadhira yako hasa ikiwa unazungumzia hadhira isiyokujua au wageni.
- Tanguliza mada yako.

3. **Mwili**

Hakikisha kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho

Ujumbe wako wote unapaswa kuwa katika usemi halisia wala si wa taarifa.

4. **Tamati**

- Hakikisha kwamba mwisho wa hotuba yako unatambulika.
- Unaweza kumaliza kwa shukurani

c) **Sifa za hotuba:**

- Aya ya kwanza huwa utangulizi na hutambulisha kitakachozungumziwa, salamu na msemaji.
- Aya kadhaa zinazofuata utangulizi huhusu ujumbe wa hotuba nzima.
- Hotuba huandikwa katika nafsi ya kwanza na huwa katika usemi asili.
- Hotuba huandikwa katika wakati uliopo.
- Aya ya mwisho huhitimisha hotuba kwa kutoa shukrani na kuwaaga wasikilizaji.

### 3.5.2 Maelekezo ya ziada kwa mwalimu

***Maekelekezo haya yamependekezwa kwa sababu tofauti. Kwanza, yameandaliwa kwa ajili ya kukamilisha au kuimarisha kazi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Pili, yamefikiriwa kwa madhumuni ya kubadilisha kazi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi ambazo zimetathminiwa kutofaa katika nafasi zilimowekwa. Kwa hiyo, ni sharti kwa mwalimu kuchagua kazi anayoiona kuwa ya lazima au muhimu baadhi ya kazi zilizopendekezwa ama katika kitabu cha mwanafunzi au katika kitabu hiki cha mwalimu.***

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.98)**

*Wanafunzi wasikilize hotuba iliyorekodiwa na kuitolea muhtasari kimazungumzo. Mwalimu achague hotuba iliyorekodiwa na kuwashirikisha wanafunzi kwenye kazi ya kusikiliza na kuzungumza.*

**Matumizi ya lugha (Uk.105)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi watoe :*

*a. maana ya hotuba*

*b. muundo wa hotuba*

*c. sifa za hotuba*

Majibu yanayopendekezwa :

**a) Maana ya hotuba**

Insha ya hotuba ni insha ambayo hutoa maneno halisi ya mzungumzaji/hatibu/kiongozi anapozungumzia hadhira, kuhusu jambo fulani. Insha ya hotuba huandikwa katika hali ya usemi halisi na mwandishi hatakiwi kuweka alama za kunukuu anapoanza insha yake.

Hotuba inaweza kutolewa na kiongozi wa kisiasa, utawala, kidini, kikundi, shirika fulani, daktari, n.k. Hadhira katika hotuba husheheni wageni waalikwa, wanachama, wafuasi, wananchi, n.k ambao wanahusishwa katika mada inayorejelewa katika hotuba hiyo. Mengi ya maswala yanayojitokeza katika insha za hotuba ni maswala ibuka katika jamii k.v upangaji wa uzazi, usalama, n.k

**b) Muundo wa Hotuba**

**1. Anwani**

Anwani, mada au kichwa cha hotuba huchukua herejelea hatibu pamoja na mada ya hotuba. Pia mada inaweza kutaja hadhira.

Mifano:

- Hotuba ya Waziri wa Afya kuhusu madhara ya ukimwi kwa wananchi.
- Hotuba ya Mwalimu Mkuu kwa Wazazi

**2. Utangulizi**

- Anza hotuba yako kwa kuwatambua waliohudhuria mkutano (hadhira).
- Wataje kwa majina/vyeo vyao kuanzia yule wa cheo cha juu hadi wa chini, mabibi na mabwana.
- Kumbuka kwamba huhitajiki kuwasalimia. Kuwatambua kwa majina pekee kunatosha.
- Jitambulishe kwa hadhira yako hasa ikiwa unazungumzia hadhira isiyokujua au wageni.
- Tanguliza mada yako.

**3. Mwili**

- Hakikisha kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho
- Ujumbe wako wote unapaswa kuwa katika usemi halisia wala si wa taarifa.

**4. Tamati**

- Hakikisha kwamba mwisho wa hotuba yako unatambulika.
- Unaweza kumaliza kwa shukurani

**c) Sifa za hotuba:**

- Aya ya kwanza huwa utangulizi na hutambulisha kitakachozungumziwa, salamu na msemaji.
- Aya kadhaa zinazofuata utangulizi huhusu ujumbe wa hotuba nzima.
- Hotuba huandikwa katika nafsi ya kwanza na huwa katika usemi asili.
- Hotuba huandikwa katika wakati uliopo.
- Aya ya mwisho huhitimisha hotuba kwa kutoa shukrani na kuwaaga wasikilizaji.

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.106)**

1. *Darasani, wanafunzi wasikilize hotuba iliyorekodiwa, watoe muhtasari wake pamoja na ujumbe unaolengwa katika hotuba hiyo.*

2. *Wanafunzi wachaguliwe hotuba fulani na kushirikishwa kwenye uchambuzi wa hotuba hiyo kwa kuzingatia muundo na sifa zake.*

Inambidi mwalimu kuandaa vifaa husika ili utekelezaji wa kazi hizi mbili urahisishwe.

**Zoezi la kuandika (Uk.106)**

*'Umealikwa kuwahutubia wanafunzi wa shule ya msingi uliyosomea kuhusu umuhimu adabu kwa mwanafunzi'. Andika hotuba utakayotoa. Mwalimu ahakikishe kuwa muundo wa hotuba umezingatiwa.*

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk. 120)**

*Chagua hotuba moja iliyorekodiwa au iliyoandikwa ili kusomewa wanafunzi. Katika makundi madogomadogo, wanafunzi watoe kimazungumzo muhtasari au ufupisho wa hotuba hiyo.*

**Kusililiza na kuzungumza (Uk.127)**

*Chagua ufupisho wa hotuba moja iliyorekodiwa au iliyoandikwa ili kusomewa wanafunzi. Kwa kazi binafsi, mwanafunzi airudie hotuba hiyo kwa kuisimulia katika maneno yake binafsi.*

## 3.6 TATHMINI YA MADA YA MADA YA TATU

*Tathmini hii ipendekezwe kuwa jaribio la jumla. Kwa kazi binafsi, kila mwanafunzi anapaswa kujibu maswali yote yaliyopendekezwa na mwalimu kwa kutumia karatasi. Inambidi mwalimu kuyaanda majibu awali pamoja na vipimo vya tathmini kwa kila jibu.*

**Tanbihi:** Mwalimu halazimishwi kutoa kwa wanafunzi jumla ya maswali yote yaliyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi. Inambidi awe huru katika kuchagua maswali anayoona kuwa ni muhimu kuliko mengine. Ni haki kwake kutunga maswali yake bila kutegemea haya yaliyoandaliwa katika kitabu cha mwanafunzi.

Yafuatayo ni majibu yaliyopendekezwa kurejelewa:

**Zoezi la kuandika, uk. 129**

*Mwalimu awe huru katika tathmini ya kazi hii. Jambo muhimu la kuzingatia ni mwongozo wa kutunga hotuba na sifa zake.*

**Zoezi la 1, uk. 129**

a. unguza

b. tembelewa
c. lilia

**Zoezi la 2, uk. 129**

a. - lim
b. -kuj
c. -end
d. -tuli
e. -on

**Zoezi la 3, uk. 129**

1.

a) uvuvi, mvuvi, kuvua
b) upanzi, mpanzi, kupanda
c) upishi, mapishi, mpishi, kupika
d) utabibu, tabibu, kutibu
e) uchungaji, mchungaji, kuchunga

2. Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe nomino walizounda hapo juu.

Kwa mfano:

a) Uvuvi wa mvuvi huyu humletea pesa nyingi.
b) Huu ni msimu wa upanzi humu nchini.
c) Mpishi wa shule yetu ameondoka.
d) Utabibu unahitaji umakini.
e) Mchungaji wa kondoo wetu ana jipu kifuani.

**Zoezi la 2 la kuandika, uk.129**

Mwalimu atathmini hotuba ambazo wanafunzi wataandika na kuwasomea wanafunzi wenzao katika sherehe za siku ya wazazi shuleni mwao.

**Zoezi la 4, uk. 130**

| Kitenzi (kauli ya kufanya | Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendeka | Kauli ya kutendesha | Kauli ya kutendewa |
|---|---|---|---|---|
| Shona | Shonea | shoneka | shonesha | shonewa |
| Andika | Andikia | andikika | andikisha | andikiwa |
| Ona | Onea | oneka | onekesha | onewa |
| Pika | Pikia | pikika | pikisha | pikiwa |
| Onja | Onjea | onjeka | onjesha | onjewa |
| Tembea | Tembelea | tembeleka | tembeleza | tembelewa |

**Zoezi la 5, uk.130**

1. a+me+nyw+esh-w+a

- ‘-a-’ ni kiambishi ngeli
- ‘-me-’ ni kiambishi cha wakati uliotimilika
- ‘-nyw-’ ni mzizi wa kitenzi
- ‘-esh-’ ni kiambishi cha mnyambuliko
- ‘-w-’ ni kiambishi cha mnyambuliko
- ‘-a-’ ni kiishio

2. u+me+m+kasiri+sh+a

- ‘-u-’ ni kiambishi cha nafsi
- ‘-me-’ ni kiambishi cha wakati uliotimilika
- ‘-m-’ ni kiambishi cha mtendewa
- ‘-kasiri-’ ni mzizi wa kitenzi
- ‘-sh-’ ni kiambishi cha mnyambuliko
- ‘-a-’ ni kiishio

3. tu+ta+palili+a

- ‘tu-’ ni kiambishi cha nafsi
- ‘-ta-’ ni kiambishi cha wakati ujao
- ‘-palili-’ ni mzizi wa kitenzi
- ‘-a’ ni kiishio

4. wa+li+zur+u

- ‘wa-’ ni kiambishi ngeli
- ‘-li-’ ni kiambishi cha wakati uliopita
- ‘-zur-’ ni mzizi wa kitenzi
- ‘-u-’ ni kiishio kitenzi

5. wa+na+shereheke+a

- ‘-wa-’ ni kiambishi cha nafsi
- ‘-na-’ ni kiambishi cha wakati uliopo
- ‘-shereheke-’ ni mzizi wa kitenzi
- ‘-a’ ni kiishio

**Zoezi la 6, uk. 130**

*Utungaji wa sentensi ni wa kibinafsi. Kwa hiyo, mwalimu asisitizie maana ya sentensi kutokana na kauli ya vitenzi iliyotumiwa:*

**Kwa mfano:**

1. Mama anamnywesha mtoto dawa.
2. Mwalimu alimketisha mwanafunzi kitini.
3. Shangazi amejishughulisha na kazi za pale nyumbani.
4. Nilimwandikisha barua kwa chifu.
5. Mwalimu alimsomesha mwanafunzi yule.

### 3.7. KAZI ZA ZIADA ZA UJIFUNZAJI

***Kazi hizi zimegawanyika katika sehemu tatu: Kwanza, kuna kazi za urekebishaji ambazo zimewalenga wanafunzi wasioelewa haraka katika ujifunzaji wao; pili, kazi za uimarishaji wa***

***uwezo wa mada kwa ujumla; tatu, kazi zinazopendekezwa kwa wanafunsi wenye uelewa wa haraka.***

### 3.7.1. Kazi za urekebishaji

1. Eleza maana ya hotuba
2. Jadili sehemu kuu za hotuba
3. Jadili taratibu za ufupisho wa habari
4. Anapenda. Ambisha kitenzi hiki na kueleza viambishi vyake.

**Majibu**

1. Insha ya hotuba ni insha ambayo hutoa maneno halisi ya mzungumzaji/hatibu/kiongozi anapozungumzia hadhira, kuhusu jambo fulani. Insha ya hotuba huandikwa katika hali ya usemi halisi na mwandishi hatakiwi kuweka alama za kunukuu anapoanza insha yake.

   Hotuba inaweza kutolewa na kiongozi wa kisiasa, utawala, kidini, kikundi, shirika fulani, daktari, n.k. Hadhira katika hotuba husheheni wageni waalikwa, wanachama, wafuasi, wananchi, n.k ambao wanahusishwa katika mada inayorejelewa katika hotuba hiyo. Mengi ya maswala yanayojitokeza katika insha za hotuba ni maswala ibuka katika jamii k.v upangaji wa uzazi, usalama, n.k
2. Sehemu za hotuba

a) Anwani

Anwani, mada au kichwa cha hotuba huchukua herejelea hatibu pamoja na mada ya hotuba. Pia mada inaweza kutaja hadhira. Mifano:

- Hotuba ya Waziri wa Afya kuhusu madhara ya ukimwi kwa wananchi.
- Hotuba ya Mwalimu Mkuu kwa Wazazi

b) Utangulizi

- Anza hotuba yako kwa kuwatambua waliohudhuria mkutano (hadhira).
- Wataje kwa majina/vyeo vyao kuanzia yule wa cheo cha juu hadi wa chini, mabibi na mabwana.
- Kumbuka kwamba hauhitajiki kuwasalimia. Kuwatambua kwa majina pekee kunatosha.
- Jitambulishe kwa hadhira yako hasa ikiwa unazungumzia hadhira isiyokujua au wageni.
- Tanguliza mada yako.

c) Mwili

- Hakikisha kuna mtiririko wa hoja kuanzia mwanzo hadi mwisho

- Ujumbe wako wote unapaswa kuwa katika usemi halisia wala si wa taarifa.

d) Tamati

- Hakikisha kwamba mwisho wa hotuba yako unatambulika.
- Unaweza kumaliza kwa shukurani

3. Taratibu za ufupisho

a. Soma taarifa uliyopewa kwa mfululizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.
b. Soma taarifa hiyo kwa mara ya pili huku ukidondoa hoja muhimu na kuziandika.
c. Chunguza iwapo kuna hoja ambazo zimesahaulika katika taarifa asilia.
d. Unganisha hoja zako kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.
e. Soma hoja ulizounganisha kuhakikisha zina mtiririko mzuri.
f. Hariri makala yako kuondoa makosa ya kisarufi.
g. Zingatia idadi ya maneno yanayostahili.

4. anapenda = a+na+pend+a

'a' ni kiambishi cha nafsi ya tatu umoja (yeye)

'na' ni kiambishi cha wakati uliopo

'pend' ni mzizi wa kitenzi

'penda' 'a' ni kimalizio cha kitenzi 'penda'

**3.7.2.Kazi za uimarishaji**

**Maswali :**

1. Bainisha marika ya watu mbalimbali wanaoweza kutoa hotuba kwa hadhira pamoja na mada zinazoweza kuzungumziwa.
2. Jadili umuhimu wa ufupisho
3. Unda majina mawili mawili kutokana na vitenzi vifuatavyo: kula, kulea, kufa, kulia

**Majibu:**

1. Hotuba inaweza kutolewa na kiongozi wa kisiasa, utawala, kidini, kikundi, shirika fulani, daktari, n.k. Mada zinazoweza kuzungumziwa huhusu maswala ibuka katika jamii k.v upangaji wa uzazi, usalama, uchumi, usafi, elimu, siasa, itikadi, n.k.

2. Umuhimu wa ufupisho:

- Baadhi ya madhumuni muhimu ya kufundisha muhtasari ni: kuwawezesha wanafunzi kuelewa makala au taarifa iliyotolewa, kisha kuteua kilicho muhimu ili kuwasilisha ujumbe wa makala au taarifa hiyo kwa ufupi na kwa njia inayoeleweka.

- Lengo kuu hasa ni kuwapa wanafunzi ustadi utakaowawezesha kukabiliana na majukumu yatakayohitaji ufupishaji katika maisha yao, kwa mfano: ufupishaji wa makala, barua za ofisini na uandishi wa matangazo.

3. Uundaji wa majina kutoka kitenzi

a) kula: mlo, mlafi
b) kulea : malezi, mlezi
c) kufa : kifo, mfiwa
d) kulia : mlio, kilio

### 3.7.3. Kazi kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

*“Ninafuraha kujumuika nanyi leo katika kile kitakachoingia katika historia kama maandamano makubwa zaidi ya uhuru katika historia ya taifa letu. Miaka mitano iliyopita, Mmarekani mkuu, ambaye katika kivuli chake cha mfano tunasimama leo, alitia saini Tangazo la Ukombozi. Amri hii muhimu ilikuja kama mwanga mkuu wa tumaini kwa mamilioni ya watumwa wa Negro ambao walikuwa wameteketezwa kwa moto wa ukosefu wa haki unaonyauka. Ilikuja kama mapambazuko ya furaha kumaliza usiku mrefu wa utumwa.*

*Lakini miaka mia moja baadaye, Negro bado sio bure. Miaka mia moja baadaye, maisha ya Weusi bado yamelemazwa kwa huzuni na kanuni za ubaguzi na minyororo ya ubaguzi. Miaka mia moja baadaye, Weusi wanaishi kwenye kisiwa cha upweke cha umaskini katikati ya bahari kubwa ya ustawi wa mali. Miaka mia moja baadaye, Negro bado amedhoofika katika pembe za jamii ya Amerika na anajikuta uhamishoni katika ardhi yake mwenyewe…”*

Dondoo la hotuba hapo juu linakukumbusha nini katika historia ya dunia?

**Jibu:**

Hili ni dondoo kutoka hotuba"Nina Ndoto" ambayo ilitolewa na mwanaharakati wa haki za kiraia wa Marekani Martin Luther King Jr. wakati wa Machi juu ya Washington kwa Ajira na Uhuru mnamo Agosti 28, 1963, ambapo alitoa wito wa haki za kiraia na kiuchumi na mwisho. kwa ubaguzi wa rangi nchini Marekani. Ikiwasilishwa kwa zaidi ya wafuasi 250,000 wa haki za kiraia kutoka hatua za Ukumbusho wa Lincoln huko Washington, DC, hotuba hiyo ilikuwa wakati wa kubainisha vuguvugu la haki za kiraia na miongoni mwa hotuba muhimu zaidi katika historia ya Marekani.

Kuanzia na kurejelea Tangazo la Ukombozi, ambalo liliweka huru mamilioni ya watumwa mnamo 1863, King alisema "miaka mia moja baadaye, Negro bado sio huru". Kufikia mwisho wa hotuba, King alitoka kwenye maandishi yake aliyotayarisha kwa upotoshaji ulioboreshwa kwa sehemu juu ya mada "Nina ndoto", iliyochochewa na kilio cha Mahalia Jackson: "Waambie kuhusu ndoto, Martin!"

Katika sehemu hii ya hotuba iliyosisimua zaidi wasikilizaji na sasa imekuwa maarufu zaidi, Mfalme alielezea ndoto zake za uhuru na usawa unaotokana na nchi ya utumwa na chuki. Kwa kifungu kimoja cha maneno, Martin Luther King Jr. alijiunga na Jefferson na Lincoln katika safu ya wanaume ambao wameunda Amerika ya kisasa.

## MADA KUU YA 4 : UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAZUNGUMZO

## MADA NDOGO YA 4: MDAHALO NA MJADALA

### 4.1. Uwezo upatikanao katika mada

Kuandaa midahalo na mijadala kwa kuzungumza kwa ufasaha; Kuambisha maneno katika Kiswahili.

### 4.2. Ujuzi wa awali

Midahalo na mijadala si dhana mpya kwa wanafunzi wa kidato cha sita. Ukweli huu unadhibitishwa na mada ya nne ‘Mdahalo na Mjadala’ katika kidato cha nne.

### 4.3. Kidokezo

#### 4.3.1. Kidokezo cha mada na maelekezo yake

Mwalimu awaulize wanafunzi swali lifuatalo:

Fikiria majadiliano yaliyotokea siku moja kati ya pande mbili. Kundi la kwanza lilitetea maoni yake na jingine vilevile. Pande hizi huaitwaje? Majadiliano yao huitwaje?

#### 4.3.2. Maelekezo ya kidokezo cha mada

Mwalimu achague kimakusudi kauli na kuiandika ubaoni. Kwa mfano, “pesa huleta amani katika jamii.” Baadaye,mwalimu awaulize ni wanafunzi wepi wanaokubaliana na kauli hii na ni wepi wasiokubaliana nayo. Hivyo kila kundi litetee msimamo wake.

### 4.4. Orodha ya masomo

| | **Kichwa cha somo** | **Malengo ya kujifunza (Maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema)** | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|---|
| **1** | Dhana ya mdahalo na mwongozo wake | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya mdahalo na umuhimu wake katika ujifunzaji wa lugha; Kubainisha taratibu za uandaaji wa mdahalo<br>**Stadi:** Kujadili dhana ya mdahalo na mwongozo wake; Kuandaa mdahalo kwa kuzingatia taratibu zake..<br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kukuza tabia ya kujadiliana na wengine | 22 |
| **2** | Dhana ya mjadala na mwongozo wake | **Maarifa na ufahamu:** Kueleza dhana ya mjadala na umuhimu wake katika ujifunzaji wa lugha; Kubainisha taratibu za kuandaa na mjadala | 22 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | **Stadi** : Kujadili dhana ya mjadala na mwongozo wake; Kuandaa mjadala kwa kuzingatia taratibu zake.<br><br>**Maadili na mwenendo mwema**: Kuonesha moyo wa heshima kwa maoni ya washiriki wengine, ushirikiano na uajibikaji. | |
| **-** | Sarufi: Uambishaji wa maneno katika Kiswahili | **Maarifa na ufahamu:** Kutambua viambishi muhimu katika uambishaji wa maneno katika Kiswahili.<br><br>**Stadi :** Kuambisha aina za maneno katika Kiswahili.<br>**Maadili na mwenendo mwema:** Kuendeleza maarifa ya ubuniaji wa msamiati wa lugha. | **-** |
| **Tathmini ya mada** | | | **2** |
| **Jumla ya vipindi vya mada ya kwanza:** | | | **46** |

**Maelekezo kuhusu uandaaji wa masomo yaliyoonyeshwa hapo juu:**

- **Vipengele vya muundo wa somo**

Kila somo hujengwa na vipengele vifuatavyo:

1. Kusoma na ufahamu vifungu vya habari
2. Msamiati kuhusu vifungu vya habari vilivyosomwa
3. Matumizi ya lugha
4. Kusikiliza na kuzungumza

5. Sarufi

6. Kuandika

- **Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila kipengele cha somo:**

**(a) Kusoma na ufahamu kifungu cha habari**

- **Kusoma:** Kwa kutegemea kitabu cha mwanafunzi au nakala ya vifungu vya habari, wanafunzi washirikishwe kwenye kazi ya kusoma kifungu husika kwa njia tofauti: kusoma kimya au kusoma kwa sauti. Mwalimu ashirikishe wanafunzi wote kwenye kazi hii kwa kutumia njia moja au nyingine. Ili kurahisisha kazi hii na kufaulu kuwashirikisha wanafunzi wote, kazi hii huweza kufanyika katika makundi madogomadogo au katika jozi.
- **Ufahamu:** Ufahamu wa kifungu cha habari huweza kufikiwa kwa njia nyingi kama vile kufasiri michoro au picha zilizotumiwa katika kifungu cha habari husika; kuuliza maswali ya ufahamu, kutoa dhamira kuu zilizosisitiziwa katika kifungu cha habari, kutoa muhtasari wa habari iliyozungumziwa, n.k. Kwa hiyo, inambidi mwalimu achagua njia moja au zaidi baadhi ya hizi au nyingine ambayo haikutajwa hapa juu.

**(b) Matumizi ya msamiati**

Katika kipengele hiki, mwalimu anastahili kujenga kwa wanafunzi tafakuri tunduizi, yaani kuwaongoza wanafunzi kugunduwa wao wenyewe maana ya msamiati husika kwa kutegemea muktadha wa kifungu cha habari kwa ujumla. Si vizuri kupendekeza matumizi ya kamusi kama hatua ya kwanza ya kutoa maana ya msamiati. Kadhalika, maana ya msamiati huweza kupatikana kwa kutumia michoro au picha husika. Vifaa hivi huweza kuandaliwa na mwalimu lakini ni vizuri kuwashirikisha wanafunzi katika zoezi la kuchora michoro kulingana na maana ya msamiati husika. Pia, mbinu ya kutoa kinyume au kisawe cha msamiati husika huwa muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa msamiati.

**(c) Matumizi ya lugha**

Ni wajibu wa mwalimu kuhusisha kifungu cha habari na maisha ya kila siku ya wanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima wanafunzi wapewe kazi zinazostahili kuamsha akili ili kutafuta njia ya utatuzi wa matatizo yanayoweza kuikumba jamii wanamoishi.

**(d) Kusikiliza na kuzungumza**

- Kusikiliza: Wanafunzi wanaweza kukuza uwezo wa kusikiliza kwa njia tofauti: kusomewa kwa sauti kifungu cha habari, kusikiliza habari au hotuba zilizorekodiwa, kusikiliza hadithi au habari kwenye redio, televisheni au tarakilishi. Kwa hiyo, inambidi mwalimu kutumia njia hizi tofauti za kukuza stadi za kusikiliza kwa wanafunzi.
- Kuzungumza: Kuna njia nyingi za kukuza stadi za kuzungumza kwa wanafunzi. Baadhi ya hizi kuna midahalo na mijada, maigizo, uwasilishaji darasani, nyimbo, michezo, mazungumzo, masimulizi, mhadhara, n.k. Katika kazi zake za ujifunzaji, mwanafunzi ashirikishwe kikamilifu katika kazi mbalimbali kwa kuchanganya mbinu zilizotajwa hapo juu.

**(e) Sarufi**

Sarufi inayotarajiwa katika uwezo mahsusi wa mada **haifundishwikamasomo la kujitegemea baada ya mada** bali hujitokeza mwishoni au kati kati ya kila somo. Kwa hiyo vipera vya sarufi hii hujigawa kulingana na idadi ya masomo yanayoiunda mada nzima.

**(f) Kuandika**

Wakati wa kazi zinazofanyika katika makundi madogomadogo, wakati wa maelezo ya mwalimu, wakati wa uwasilishaji wa kazi darasani, wakati wa kutoa muhtasari wa somo na hasa wakati wa majaribio na mitihani au katika kuziandaa kazi za nyumbani, inambidi mwalimu awashirikishe na kuwahimiza wanafunzi kuandika. Pia, mwalimu asisahau imla kwa wanafunzi katika kazi zao za ujifunzaji.

## SOMO LA 1: DHANA YA MDAHALO NA MWONGOZO WAKE

**i) Malengo ya ujifunzaji**

- Kujadili dhana ya mdahalo na mwongozo wake
- Kuandaa mdahalo kwa kuzingatia taratibu zake.

**ii) Zana au vifaa vya ufundishaji**

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za midahalo
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu janja
- Ubao, chaki
- Midahalo iliyorekodiwa
- Vielelezo vya mdahalo
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenye matatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu: Mdahalo kuhusu athari za mavazi ya kisasa**

- ☞ **( Uk.135)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome mdahalo kuhusu athari za mavazi ya kisasa na kujibu maswali ya ufahamu yaliyotokea. Mwalimu awaelekeze kwenye majibu yafuatayo :*

1. Shetani wa mtu ni mtu: ni sawa na adui wa binadamu ni binadamu mwenzake. Methali hii inamaanisha kuwa anayemtendea binadamu mabaya ni binadamu mwenzake.
2. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi.
3. Uzinifu hupoteza utamaduni wa watu na umewafanya wasichana wadogo kujiingiza katika maisha ya kushiriki ngono wakiwa wachanga.
4. Uzinzi na uasherati ni tabia ya kupenda sana kufanya ngono.
5. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi.
6. Yamechangia katika uzinifu kwa kuwa wasichana wadogo wanazini na akina baba waliokomaa.
7. Serikali kupiga marufuku mavazi hayo ya kisasa.
8. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi.
9. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi. Kwa mfano: utumiaji wa dawa za kulevya, shinikizo kutoka kwa marika, umaskini n.k.
10. Mdahalo ni mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi wenye mitazamo tofauti kuhusu jambo fulani wanalozungumzia.

**Matumizi ya msamiati**

**Zoezi la 1 (uk. 136)**

*Katika makundi madogomadogo, waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zilizotolewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo. Matumizi ya kamusi ya Kiswahili sanifu yapendekezwe.*

**Majibu ya msamiati**

1. mdahalo - mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi wenye mitazamo tofauti kuhusu jambo fulani wanalozungumzia
2. uzinifu - tabia ya kupenda sana kufanya ngono
3.

a. wapinzani - watu wanaopinga jambo fulani au maoni fulani

b. hoja - maelezo ya kupinga au kuunga mkono jambo lililokwisha kusemwa

4. kikwazo - pingamizi, kizingiti au kizuizi cha mafanikio au utekelezaji wa jambo fulani
5. maadili - tabia njema na zinazokubalika katika jamii
6. sampuli - muundo wa kitu
7. sugu - -enye tabia isiyoweza kubadilika kwa urahisi
8. vibiritingoma - wanawake malaya
9. uasherati - tabia ya kupenda sana kufanya ngono
10. ushawishi - hali ya mtu kuvutika kutenda jambo fulani

**Mfano wa sentensi:**

1. Leo tutakuwa na mdahalo kuhusu athari za teknolojia ya kisasa.
2. Watu wawili walihukumiwa kwa uzinifu.
3. Katika mdahalo wa jana, upande wa wapinzani ulikuwa na hoja nyingi.
4. Uvivu ni kikwazo cha maendeleo.
5. Mwanafunzi mwenye maadili mema sharti atuzwe.
6. Sijawahi kuona mavazi sampuli hii.
7. Jambazi sugu alifyatuliwa risasi tatu.
8. Yusufu alionekana akizungumza na vibiritingoma kando ya mkahawa.
9. Mungu hapendi uasherati.
10. Nilivutiwa na ushawishi wa mwenyekiti wa kampuni hii.

**Matumizi ya lugha : Sifa bainifu za mdahalo (Uk.136)**

**Tanbihi :** Masomo mawili yanayopatikana katika kitabu cha mwanafunzi , yaani Somo la 16 (Uk. 132 – 140) na Somo la 17 (Uk. 141 – 149) yameunganishwa.

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili : a) sifa bainifu za mdahalo ; b) mwongozo wa mdahalo. Kila kundi liwasilishe matokeo yake ya majadiliano yao mbele ya darasa.*
*Majibu yanayopendekezwa:*

(b) Maana na sifa bainifu za mdahalo :

Mdahalo ni mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mitazamo tofauti.

Zifuatazo ni baadhi ya sifa za mdahalo :

- Mtazamo wa kwanza hutoa hoja zinazotetea au kuunga mkono wazo kuu.
- Mtazamo wa pili hutoa hoja za kupinga au kukataa wazo kuu.
- Washiriki wa mdahalo huwa: mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi pamoja na wasikilizaji washiriki.

(a) Mwongozo wa mdahalo

1. Kabla ya mdahalo kufanyike ni lazima ichaguliwe mada ya kujadiliwa
2. Wanafunzi wapatiwe muda wa kutafuta mawazo kuhusiana na na mada husika ya mdahalo
3. Kuwepo kwa pande mbili za mdahalo. Yaani, upande wa watetezi wa mada na upande wa wapinzani wa mada.
4. Kuwepo kwa mwenyekiti wa kuongoza mjadala
5. Kuwepo kwa mandhari yamdahalo.

**Kusikiliza na kuzungumza**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waigize kuhusu athari za rushwa kwa Wanyarwanda kwa kuzingatia sehemu kuu za mdahalo. Kila kundi liwasilishe maigizo yake mbele ya darasa.*

Maelekezo kwa kazi hii :

Mwalimu aandae kanda yenye mdahalo uliorekodiwa kisha awape wanafunzi fursa ya kuisikiliza. Baada ya wanafunzi kuisikiliza kanda hiyo, awape fursa ya kujibu maswali husika.

**Sarufi : Maana ya nomino**

**Zoezi la 3 (Uk. 137)**

*Katika jozi, wanafunzi wataje aina za nomino wanazozifahamu kisha watoe mifano miwili miwili ya nomino kwa kila aina.*

**Mfano wa majibu :**

1. Nomino za jamii - hutaja vitu au watu katika makundi.

   Mifano: umati, tita, furushi n.k.

2. Nomino dhahania - hizi ni nomino ambazo hutaja vitu vya kufikirika tu.

   Mifano: wema, uchovu, upendo n.k.

3. Nomino za wingi - huonyesha nomino ambazo hupatikana katika wingi pekee.

   Mifano: maji, maziwa, marashi n.k.

4. Nomino za pekee - hizi hutaja mtu, kitu au mahali maalumu.

   Mifano: majina ya watu, majina ya miji, majina ya mito, majina ya lugha mbalimbali, majina ya siku za wiki, miezi n.k.

5. Nomino za kawaida - hujumuisha nomino za makundi ambayo hayabainiki waziwazi. Mifano: kiti, kikombe, mpira n.k.

**Zoezi la 4 (uk. 138)**

*Katika jozi, wanafunzi watunge sentensi mbili mbili sahihi kwa kutumia: a) Nomino dhahania ; b) Nomino za wingi*

**Mfano wa jibu :**

i) Sentensi zenye nomino dhahania:

1) Upendo wake kwa mamake ni wa dhati.
2) Nililala mapema kwa sababu ya uchovu mwingi.

ii) Sentensi zenye nomino za wingi:

1) Marashi yangu yameisha.
2) Yachemshe maziwa ya mtoto.

**Zoezi la 5 (uk. 140)**

*Katika jozi, wanafunzi waunde nomino kutokana na maneno yaliyotolewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia nomino zilizoundwa.*

**Mfano wa jibu**

1. Werevu

   Werevu wa Neza umemfikisha chuo kikuu.

2. Ufagio, mfagizi

   Ufagio wa mfagizi umepotea.

3. Mchoro, mchoraji

   Mchoraji aliyeuchora mchoro wa msitu ametuzwa.

4. Ubaya

   Mbaya ataadhibiwa kwa ubaya wake.

5. Mpenzi, mapenzi

Mpenzi wangu ana mapenzi tele

**Zoezi la 3 kuhusu vivumishi (Uk.146)**

*Katika jozi, wanafunzi wataje aina za vivumishi wanazofahamu kisha watoe mifano miwili miwili ya vivumishi kwa kila aina.*

1. Vivumishi vya idadi kamili: moja, sita, saba, nane n.k
a) Mukamunana alinunuliwa vitabu sita.
b) Nitatumia kalamu sita muhula huu.
2. Vivumishi vya idadi isiyo kamili: chache, nyingi n.k.
a) Niletee maji machache tu.
b) Kurasa nyingi zimeraruliwa.
3. Vivumishi vya sifa: -fupi, -refu, -baya, -zuri n.k.
a) Wanafunzi wabaya wamemwibia mwalimu.
b) Nilipoteza rula ndefu.

**Zoezi la makundi (Uk. 147)**

*Katika jozi, wanafunzi wahusishe kwa usahihi mchoro na picha husika na sentensi sahihi.*

**Jibu :**

A - 5
B - 4
CH - 2
D - 3
E - 1

**Zoezi la 4 (Uk. 149)**

*Katika jozi, wanafunzi waunde vivumishi kutokana na maneno husika kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia vivumishi vilivyoundwa.*

**Jibu :**

1. Mwerevu

   Mwanafunzi mwerevu ametuzwa.
2. Mcheshi
3. Mwanasiasa mcheshi amewasili ukumbini.

   –embamba
4. Uzi mwembamba utatumika kushonea gunia.

   –nene
5. Watoto wanene wametibiwa.

   –dogo
6. Viti vidogo vitakaliwa na watoto.

## SOMO LA 2: DHANA YA MJADALA NA MWONGOZO WAKE

### i) Malengo ya ujifunzaji

- Kujadili dhana ya mjadala na mwongozo wake
- Kuandaa mjadala kwa kuzingatia taratibu zake.

### ii) Zana au vifaa vya ufundishaji

Vifaa vitakavyosaidia mwalimu ni kama:

- Kitabu cha mwanafunzi, Kidato cha sita
- Mwongozo wa mwalimu, Kidato cha sita
- Nakala za mijadala
- Tarakilishi, projekta
- Redio rekoda au simu janja
- Ubao, chaki
- Mijadala iliyorekodiwa

- Vielelezo vya mijadala
- Kamusi sanifu ya Kiswahili
- Mtandao wa intaneti

Tanbihi: Mwalimu anaweza kuandaa vifaa kadhaa viwezavyomsaidia kufanikisha somo lake akitilia mkazo kwenye wale wanafunzi wenye matatizo maalum katika ujifunzaji wao. Hapa inambidi mwalimu awe mbunifu wa vifaa na zana za ufundishaji na ujifunzaji na kuwashirikisha wanafunzi katika kazi hiyo.

**iii) Mbinu za kuongoza kazi za ujifunzaji**

Kazi za ujifunzaji zinatarajiwa kufanyika kwa kutumia mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile kazi binafsi, kazi katika jozi, kazi katika makundi madogomadogo, n.k.

**iv) Majibu ya kazi kutoka kitabu cha mwanafunzi**

**Kusoma na ufahamu:Mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo ( Uk.152)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wasome mdahalo kuhusu umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda na kujibu maswali ya ufahamu yaliyopo. Mwalimu awaelekeze kwenye majibu yafuatayo:*

1. Ni hali au fikira ya mtu kuipenda nchi yake kwa dhati.
2. Kupiga kura huhakikisha kuwa nchi inatawaliwa na viongozi waadilifu.
3. Mzalendo huijali nchi yake, huitetea na kuistawisha.
4. Ni wajibu wa raia kuilinda mipaka ya nchi yake, kuripoti wahalifu na washirika wao na kuepukana na vishawishi vya makundi ya kigaidi.
5. Uzalendo ni nguzo ya mshikamano wa kitaifa na umoja wa wananchi.
6. Anaweza kufundishwa wimbo wa taifa, mila na tamaduni, ushirikiano, kula pamoja na kuheshimu wazee.
7. Uchumi kuzorota, miundo msingi kukosekana na ile iliyopo kudhoofika kufanya gharama ya bidhaa muhimu kuwa ghali.
8. Viongozi wana wajibu wa kuleta amani, maendeleo, umoja wa nchi, kukua kwa uchumi na kustawi katika elimu na miundo msingi.

9. Wimbo wa taifa utawafanya kuipenda nchi, kuthamini uhuru wa nchi yao, historia yao na kutetea umoja wa nchi yao.
10. Mwalimu atathmini namna wanafunzi watakavyoimba wimbo wao wa taifa.

**Matumizi ya msamiati**

**Zoezi la 1 (Uk.153)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waeleze maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi zilizotolewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo kama ulivyotumika katika mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda.*

***Maana ya msamiati :***

1. umeimarika - umekuwa thabiti
2. ari - hamu ya kutaka kufanya jambo bila ya kushindwa
3. utu - hali ya kuwa na tabia nzuri ya kibinadamu
4. bomu - silaha ambayo imetengenezwa ili kutoa mlipuko na husababisha uharibifu mkubwa sana
5. mshikamano - hali ya kuwa na msimamo na ushirikiano katika kutimiza jambo fulani
6. uhalifu - tendo la kuvunja sheria za jamii
7. usalama - hali ya kutokuwepo hatari au fujo
8. dhahiri shahiri - wazi kabisa
9. ufisadi - utumiaji mbaya wa mali ya chama, shirika au serikali
10. miundo msingi - mfumo fulani labda wa ujenzi, uchukuzi n.k.

***Mfano wa sentensi:***

1. Usalama umeimarika katika nchi yetu.
2. Wanafunzi wengi wana ari ya kusoma Kiswahili.
3. Wizi wa kimabavu ni ukosefu wa utu.
4. Washambulizi hao walirusha bomu katika kanisa moja.
5. Wanajamii hawa wana mshikamano wa kuonewa fahari.
6. Vijana wengi wanaotumia dawa za kulevya hujiingiza katika uhalifu bila kujua.
7. Wanajeshi hawa watashika doria ili kudumisha usalama.

8. Ushahidi ulionyesha dhahiri shahiri kuwa mwizi huyo alinaswa na kamera za duka.
9. Viongozi wanaoshiriki ufisadi hawatapigiwa kura tena.
10. Ili kuimarisha miundo msingi yetu, waziri wa uchukuzi ametuahidi mambo mengi.

**Matumizi ya lugha (Uk.153)**

**Tanbihi :** Masomo mawili katika kitabu cha mwanafunzi , yaani Somo la 18 (Uk. 150 – 156) na Somo la 19 (Uk. 157 – 166) yameunganishwa.

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili : a) sifa bainifu za mjadala; b) mwongozo wa mjadala. Kila kundi liwasilishe matokeo yake ya majadiliano yao mbele ya darasa.*

Majibu yanayopendekezwa :

**a. Sifa za mjadala**

- Washiriki wa mjadala huwa: mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi pamoja na wasikilizaji washiriki.
- Baadhi ya sifa za mjadala ni: kuwepo kwa mazungumzo; huhusisha mitazamo mmoja; huhusu mada maalum, mada yenyewe huhusu jamii, n.k.

**b. Mwongozo wa mjadala**

Uandikapo insha ya aina hii, lazima uyazingatie yafuatayo.

- Utangulizi – Utaonyesha msimamo wako. Hivi ni kusema, utaeleza unaunga mkono upande upi.
- Mwili: utatetea uamuzi wako. Hivi ni kusema utaonyesha uzuri wa swala unalounga mkono huku ukionyesha kasoro za swala ulipingalo.
- Tamati: Utasisitiza uamuzi wako wa kuiunga mkono au kupinga hoja husika huku ukiwapatia watu changamoto ya kubadili mawazo yao na kukuunga mkono.

*Katika makundi ya wanafunzi wanne wanne, jadilini kuhusu mwongozo wa kutunga mjadala kwa kuzingatia mambo muhimu yanayofaa kuwepo kwa kurejelea mifano ya mijadala mliyosoma hapo awali. Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake ya majadiliano mbele ya wanafunzi wenzao.*

**Zoezi la 2 (uk. 154)**

*Sikilizeni mjadala uliorekodiwa katika redio kisha katika makundi madogomadogo, wanafunzi:*

*a. wajadili sifa za mjadala huo waliousikiliza darasani.*
*b. waeleze mada ya mjadala huo.*
*c. wajadili hoja zilizotolewa katika mjadala huo*

**Maelekezo kwa kazi hii**:
Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi yao kisha atayarishe kanda yenye mjadala uliorekodiwa na kuwapa wanafunzi fursa ya kusikiliza mjadala. Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi kulingana na maoni yao.

**Kusikiliza na kuzungumza**
*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi waigize mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda. Kila kundi liwasilishe maigizo yake mbele ya darasa.*

*Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuigiza mjadala waliosoma. Ahakikishe kuwa wamezingatia ujasiri wa kusimama na kuigiza mbele ya darasa.*

**Sarufi**

**Zoezi la 3(Uk.155)**

*Katika jozi, wanafunzi watunge sentensi tano tano kwa usahihi kwa kila aina za vitenzi zilizotolewa.Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi na zihusishe vitenzi vikuu na visaidizi. Kwa mfano:*

1. Mwalimu angali anafundisha.
2. Mtoto alikuwa akiimba mama alipofika.
3. Sisi tutakuwa tukicheza uwanjani.
4. Mgeni amekuwa akibisha kwa muda mrefu.
5. Birasa angali anasafiri.

**Zoezi la 4 (uk. 156)**

*Katika jozi, wanafunzi waunde vitenzi kutokana na maneno yaliyotolewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi vilivyoundwa.*

**Mfano wa majibu :**

1. erevuka, erevusha
   Mtoto wake ameerevuka.

2. chosha, choshwa
   Kazi ya kupaka ukuta rangi imenichosha.

3. cheza, chezwa, chezea, chezeka
   Mpira wa vikapu utachezwa kesho.

4. nenepa, nenepesha
   Dawa alizonyweshwa dada yangu zimemnenepesha.

5. fuga, fugwa, fugia, fugika
   Kanga ni ndege anayefugika.

**Uundaji wa viwakilishi (Uk.164)**

Vivumishi vinaweza kutumika kama viwakilishi moja kwa moja katika umbo lao bila kuongezewa viambishi awali au viambishi tamati.

**Kwa mfano:**

- Sentensi yenye kivumishi: Mtoto mkorofi amefukuzwa shule.
- Sentensi yenye kiwakilishi: Mkorofi amefukuzwa shule.

**Zoezi la 4 (Uk.163-164)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi watumie viwakilishi sahihi badala ya nomino zilizotumika katika sentensi zilizotolewa.*

**Jibu:**

1. Kilichoraruka kimeshonwa tena.
2. Ambaye alikuwa akilia amenyamaza.
3. Zote zimefuliwa zikawa safi na kuanikwa.
4. Mangapi yameagizwa kutoka ng'ambo?
5. Yake yamemwagika sakafuni.

**Zoezi la 5 (Uk.164)**

*Katika jozi, wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia vivumishi vilivyotolewa kama viwakilishi.*

Mfano wa sentensi :

1. Mwekundu utatumika kushona nguo yangu.
2. Ndefu imekatika.
3. Safi yatanywewa na wageni.
4. Vyeusi vimepigwa rangi.
5. Vikali vitakata mboga.

## 4.5. MAELEZO NA MAELEKEZO YA ZIADA KUHUSU UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI

### 4.5.1 Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi

***Maelezo ya ziada kwa mwanafunzi ni maelezo ambayo yameandaliwa kuongezea au kukamilisha yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Kwa hiyo, ni lazima yazingatiwe katika ufundishaji wa masomo ya mada hii.***

**Matumizi ya lugha (Uk.136)**

**Mwongozo wa mdahalo**

Unapoandaa mdahalo ni lazima taratibu zifuatazo zizingatiwe.

1. Kabla ya mdahalo kufanyike ni lazima ichaguliwe mada ya kujadiliwa.
2. Wanafunzi wapatiwe muda wa kutafuta mawazo kuhusiana na na mada husika ya mdahalo.
3. Kuwepo kwa pande mbili za mdahalo. Yaani, upande wa watetezi wa mada na upande wa wapinzani wa mada
4. Kuwepo kwa mwenyekiti wa kuongoza mjadala
5. Kuwepo kwa mandhari yamdahalo.

**Matumizi ya lugha (Uk. 157)**

**Mwongozo wa mjadala**

Uandikapo insha ya aina hii, lazima uyazingatie yafuatayo.

- Utangulizi – Utaonyesha msimamo wako. Hivi ni kusema, utaeleza unaunga mkono upande upi.
- Mwili: utatetea uamuzi wako. Hivi ni kusema utaonyesha uzuri wa swala unalounga mkono huku ukionyesha kasoro za swala ulipingalo.
- Tamati: Utasisitiza uamuzi wako wa kuiunga mkono au kupinga hoja husika huku ukiwapatia watu changamoto ya kubadili mawazo yao na kukuunga mkono.

**4.5.2 Maelekezo ya ziada kwa mwalimu**

***Maekelekezo haya yamependekezwa kwa sababu tofauti. Kwanza, yameandaliwa kwa ajili ya kukamilisha au kuimarisha kazi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi. Pili, yamefikiriwa kwa madhumuni ya kubadilisha kazi zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi ambazo zimetathminiwa kutofaa katika nafasi zilimowekwa. Kwa hiyo, ni sharti kwa mwalimu kuchagua kazi anayoiona kuwa ya lazima au muhimu baadhi ya kazi zilizopendekezwa ama katika kitabu cha mwanafunzi au katika kitabu cha mwalimu hiki.***

**Kusikiliza na kuzungumza (Uk.137)**

1. *Kwa kazi ya kipekee, mwanafunzi azungumzie umuhimu wa mdahalo.*
2. *Katika jozi, wanafunzi wakumbuke mdahalo au mjadala mmoja walioshiriki na kujadili taratibu zilizoandaliwa.*
3. *Katika kundi, wanafunzi washirikishwe kwenye midahalo kuhusu mada zifuatazo: Faida au hasara za rushwa; dawa za kulevya; unyanyasaji wa kijinsia, desturi ya kujitegemea, ugonjwa wa Ukimwi, athari za mavazi ya kisasa, n.k.*

**Maelekezo ya majibu kwa kazi hizi :**

1. Umuhimu wa midahalo:

a. Midahalo inaongeza umakinifu, zaidi ya uzungumzaji wa mbele ya hadhira pekee yake

b. Midahalo ni zoezi la ufanisi zaidi kwa wanafunzi kwa ajili ya kufundisha ujuzi wa utafiti.

c. Midahalo inatoa faida nzuri kwa watu wanaoingia kwenye ajira kwenye sekta zote

d. Kuna mahusiano ya wazi kati ya kushiriki kwenye mdahalo na kuongezeka kwenye ujuzi wa kuandika na kusikiliza.

e. Kuna uwiano kati ya kushiriki kwenye mdahalo na kupata nafasi za uongozi kwenye jamii

f. Washiriki wa mdahalo wenye ujuzi wana alama ndogo ya ukali wa sauti kwenye maisha ya kawaida

g. Kufanya midahalo kunapunguza (kwa kama mara tatu) uwezekano wa kuacha shule

h. Kufanya midahalo ni moja kati ya mazoezi yanayopendekezwa na washiriki waliopita. Kiuhalisia, inapendekezwa kwa pamoja na wanafunzi

2. Wanafunzi wawili waongee kwanza kuhusu midahalo waliyohudhuria na kuchagua mmoja wa kujadilia

3. Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi mbalimbali na kuwapatia mada husika na kuongoza midahalo kuhusu mada hizo.

**Matumizi ya lugha (Uk.157)**

*Katika makundi madogomadogo, wanafunzi wajadili : a) sifa bainifu za mjadala ; b) mwongozo wa mdahalo. Kila kundi liwasilishe matokeo yake ya majadiliano yao mbele ya darasa.*

Majibu yanayopendekezwa :

**a. Sifa za mjadala**

- Washiriki wa mjadala huwa: mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi pamoja na wasikilizaji washiriki.
- Baadhi ya sifa za mjadala ni: kuwepo kwa mazungumzo; huhusisha mitazamo mmoja; huhusu mada maalum, mada yenyewe huhusu jamii, n.k.

**b. Mwongozo wa mjadala**

Uandikapo insha ya aina hii, lazima uyazingatie yafuatayo.

- Utangulizi – Utaonyesha msimamo wako. Hivi ni kusema, utaeleza unaunga mkono upande upi.
- Mwili: utatetea uamuzi wako. Hivi ni kusema utaonyesha uzuri wa swala unalounga mkono huku ukionyesha kasoro za swala ulipingalo.
- Tamati: Utasisitiza uamuzi wako wa kuiunga mkono au kupinga hoja husika huku ukiwapatia watu changamoto ya kubadili mawazo yao na kukuunga mkono.

**MAREJEO**


1. BAKITA (2015); *Kamusi Kuu ya Kiswahili*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.
2. Mbaabu I. (1992); *Sarufi ya Kiswahili*; Longman; Nairobi, Kenya.
3. Mdee J.S. , Njogu K., na Shafi A. (2011) *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.
4. Ntawiyanga S. na Kinya J. (2015); *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 2*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.
5. Said A. Mohammed (1980); Riwaya ya *Utengano*; Longhorn; Kenya.
6. Timothy M. Arege (2009); Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*; Longhorn; Kenya.
7. TUKI (2009); *Stadi za Lugha ya Kiswahili*; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
8. Waihiga G. na Wamitila K. W. (2013); *Chemchemi za Kiswahili, kidato cha 3*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.
9. Waihiga G. na Kagwa F. M. (2003); *Darubini ya Kiswahili*; Phoenix Publishers; Nairobi, Kenya.
10. Walibora K. (2002); Riwaya ya *Siku Njema*. Longhorn; Kenya.